# Nipashe

Jumatano Novemba 20, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580080

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Meya wa Chadema Arusha ajiuzulu na kutimkia CCM

UKURASA 3


siasa

Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

Kuhofia hatima mafao kulivyomsukuma 'Ben' kununua ardhi, vitega uchumi

SINTOFAHAMU MITAA

Wachambuzi washukia wanasiasa, waonya hakuna tija kutunisha misuli

Rais mzawa wa Bolivia aikimbia nchi kujihifadhi 'peponi' Mexico

Mkapa asimulia mgogoro Kenya amtaja JK alivyomwengua Ruto Ukurasa 14

UKURASA 13


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MAGUFULI APOKEA UJUMBE MAALUM WA RAMAPHOSA**

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amemhakikishia Rais John Magufuli kuwa matukio ya mashambulizi dhidi...

UKURASA WA 4

**WALIOKOSA MIKOPO ELIMU JUU WAPEWA MATUMAINI**

SERIKALI imesema kuwa wanafunzi waliopunjwa na wale waliokosa mikopo inayotolewa na Bodi...

UKURASA WA 5

**RC AMTUHUMU MBUNGE CCM KWA UCHONGANISHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk Anna Mghwira, amemwonya Mbunge wa Siha (CCM)...

**MKAPA ATOBOA SIRI YA KUMILIKI ARDHI**

UKURASA 15


# MBOWE AUGUA

**ADAIWA** kulazwa hospitalini, hatima ya kina Msigwa, Mdee kujulikana leo...*Endelea ukurasa wa 2*



Distributed via ippmedia

Wabunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Ester Bulaya, Halima Mdee, John Heche na Peter Msigwa, wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Kupanda bei mahindi kwaishtua serikali

UKURASA 2


**MICHEZO** KASEJA AIONA TAIFA STARS AFCON 2021 UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Mbowe alazwa hospitalini

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya kufutiwa dhamana au kuachiwa kwa wabunge wanne wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mbunge wa Iringa mjini, Peter Msigwa na wenzake watatu wanaokabiliwa na kesi ya uchochezi, itajulikana leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Pia mahakama hiyo ilielezwa mshtakiwa wa kwanza ambaye ni Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, hakuwapo mahakamani jana kutokana na ugonjwa na kwamba amelazwa katika Hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam.

Wabunge wengine wanaoshikiliwa katika mahabusu ya Segerea, jijini Dar es Salaam kwa kukiuka masharti ya dhamana na kushindwa kufika mahakamani ni wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Jana mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, ilisikiliza hoja za pande zote mbili wakiwamo washtakiwa na Jamhuri kuhusu utetezi wa kufutwa dhamana yao kwa kushindwa kufika mahakamani.

Mapema, kabla ya kusikiliza hoja hizo, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Joseph Pande, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, Mawakili wa Serikali, Jaqline Nyantori na Salim Msemo, ulidai kuwa mshtakiwa wa kwanza, Mbowe hayupo lakini wengine wanane wapo mahakamani.

Mdhamini wa Mbowe Grayson Selestine alidai kuwa mshtakiwa ameshindwa kufika mahakamani kwa sababu amelazwa Hospitali ya Aga Khan tangu juzi.

Washtakiwa kwa nyakati tofauti waliwasilisha hoja zao wakiomba huruma ya mahakama dhamana zao zisifutwe.

Msigwa alidai kuwa Novemba 15, mwaka huu asubuhi akiwa pamoja na Heche kwenye gari moja, walipata ajali mkabala ya jengo la Dar free Market na kwamba kwa sababu anaiheshimu mahakama, alilazimika kuchukua usafiri wa haraka bodaboda lakini alipofika alichelewa na kesi ilikuwa imeshapigwa kalenda.

"Wadhamini wangu mmoja amesafiri na mwingine amekihama Chama cha Chadema kwa hiyo sina mawasiliano naye, naiomba mahakama isinifutie dhamana," alidai Msigwa.

Mdee akiwasikisha utetezi wake alidai kuwa siku hiyo hakuwa sawa kiafya kutokana na kuumwa na kichwa na kwamba alifika mahakamani lakini alichelewa kesi likuwa imeshaahirishwa.

Wadhamini wake Mdee, kwa nyakati tofauti walidai kuwa mshtakiwa ni mwaminifu na kwamba mahakama isimfutie dhamana.

Heche alidai kuwa ni, mkazi wa Tarime hana makazi jijini Dar es Salaam hivyo hajawahi kuidharau mahakama kuacha kufika kusikiliza kesi yake lakini siku ya tukio alipata ajali akiwa ameongozana na Msigwa ikasababisha wachelewe kufika mahakamani.

Alidai wadhamini wake wote wamesafiri na walishindwa kufika mahakamani kumtolea udhuru na kuiomba mahakama isimfutie dhamana.

Bulaya alidai kuwa Novemba 14, mwaka huu alipata msiba wa mama yake mdogo mkoani Singida, hata hivyo, alimfahamisha mdhamini wake kuhusu msiba huo na kwamba ilikuwa ni lazima ahudhurie mazishi.

Alidai kuwa hajawahi kuidharau mahakama wala maofisa wa pande zote mbili katika kesi hiyo na kuiomba isimfutie dhamana.

Wadhamini wake Bulaya, Martha Charles na Joel Mwakalebela, kwa nyakati tofauti walidai kuwa walishtukia kesi imesha ahirishwa na walifanya juhudi za kufika kwa hakimu kumueleza lakini walijibiwa kwamba uamuzi wa mahakama umeshatolewa.

Wakili wa Serikali, Msemo alidai kuwa upande wa Jamhuri unawasilisha maombi mahakamani wakiiomba kuwafutia dhamana washtakiwa wanne kwa kukiuka masharti ya dhamana.

Alidai kuwa hakuna taarifa yoyote kutoka kwa washtakiwa hao zilizotolewa mahakamani siku ya kesi na kwamba mahakama ipuuze na iwafutie dhamana.

Pia, pamoja na mambo mengine alidai hoja ya Msigwa kudai kuwa mdhamini mmoja ame-

INAENDELEA UK 8

# Kupaa bei mahindi kwaishtua serikali

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imekiri kupaa kwa bei ya mahindi kufikia Sh.107,000 kwa gunia huku ikiwataka watafiti kufanyia kazi suala hilo na kutoa mapendekezo ili kukabiliana na hali hiyo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo, alisema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha uwasilishaji wa taarifa mbili za utafiti kuhusu kuimarisha usalama wa chakula na biashara ya mazao ndani na nje ya nchi uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa masuala ya Kiuchumi na Kijamii (ESRF) kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Afrika (AGRA) na Wizara ya Kilimo.

Alisema utafiti huo ulitokana na kilio kilichokuwapo mwaka jana cha kuzuia uuzaji wa mazao ya chakula hususan mahindi nje ya nchi na kwamba mahindi yanatumika zaidi kwenye nchi za Afrika Mashariki.

"Kitu mnachotakiwa kuangalia kwenye kikao hiki ni bei ya mahindi ambayo imepanda sana kwa sasa. Watu wa mijini wameanza kuzungumzia hili, bei imeshafika Sh. 107,000 kwa mujibu wa takwimu zetu rasmi sasa kulinganisha na mwaka jana bei ilikuwa Sh. 65,000," alisema.


"Bei kwa sasa imepanda hatujui kwa sababu ya nini kwa sababu bei ya juu sana inafikiwa Februari kwa hiyo Februari, mwakani hatuna uhakika bei itakuwa sehemu gani. Kwa hiyo warsha hii pamoja na mambo mengine, ijadili hayo na kutoa mapendekezo namna ya kukabiliana na hali hii," alisisitiza.

Taarifa kutoka kwa waandishi wa mikoa mbalimbali jana zilionyesha kuwa bei ya gunia la mahindi kwa Ruvuma ni Sh. 65,000, Arusha (Sh. 97,000), Kilimanjaro (Sh. 107,000) na Iringa (Sh. 87,000).

Prof. Tumbo alisema kupanda kwa bei hiyo hakutokani na kukosekana kwa chakula, na kusisitiza kuwa chakula kipo.

"Tunaamini mtatoa ushauri mahsusi kwa Wizara ya Kilimo na tutauchukua namna gani twende mbele, hatuwezi kukwepa mahindi kwa kuwa ni zao linalopendwa sana na ni moja ya viashiria vya usalama wa chakula, bado tumefungua mipaka vyakula vinaenda nje na kuingia

INAENDELEA UK 8


Distributed via ippmedia

Rais John Magufuli akipokea barua yenye ujumbe maalum kutoka kwa Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, iliyowasilishwa kwake na Mjumbe Maalum wa Rais huyo, Waziri wa zamani wa Nishati wa nchi hiyo, Jeffrey Radebe, baada ya kuwasili Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Magufuli apokea ujumbe maalum wa Ramaphosa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amemhakikishia Rais John Magufuli kuwa matukio ya mashambulizi dhidi ya wageni nchini Afrika Kusini sio msimamo wa Serikali ya nchi hiyo, na kwamba Serikali hiyo itaendeleza na kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano wake wa kindugu na kihistoria na Tanzania.

Rais Ramaphosa alimtuma Mjumbe Maalum, Jeffrey Radebe, ambaye ni Waziri wa Nchi mstaafu wa Afrika Kusini aliyeongozana na Mshauri wa Rais wa Afrika Kusini katika masuala ya ushirikiano wa kimataifa, Dk. Khulu Mbhatha, kuwasilisha barua yenye ujumbe huo kwa Rais Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam jana.

Katika ujumbe huo, Rais Ramaphosa alifafanua kuwa Afrika Kusini inatambua mchango mkubwa wa Tanzania kwa nchi hiyo wakati wa harakati za kupinga ubaguzi wa rangi na kupigania uhuru ambapo Tanzania ilijitolea kambi na misaada mbalimbali kwa wapigania uhuru.

Katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli alisema Tanzania itaendelea kushirikiana na Afrika Kusini, na kusisitiza ushirikiano zaidi katika maeneo ya biashara na uwekezaji.

Wakati huo huo, Rais Magufuli alikutana na Mjumbe Maalum wa Waziri Mkuu wa Ethiopia ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Hirut Zemene Kassa.

Katika ujumbe huo, Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, alimhakikishia Rais Magufuli kuwa Ethiopia itaendeleza na kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati yake na Tanzania.

Rais Magufuli alisema Tanzania itadumisha na kukuza zaidi uhusiano wake na Ethiopia katika maeneo mbalimbali ikiwamo ushirikiano katika usafiri wa anga.

## HABARI KITAIFA



Ujenzi wa barabara za juu eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam, unaendelea kwa kasi ambapo ukikamilika utarahisisha kupunguza foleni za magari kwenye makutano ya barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Mandela. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Meya wa Chadema Arusha atimkia CCM

**Na Mary Geofrey**

MEYA wa Jiji la Arusha, Kalisti Lazaro (Chadema), amejiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa madai ya kuchoshwa na vitisho vya viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Kutokana na uamuzi wake huo, Lazaro amejiuzulu nafasi zake za udiwani, umeya wa Jiji la Arusha, Uenyekiti wa Mameya na Madiwani wote wa Chadema na ujumbe wa Kamati Kuu ya Chadema.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humprey Polepole, Lazaro alifika ofisi ndogo za chama hicho Lumumba jijini Dar es Salaam akidai kushindwa kuvumilia wakati mgumu aliokuwa anapitia katika utendaji wake wa kazi.

Taarifa hiyo ya Polepole ilidai Lazaro alipokea barua za onyo mara kadhaa kutoka kwa uongozi wa Chadema, wakimtaka kutotoa ushirikiano kwa viongozi wa serikali na kutompongeza hadharani Rais John Magufuli.

Polepole alidai katika taarifa yake hiyo kuwa vitisho vya mara kwa mara ndivyo vimesababisha kiongozi huyo kujivua nafasi zake hizo na kujiunga na CCM.

Polepole pia alidai Lazaro ameeleza kuchukizwa na uamuzi wa Chadema kujitoa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

"Ndugu Lazaro amesema sasa yuko tayari kuchapa kazi ya wananchi akiwa ndani ya CCM na kwamba yupo tayari kwa maelekezo ya kazi kutoka uongozi wa chama hicho," Polepole alidai.

Alisema Lazaro atapokewa rasmi na wanachama wa CCM Mkoa wa Arusha katika tarehe ambayo itapangwa.

# Vigogo Saccos kortini tuhuma za mil. 148/-

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma, imewaburuza mahakamani viongozi watatu wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo Matumaini Saccos wilayani Chamwino kwa kosa la kujipatia kwa njia ya udanganyifu mkopo wa Sh. milioni 148 kutoka Benki ya Uwekezaji (TIB).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa taasisi hiyo, Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema viongozi hao wametenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa sura ya 329 marejeo ya mwaka 2018.

Kibwengo aliwataja viongozi wa saccos hiyo ambao ni Meneja Charles Chilongani (51),Mhasibu Isaya Chigalila (54) na karani Mwanahamis Kaisi (33) ambao wote ni wakazi wa kata ya Msanga Chamwino.

Kibwengo alisema watuhumiwa hao kwa pamoja ndani ya mwaka 2011 na 2013 walichakata bila idhini ya mrajisi wa vyama vya ushirika na kuiwezesha Saccos hiyo kupata bila kustahili mkopo wa Sh. milioni 148 kinyume na matakwa ya sheria ya vyama vya ushirika namba 20 ya 2003 na kanuni zake za 2004.

Alisema watuhumiwa hao walibainika na kosa hilo baada ya Takukuru kujiridhisha na uchunguzi wa kina kubainika kweli wamefanya kosa hilo la udanganyifu na kujipatia fedha hizo za mkopo katika Saccos hiyo.

"Watuhumiwa hawa wanafikishwa mahakamani kwa ajili ya kujibu mashtaka yao,"alisema Kibwengo.

Katika hatua nyingine, alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya mash-

INAENDELEA UK 8

# Magufuli ateua mwenyekiti TMA

**Na Mwandishi Wetu**

Rais John magufuli, amemteua Dk. Burhan Nyenzi kuwa mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Taarifa ilitoyolewa jana na Kurugenzi na Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilisema Dk. Nyenzi ambaye ameteuliwa kwa kipindi cha pili anatoka Tanzania Bara.

Pia taarifa hiyo ilisema Rais amemteua Dk. Makame Omar makame kutoka Zanzibar kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo.

Dk. Makame kwa sasa ni Mhadhiri Mwandamizi wa Jiografia katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

Taarifa hiyo ilimkariri Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, kuwa uteuzi huo ulianza juzi.

Distributed via ippmedia


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NO. 42 MWAKA 2019

ROSE ANDERSON KIDA
(Holding power of Attorney of
ANDERSON NAFTHAL KIDA……………………………………MDAI

DHIDI YA

ROSELINE IAN MOSHI
ABEL NGALLABA
JOSEPH MATHEW MPOKI ……………………………WADAIWA

KUITWA SHAURINI

Kwa:
1. ROSELINE IAN MOSHI
2. ABEL NGALLABA
3. JOSEPH MATHEW MPOKI

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yenu, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinapatikana katika Mahakama hii kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ninyi wenyewe au wakili au mwakilishi wenu anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 11/2/2020 saa tatu kamili (3:00) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Jaji J. A. De-Mello, kujibu madai hayo dhidi yenu. Mnaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo mnatarajia kuvitumia katika utetezi wenu siku hiyo.

ANGALIA: Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa mmepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wenu.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 17 mwezi 10, 2019.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM.

115525102



Dealers in: Land and housing Tribunal; Broker Auctioneers, Bailiff Debt Collections and General Supplies

MCL

MSOLOPA INVESTMENT CO. LTD

NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

Kwa idhini tuliyopewa na MAENDELEO BANK PLC Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapa chini, walipe madeni wanayodaiwa.

Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana(mali) zao kwa mnada wahadhara.

| S/N | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ephraim Simon/Noble E.D.E Engineering and Construction Co.Ltd | Nyumba yenye hati no. 95370, kiwanja No 1242 & 1244, kitalu A Tabata Kisukulu . | 06/12/2019. kuanzia saa 4asubuhi na kuendelea |
| 2 | Titus Lazaro Mgimba/Jenga Quality Animal Feeds Limited | Nyumba yenye hati no. 172182,kiwanja No342,kitalu C Pugu kajiungeni | 07/12/2019,kuanzia saa 5 asubuhi na kuendelea |
| 3 | Betty Matandala/T/A CHLY Traders Investments | Nyumba yenye hati No. 82928, kiwanja No 760, kitalu E, Eneo la Tabata | 06/12/2019. kuanzia saa 6 mchana na kuendelea |
| 4 | Magdalena Cletus Mgombere | Nyumba yenye hati no. 74730,kiwanja no.35 ,kitalu no.1, eneo la Bunju. | 05/12/2019. Kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea |
| 5 | Jadal Enterprises/Yuda Salum Mgavilwa | Toyota Noah T 958 DHJ | 05/12/2019. Kuanzia saa 6 mchana na kuendelea. |
| 6 | Jadal Enterprises /Yuda Salum Mgavilwa | Nyumba yenye hati ya mahuziano iliyopo eneo la Mbezi luis. | 05/12/2019. Kuanzia saa 6 mchana na kuendelea. |

MASHARTI YA MNADA
1. Nyumba zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakaeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei itakayofikia siku ya mnada na 75% katika muda ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hatimiliki, Kutwaa Nyumba/ Kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

KWA MAWASILIANO ZAIDI

MAENDELEO BANK
LUTHA HOUSE
P.O.BOX 216
DAR ES SALAAM
MOB:0688 699 289

MSOLOPA INVESTMENT COMPANY LIMITED
P.O.BOX 40561-DAR ES SALAAM
MOB:0688 332233,0767 666767, 0657 363933,0653 232378

# Mpango aomba ufadhili njia nne Moro- Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ameiomba Benki ya Maendeleo ya Afrika kuipatia Tanzania mkopo nafuu kwa ajili ya kujenga barabara ya njia nne kuanzia Morogoro hadi Dodoma ili kuboresha usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo.

Dk. Mpango alitoa ombi hilo jijini Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) anayewakilisha nchi nane za ukanda wa Afrika Mashariki, Amos Cheptoo.

"Barabara hii ilijengwa muda mrefu miaka ya 1980, malori mengi yanapita hapa kwenda Mwanza, Kigoma na nje ya nchi hasa Burundi na Rwanda na unaona kabisa imeelemewa na imeanza kuharibika," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alimwomba Mkurugenzi Mtendaji waanze kuliweka jambo hilo kwenye miradi itakayogharimiwa na benki hiyo baadaye ili barabara hiyo itakayokuwa na uwezo wa kuelekeza magari mawili kwenda upande mmoja na mengine mawili upande mwingine ijengwe.

"Baada ya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi, tunahitaji usafirishaji kwa njia ya barabara uwe na tija zaidi, uende haraka zaidi lakini pia kupunguza ajali. Hivi sasa kuna ajali nyingi kwa sababu magari yanayokwenda Dar es Salaam na yanayokuja Dodoma au kwenda Mwanza yanapishana kwenye haka kanjia kamoja," alisisitiza.

Cheptoo aliyeko nchini kwa ziara ya kikazi ya siku mbili, alisema benki yake itahakikisha Tanzania inapata mikopo ya miradi yake ya kimkakati na ya kipaumbele ukiwamo huo wa barabara ya Morogoro hadi Dodoma.

Katika hatua nyingine, Cheptoo ameitaka sekta binafsi nchini kuchangamkia fursa za mikopo nafuu zilizoko katika benki hiyo. Alisema sekta binafsi nchini ina nafasi nzuri ya kupata mikopo na utaalam utakaoiwezesha kujikwamua kiuchumi kwa lengo la kutokomeza umasikini katika Bara la Afrika.

"Sekta Binafsi hapa Tanzania haijatumia vizuri dirisha la mikopo ya sekta hiyo ikilinganishwa na nchi zingine za ukanda huu wa Afrika na ninakuomba Waziri wa Fedha na Mipango uihamasishe ikope fedha hizo ili kukuza mitaji yao na kuongeza tija," alisema Bw. Cheptoo

Aidha, alisema AfDB iko katika hatua za mwisho za kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato Dodoma na tayari imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mzunguko mjini Dodoma na miradi mipya ya kuzalisha umeme ambayo iko mbioni kuwasilishwa katika vikao vya bodi ya benki hiyo hivi karibuni.



Ofisa Mkuu wa Uendeshaji Ice Lion General Insurance, Jared Awando (kushoto), akikabidhiwa zawadi na Nacy Mwanyika kutoka East Africa Television/ Radio, baada ya mahojiano katika kampeni ya kibiashara zaidi inayoratibiwa na vituo hivyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: EATV/RADIO**

# Waliokosa mikopo elimu juu wapewa matumaini

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema kuwa wanafunzi waliopunjwa na wale waliokosa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), wataipata kwa sababu kilichokwamisha ni mfumo.

Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, aliyasema hayo jana, huku akiwaeleza wanafunzi hao wenye sifa ya kuipata kuwa fedha zote zilishatolewa wiki tano kabla ya wao kuripoti vyuoni.

Ole Nasha alisema halikuwa kusudio la serikali wala bodi ya mikopo kupunguza fedha hizo, kilichotokea ni mfumo ulijielekeza vibaya.

"Mnafahamu kwa sababu mfumo huu unajiendesha unaweza kuharibika lakini tayari bodi ya mikopo wameandika barua kwa vyuo vyote kuwaambia kwamba lazima kosa hilo lirekebishwe na mwanafunzi yeyote aliyepunjwa fedha zake, atapata mpaka senti ya mwisho," alisema.

Naibu Waziri huyo aliwatangazia wanafunzi wote waliokumbwa na kadhia hiyo kwamba jitihada zinafanyika ili wapate fedha zao kwa sababu moja kubwa, waliingia mkataba.

"Ukikubali upunjwe sasa hivi bado kwenye mfumo wa kurejesha utalipa, hatutaki upate hiyo kadhia, ni mfumo ndio ulileta shida," alisema.

Alisema wiki tano kabla ya vyuo kufunguliwa serikali ilikuwa imeshatoa Sh. bilioni 125 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu, ikiwa ni maagizo ya Rais John Magufuli kuwa hataki wanafunzi wacheleweshewe mikopo.

"Mfahamu fedha zote zimeshatolewa kwa nusu mwaka wa kwanza, wacheleweshaji wanaanzia wanafunzi wenyewe, vyuo, taasisi zetu za udhibiti NACTE (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi) na TCU (Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania) kama hawaendi vizuri bodi ya mikopo haitaweza kwenda mbele," alisema.

Distributed via ipmedia






# BoT yaishauri benki ya Exim

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imeishauri Benki ya Exim Tanzania kuhakikisha inawekeza zaidi katika kutoa huduma maalumu na zenye ubunifu kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ili waongeze nguvu katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi nchini.

Aidha, BoT imeeleza kufurahishwa na jitihada na mafanikio ambayo benki hiyo inayopata katika kujitanua ndani na nje.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Gavana wa BoT, Dk. Bernard Kibesse ,wakati akifungua tawi jipya la benki ya Exim Tanzania katika Mtaa wa Mkwepu jijini Dar es Salaam, baada ya benki hiyo kukamilisha taratibu za umiliki wa iliyokuwa Benki ya UBL Tanzania. Katika uzinduzi huo, Dk Kibesse aliimuwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Philip Mpango.

"Ni fahari kwetu kuona benki ya kizalendo inafanya mambo makubwa kama haya. Mmekuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa mabenki nchini jinsi inavyojizatiti, kujiimarisha ndani na nje ya mipaka ya nchi. Hatua hii ni sawa na kuitikia kilio cha wadau wa huduma za kifedha nchini wanaohitaji huduma zinazokidhi mahitaji yao pia huduma zinazolingana na zile za kimataifa na kwenye mazingira yaliyoboreshwa," alisema.

Alitoa wito kwa benki hiyo kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo wafanyabiashara wadogo na wa kati ili waweze kuongeza nguvu katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi nchini ili kulisaidia taifa kufikia malengo yake ambayo ni pamoja na kufikia pato la kati ifikapo mwaka 2025.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu, alisema hatua hiyo inakwenda sambamba na msimamo wa Rais John Magufuli ambae amekuwa akisisitiza juu ya umuhimu wa kuwa na benki kubwa zaidi na ndogo nchini, kwa kuwa ni hatua muhimu kwa afya ya kifedha katika ukuaji wa uchumi hususani katika kutoa huduma kamili na zenye ubunifu kwa wateja.

"Aidha, ufunguzi wa matawi mapya kama hili utasaidia kuimarisha uwepo wa Benki ya Exim kiushindani katika maeneo mbalimbali ili kutoa kwa urahisi huduma zetu kwa wakazi na wamiliki wa biashara wa maeneo haya."

"Tunafurahi kuwakaribisha wateja wa Benki ya UBL, wafanyakazi na jamii yote ya UBL kwenye familia ya Benki ya Exim. Hatua hii si tu inaongeza uwepo wetu kwenye soko kubwa bali pia inatuongezea timu kubwa ya wafanyakazi wenye weledi katika masuala ya kibenki," alisema.

Alisema Dar es Salaam ni soko muhimu kwa Benki ya Exim na tawi hilo jipya la Mkwepu limeambatana na matumizi ya teknolojia mpya na muundo ambao utawasaidia wateja wa benki hiyo kuwasiliana na maofisa wa benki hiyo kwa njia inayowafaa na katika mazingira ambayo ni bora na salama zaidi.

## HABARI KITAIFA



Wafanyabiashara wa mafenesi wakiwa wameyalundika kando ya barabara jirani na Kituo cha Afya cha Tandale, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, wakati wakisubiri wateja. Fenesi moja linauzwa kwa 2,500/- hadi 6,000/-. **PICHA: JOHN BADI**

# RC amtuhumu mbunge kwa uchonganishi

**Na Mary Mosha, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk Anna Mghwira, amemwonya Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel, kuacha uchonganishi baina ya watumishi wa halmashauri, madiwani na wananchi na badala yake awe kiunganishi ili kuleta maendeleo.

Amesema kutokana na sababu hiyo na zingine, Halmashauri ya Wilaya ya Siha imekuwa nyuma katika ukusanyaji wa mapato na kufikia hatua ya kuwa ya mwisho miongoni mwa halmashauri za mkoani humo.

Dk Mghwira aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo katika sekta za elimu, afya, kilimo, miundombinu na ushirika.

"Sielewi ninyi wenzetu wa Siha mnakwama wapi. Mbunge nimekusikia ukizungumza hapa kuhusu maendeleo ya wilaya yako lakini ninazo taarifa kuwa wewe ni sehemu ya tatizo. Acha kuwachonganisha watendaji wa serikali, baraza la madiwani. Uwe kiunganishi, usiwe ni tatizo," alisema.

Alisema ukusanyaji wa mapato ya serikali za mitaa kwa mwaka 2018/19 kwa baadhi ya halmashauri za wilaya si wa kuridhisha huku wilaya ya Siha ikiwa nafasi ya mwisho kwa kukusanya kwa asilimia 65.

Mkuu huyo wa mkoa alisema makadirio ya mapato kwa mwaka huo ilikuwa Sh. bilioni 19.1 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali lakini hadi Juni, mwaka huu, makusanyo halisi yakiwa ni Sh. Bilioni 17.1 na kwamba Mwanga imefanya vizuri kwa kukusanya Sh. bilioni 3.1 tofauti na makadirio ya Sh. bilioni 3.03.

Kulingana na jedwali la ukusanyaji wa mapato, Siha ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 1.64 lakini ikakusanya Sh. bilioni 1.06 sawa na asilimia 65 ya lengo.

Taarifa ya mkoa inabainisha kuwa halmashauri ya Wilaya ya Moshi inafuata kwa kufanya vizuri baada ya kukusanya Sh. bilioni 2.6 kama ilivyokuwa imepanga ikifuatiwa na Hai iliyokadiria kukusanya Sh. Bilioni 1.2.

Manispaa ya Moshi ilikadiria kukusanya Sh. Bilioni 5.9 na ikakusanya Sh. Bilioni 4.9 sawa na asilimia 84, huku Rombo ikikadiria kukusanya Sh. Bilioni 1.9 na makusanyo halisi yakawa Sh. Bilioni 1.4 (asilimia 740 na Same ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 2.5 na kukusanya Sh. Bilioni 1.7 sawa na asilimia 70.

Akichangia suala la ukuaji wa taaluma, Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema, aliomba serikali kubadili mitaala ya elimu ili kuwafanya wahitimu wa elimu mbalimbali kuwa na uelewa katika kuleta mabadiliko na ugunduzi badala ya kukariri kujibu mitihani.

Alisema mitaala ya elimu iliyopo sasa inamwandaa mwanafunzi katika kusubiri ajira serikalini badala ya kujiajiri na kujitegemea katika kuendesha maisha na kuinua uchumi wa taifa kwa ujumla.

# Muhimbili yajivunia utendaji miaka 4 ya Rais Magufuli

Distributed via ippmedia

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imetumia Sh. bilioni 37.4 kufanya ununuzi wa vifaa tiba na mashine, uboreshaji miundombinu na kujenga uwezo wa wataalamu wake katika miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Uongozi wa hospitali hiyo pia umesema umefanikiwa kuongeza mapato kutoka Sh. bilioni 2.6 kwa mwezi katika kipindi cha miaka minne iliyopita hadi wastani wa Sh. bilioni tano kwa mwezi kwa sasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya hospitali hiyo katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli.

"Katika kipindi cha siku 1,460 tangu Rais Magufuli atembelee Muhimbili na kutoa maagizo kadhaa, tumeshatumia zaidi ya Sh. bilioni 37.4 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali," Prof. Museru alisema.

Alieleza kuwa Rais Magufuli aliagiza waondoe kero zilizokuwapo kwa wananchi zikiwamo za vipimo kutokufanya kazi, hasa MRI na CT-Scan kutokana na kuharibika kwa muda mrefu.

Alisema waliagizwa pia kushughulikia ukosefu wa dawa, wagonjwa waliokuwa wakilala chini kupewa vitanda na kulipa stahiki za wafanyakazi, zikiwamo posho na nauli za likizo.

Prof. Museru alisema waliagizwa kutoa huduma za ubobezi ili kupunguza rufani nje ya nchi, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, kununua na kukarabati vitendea kazi.

Alisema baada ya kufanya maboresho hayo, walifanikiwa kuokoa Sh. bilioni 32 ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi.

> **"Tofauti na miaka ya nyuma, tulikuwa tukitumia Sh. milioni 400 hadi 700 kila mwezi kwa ajili ya dawa za wagonjwa wasiomudu gharama za matibabu," Prof. Museru alisema.**

Alisema huduma zilizoanza kutolewa MNH na kiasi kilichokookolewa kwenye mabano ni upandikizaji wa figo (Sh. bilioni 4.5), upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia (Sh. bilioni mbili), huduma ya mfumo wa chakula na ini (Sh. bilioni 1.3) na huduma ya Radiolojia (Sh. bilioni 24).

Prof. Museru alisema pia wametoa dawa bure kwa wananchi zinazogharimu Sh. bilioni 72 katika miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli, sawa na Sh. bilioni 1.5 kwa mwezi.

"Tofauti na miaka ya nyuma, tulikuwa tukitumia Sh. milioni 400 hadi 700 kila mwezi kwa ajili ya dawa za wagonjwa wasiomudu gharama za matibabu," Prof. Museru alisema.

Mtendaji huyo aliendelea kueleza kuwa kwa mwezi, wanatumia Sh. milioni 600 kutibu wagonjwa wasio na uwezo wa kugharamia matibabu. maarufu wagonjwa wa msamaha.

Kuhusu vikwazo vinavyoikabili hospitali hiyo kubwa zaidi nchini, Prof. Museru alisema ni gharama za matibabu ambazo wananchi wanashindwa kumudu kwa sababu mbalimbali.

"Huduma zote tulizoanzisha za kibingwa ambazo awali zilikuwa zinatolewa nje ya nchi, tunatoza gharama ndogo kwa ajili ya kulipia huduma na siyo kufanya biashara kama ambavyo watu wanadhani. Na ndiyo sababu kuna fedha nyingi tumeziokoa kwa wagonjwa waliokuwa waende nje ya nchi kutibiwa," alisema.

00000000




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa kauli hii, Jaji Mkuu ameona mbali

**KAULI** ya Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, aliyoitoa kwa majaji wapya juzi, akiwataka wasipokee maelekezo ya namna ya kushinikiza kutoa uamuzi wa kesi mahakamani ni ya kitaaluma ikilenga kulinda hadhi ya Mahakama na kusimamia haki kwa ujumla.

Mahakama ni mhimili unaojitegemea, ambao unategemewa na wananchi katika kutoa haki kwa mujibu wa sheria, hivyo kama kuna jaji atafanya kazi, huku akiruhusu kuingiliwa katika kutoa uamuzi, ni kujichafua yeye binafsi na mhimili mzima wa mahakama na tasnia ya sheria kwa ujumla.

Nipashe tumpongeze Jaji Prof. Juma kwa kutolifumbia macho suala hili kwa kuwa majaji hao ni kweli kila mmoja alikuwa na maisha yake kabla ikiwamo marafiki, ndugu, jamaa, majaji wazoefu au wasaidizi wao wa sheria, lakini hawapaswi kuwafungulia milango ya kuruhusu waingilie utendaji wao wa kazi ambao tayari una mwongozo.

Tunamwamini Jaji Mkuu kwa kuwa ni mwanataaluma mbobezi katika sheria, hivyo anayajua mengi ni wazi ametoa wito huo kwa kuwa ushahidi wa mitego, ndipo akawaonya akibainisha kuwa kazi za ujaji ina majaribu mbalimbali.

Miongoni mwa majaribu hayo kwa majaji yanayataja ni kuingilia uhuru wao, hivyo wakatakiwa wapambane na kusimamia katika kufuata viapo vyao.

Inaeleweka kwamba kwa kuwa hii ni taaluma kuna kanuni zinazotoa mwongozo katika utekelezaji wa kazi, miongoni alijizata kuwa zinaelekeza kuwa ofisa wa Mahakama ya Tanzania, analindwa na misingi ya usawa, haki na maadili katika kazi zao kwa kufuata kanuni.

Nyingine, inawataka majaji kujikinga kuingiliwa kazi zao hasa kutoka kwa ndugu, marafiki na hata wenza wao. Kanuni nyingine, inaeleza kwamba kuna mazingira ambayo baadhi ya wana familia wanaweza kujitokeza na kutoa muongozo wa namna ya kufanya kazi zao.

Kanuni ya nyingine, inawakumbusha wasiruhusu watumishi wengine kuonyesha kwamba wako katika nafasi muhimu ya kuathiri kazi zao, zipo zinazohusu uhuru katika kufanya kazi zinaweza wakati mwingine zikasababisha kujitoa kwenye shauri lililopo mbele yako ili ionekane uko huru.

Jaji anatakiwa ajiondoe kwenye kesi inayoweza kuhoji uhuru wake, wanapaswa kusoma maamuzi mbalimbali ya Mahakama Kuu na Rufani, kisha wajiridhishe na kuona umuhimu wa kujitoa.

Miongoni mwa mambo mengine ambayo majaji wanapaswa kuyazingatia ni pale wanapopangiwa majalada ya kesi kuyasoma kwa makini ili kugundua kama kuna maslahi yoyote binafsi.

Wajiridhishe kwa sababu nyingine binafsi zisiingilie majukumu ya kukwamisha uhuru , imani ya dini na mazoea yasiruhusiwe kuingizwa kwenye mwenendo wa kesi hizo na baadae kuhamishia 'hafi' kwenye uamuzi watakaoutoa kama majaji.

Yapo mengi ambayo tunaamini kwamba kulingana na taaluma yao wamejifunza, hivyo wanatakiwa kuyatekeleza ili kuendelea kuijengea heshima taaluma yao,wakikumbuka muda walioutumia kujifunza hayo pamoja na dhamana waliyokabidhiwa.

Tunaamini kwamba kutokana na mwongozo wa kanuni zilizopo ambapo majaji wapya wameelezwa, lakini pia iwe ni nafasi kwa majaji wengine kuzikumbuka na kuzitendea haki kesi wanazoziendesha, huku wakitambua umuhimu wao kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Majaji wakisimamia kwenye mwongozo, kwa vyovyote vile hakuna atakayethubutu kuwaingilia katika utekelezaji wa majukumu yao. Isitoshe, majaji hawana sababu ya kukubali kuingiliwa kwa kuwa kuna utaratibu maalum ambao ni wa mchakato mrefu kuwaondoa katika nafasi zao.

Tunaamini kuwa Jaji Mkuu atakuwa anafuatilia mwenendo wa watumishi wa mahakama wakiwamo majaji na kutoa maelekezo pale anapoona kuna viashiria vya kuingiliwa kwa mhimili huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Vijana siasa hizi haziwi aina hii

Distributed via ippmedia

**VIJANA** ni wadau muhimu katika shughuli zote za kisiasa na maendeleo ya jamii, kutokana na ukweli kwamba wana nguvu na wepesi wanapotumwa katika kutekeleza majukumu, kuliko watu wazima.

Kwa kutambua hilo, wimbi la mageuzi ya kisiasa lilipoibuka mwanzoni mwa miaka ya 1990, katika nchi mbalimbali za Afrika ikiwamo Tanzania, baadhi yao walijitosa katika siasa.

Hatua hiyo ni tofauti na miaka ya nyuma, kwani enzi hizo idadi ya watu wanalioshika nafasi mbalimbali kwenye siasa walikuwa ni watu wenye umri mkubwa, lakini sasa hali imebadilika kufuatia vijana kujitosa huko.

Lakini pamoja na vijana kujitosa, kumewapo ushauri, ambao umekuwa ukitolewa na watu wa kada mbalimbali wakiwataka wasitumike vibaya, katika uchaguzi.

Badala yake wawe mstari wa mbele kuhimiza amani, kwa kuzingatia kwamba wao ndiyo wanaotarajiwa kuwa viongozi wa taifa la kesho, hivyo hawana budi kutumika vizuri.

Kama kweli huwa wanatumika vibaya kwa maslahi ya watu wachache, basi ni vyema sasa wakajiepusha na siasa za aina hiyo, kwani vijana wao ndiyo wanaotegemewa kuwa viongozi wa baadaye.

Siyo vizuri vijana kutumika kufanya vurugu za aina yoyote iwe katika uchaguzi au eneo jingine lolote, bali waandaliwe kuwa viongozi wa taifa la kesho na kuepuka kujiingiza kwenye mambo yasiyofaa.

Tayari ipo kwenye mfumo wa vyama vingi uliorejeshwa nchini mwaka 1992, hivyo vijana wanatakiwa kushindana kwa hoja, huku wakiandaliwa kuongoza nchi, kuliko kutumika vibaya kwenye siasa.

Nikirejea kwenye hoja yangu ni kwamba kampeni za uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa zinaendelea, na Watanzania wanatarajia kuchagua viongozi Jumapili ijayo.

Uchaguzi huo utafanyika kukiwa na sintofahamu, kufuatia baadhi ya vyama vya upinzani kuususia, vikitoa sababu mbalimbali, ikiwamo kutoridhishwa na mchakato wa uchukuaji na urejeshaji wa fomu za kuwania uongozi.

> Siyo vizuri vijana kutumika kufanya vurugu za aina yoyote iwe katika uchaguzi au eneo jingine lolote, bali waandaliwe kuwa viongozi wa taifa la kesho na kuepuka kujiingiza kwenye mambo yasiyofaa.

Pamoja na sintofahamu hiyo, serikali imeshaweka wazi kwamba haimlazimishi wala kumshinikiza mtu yeyote kwenda kupiga kura katika uchaguzi huo.

Kwa upande mwingine ni kwamba asiwapo mtu wa kumzuia mwenzake asiyende kupiga kura, eti kwa sababu chama chake kimesusia uchaguzi huo, bali kila Mtanzania awe huru kushiriki au kutoshiriki.

Bahati mbaya vijana na ndiyo huwa wanadaiwa kutumika katika mchezo huo, ni vyema sasa watafakari kwa umakini na kuacha kutumiwa na wanasiasa kwa ajili ya maslahi ya watu wachache.

Ni vyema kuzingatia kile kilichosemwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwamba jambo la msingi ni kuhakikisha ulinzi, usalama, utulivu na amani vinakuwapo siku ya kupiga kura, na hakuna atakayeshinikizwa wala kulazimishwa, lila mmoja aende kwa hiyari yake bila vurugu.

Msisitizo huo wa waziri kuhusu ulinzi, usalama, utulivu na amani ni vya muhimu kuzingatiwa na kila Mtanzania kwa ajili ya kuhakikisha uchaguzi unafanyika bila viashiria vya uvunjifu wa amani.

Kwa maana hiyo anawataka Watanzania kutumia haki yao ya msingi kwa kujitokeza kushiriki katika uchaguzi huo muhimu wa kuwapata viongozi wa mitaa, vijiji na vitongoji.

Anahimiza hilo, kutokana na ukweli kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 8(1) (a); inayosema, wananchi ndio chimbuko la mamlaka ya utawala wa nchi na kwamba serikali itapata mamlaka toka kwao.

Kwamba uchaguzi ndio njia pekee ya wananchi kukasimisha mamlaka yao kwa viongozi, na ni haki ya kila raia kushiriki katika michakato ya uchaguzi ikiwamo kupiga au kupigiwa kura kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi.

Lengo kuu hapa ni kupata viongozi, hivyo ni muhimu serikali kuhakikisha wananchi wanapata fursa ya kushiriki katika chaguzi huo wa Serikali za Mitaa, na ninadhani ndiyo maana Waziri Mkuu akawahakikishia usalama.

Kwa hiyo, pamoja na sintofahamu iliyojitokeza ya vyama vya upinzani kususia uchaguzi huo, bado wananchi wanatakiwa kwenda kupiga kura kuchagua viongozi bila kuzuiwa wala kulazimishwa.

Dhana ya haki ya kushiriki katika uchaguzi au uongozi ni muhimu, kwani ni haki ya wananchi kushiriki katika masuala yanayohusu uongozi katika nchi yao kwa ajili ya maendeleo.

# Mbowe alazwa hospitalini

INATOKA UK 2

hama chama na hana mawasiliano naye inaonyesha kwamba ana mdhamini mmoja.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa siku ya kesi mahakama ilitoa fursa kwa wakili wa utetezi, Faraji Mangula, kuwaita wadhamini kujieleza kuhusu mahali walipo washtakiwa.

Hata hivyo, hakujitokeza mdhamini yeyote mpaka mahakama ikatoa amri ya kukamatwa washtakiwa.

Mapema Ijumaa ya wiki iliyopita mahakaka hiyo ilitoa hati ya kuwakamata washtakiwa hao kwa kukiuka masharti ya dhamana pamoja na wadhamini wao kwenda kujieleza sababu ya kutotimiza wajibu wao kuwapeleka washtakiwa mahakamani.

Washtakiwa hao wanadaiwa kukiuka masharti hayo kwa kushindwa kufika mahakamani hapo bila kutoa taarifa.

Katika kesi hiyo Mbowe na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia na kuhamasisha hisia za chuki kwa Watanzania dhidi ya serikali.

# Wafikishwa kortini tuhuma kukutwa stika feki za TRA



**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

WATU wawili wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi na kusomewa mashtaka 11 yakiwamo ya utakatishaji, uhujumu uchumi na kukutwa na stika feki za Mamlaka ya Mapato (TRA).

Washtakiwa hao waliofikishwa katika mahakama hiyo jana ni Godfrey Mlangu (28), mfanyabiashara na mkazi wa Kwa Mrombo jijini Arusha na Crispin Malngu (21), mfanyabiashara na mkazi wa Kambi ya Raha jijini Arusha.

Mbele ya Hakimu Mkazi, Julieth Mawole, washtakiwa hao mbali na uhujumu uchumi na utakatishaji, pia walisomewa mashtaka ya kuunda genge la uharifu na kutengeneza pombe feki wakitumia nembo za kampuni nne zinazozalisha pombe hizo nchini.

Pia, walisomewa mashtaka ya kusambaza pombe kali aina ya kiroba iliyopigwa marufuku na serikali.

Washtakiwa walipelekwa mahabusu baada ya kukosa dhamana kutokana na mashtaka ya uhujumu uchumi na utakatishaji yanayowakabili, kuwa na vikwazo kupewa dhamana.

Wawili hao wanadaiwa kukakamatwa wiki mbili zilizopita wilayani Hai mkoani Kilimanjaro baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo kuendesha msako dhidi ya watu wanaojihusisha na utengenezaji na biashara ya pombe feki na fedha bandia wilayani huko.

# Wazibua vyoo hatarini magonjwa ya kuambukiza

**Na Mary Geofrey**

WAONAFANYA kazi ya kuzibua vyoo wapo hatarini kupata magonjwa ya kuambukiza kutokana na kufanya kazi bila tahadhari ya kuwa na vitendea kazi.

Hayo yameelezwa kwenye ripoti iliyofanywa na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Taasisi ya Kimataifa ya WaterAid, ambayo ilizinduliwa duniani kote Novemba 14, mwaka huu.

Ripoti hiyo inaelezea namna ambavyo wafanyakazi wa usafi kwenye nchi zinazoendelea, wamekuwa wakibaguliwa na jamii, kudharauliwa na kuwa masikini, licha ya kutoa huduma muhimu kwa maisha ya binadamu.

Akizungumzia zaidi kuhusu ripoti hiyo jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa Miradi wa Taasisi ya Kimataifa wa WaterAid, Twaha Mbaraka, alisema kutokana na wafanyakazi hao kukosa tahadhari wapo katika hatari ya kuambukiza magonjwa hayo kwa jamii.

Alisema wafanyakazi hao ni wale wa usafi wa vyoo, kutapisha, kuzibua mitaro ya majitaka na kutibu majitaka.

"Wakati kesho (leo), dunia ikiadhimisha siku ya choo, katika ripoti hii tunayozindua leo nchini, inaeleza kuwa watu bilioni mbili hawana vyoo vya kujisitiri. Kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania, wafanya usafi wa kwenye vyoo, hawana vifaa vya kujikinga, wanavunjiwa haki zao za msingi kama binadamu kama kutengwa na kuonekana ni kazi isiyo ya ustaarabu," alisema Mbaraka.

Alisema pia watu milioni 785 duniani mmoja kati ya 10 hawana majisafi na salama karibu na nyumba zao.

Kadhalika, alisema kati ya watoto 310,000 chini ya miaka mitano kila mwaka duniani, wanaugua ugonjwa wa kuhara kutokana na kukosekana kwa maji safi na salama.

Aliendelea kueleza kuwa kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2017/18 nchini India, watu watatu hufariki dunia kila baada ya siku tano kutokana na tatizo hilo la kukosekana kwa vifaa kufanya kazi katika maeneo ya choo.

"Kutokana na kuwapo kwa changamoto hizi, WaterAid, tumeanzisha mpango wa kutoa elimu kwa wafanya usafi wa vyoo ya usafi kwa lengo la kuinua ufahamu wa mazingira wezeshi na kuifanya kazi hiyo kwa weledi na tahadhari," alisema Mbaraka.



Distributed via ippmedia

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, Changwa Mkwanzu (aliyeshoonya mkono), akimueleza jambo Mkuu wa mkoa huo, Gelasius Byakanwa (wa pili kulia), alipofanya ziara ya kutembelea makao makuu ya ofisi za Halmashauri hiyo, katika kijiji cha Mbuyuni jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Juma Satma. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Kupaa bei mahindi kwaishtua serikali

INATOKA UK 2

ndani,"alisema.

Aliwataka watafiti kutengeneza mfumo ambao utatumika kutoa muongozo kitu gani kinatakiwa kufanyika kwa wakati gani.

TANZANIA UCHUMI WA KATI

Katika hatua nyingine, alisema taarifa rasmi ya Benki ya Dunia inaonyesha kuwa Tanzania imeshafikia uchumi wa kati.

"Sasa hivi Tanzania tunachukuliwa kama hatujafikia uchumi wa kati, naomba wataalam wetu mjue kwamba tumeshafikia uchumi wa kati sasa hayo maandishi kuwa tuna mpango wa kufikia uchumi wa kati naomba mbadili. Taarifa rasmi ya Benki ya Dunia imeshasema Tanzania ipo kwenye uchumi wa kati isipokuwa hatujajikita katikati ya uchumi wa kati ndiyo tofauti," alisema.

Alibainisha kuwa kuna wakati Tanzania iliingia uchumi wa kati lakini ikateleza na kwa sasa imerudi tena na kwamba uwezekano wa kuteleza ni mdogo.

# Vigogo Saccos kortini tuhuma za mil. 148/-

INATOKA UK 3

taka ya Taifa mkoa wa Dodoma inatarajia kumfikisha mahakamani Ibrahim Kahogo (43), mkazi wa Area kwa kosa la kughushi na kutoa taarifa za uongo kwa mtu aliyeajiriwa katika utumishi wa umma ikiwamo kutoa nyaraka za uongo kinyume cha sheria ya kanuni ya adhabu sura 16,marejeo ya 2002.

Kibwengo alisema Takukuru ilipokea taarifa ya mtuhumiwa Kahogo Juni 2019 ya kwamba mtuhumiwa akiwa katika ofisi za kamishna wa kazi jijini Dodoma alitumia njia za udanganyifu ili kumuwezesha kuomba na kuchukua vibali vya kufanya kazi kwa wageni ambao wameajiriwa na taasisi ya One Acre Fund mjini Iringa.

"Uchunguzi wetu umethibitisha kwamba mtuhumiwa alighushi nyaraka mbalimbali zikiwamo barua na vitambulisho na kujifanya ni mwajiriwa wa kampuni hiyo na kwamba ana ridhaa yao ya kufuatilia vibali hivyo kwa ajili ya waajiliwa wa kigeni, jambo ambalo siyo la kweli," alisema.

Aidha, alisema kuwa uchunguzi umebaini pia kuwa mtuhumiwa amekuwa mara kwa mara akitumia vitambulisho vyenye picha yake na majina ya watumishi wa taasisi hiyo kudanganya na kumwezesha kupata huduma katika ofisi ya kamishna wa kazi.

HABARI KITAIFA

# Wateja mafuta wapewa neno

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya mafuta ya Total imewashukuru Watanzania kwa kuiamini kwa kununua bidhaa na kutumia huduma zake.

Aidha, imeahidi kuendelea kuwapatia Watanzania huduma na bidhaa zenye ubora.

Kauli hiyo ilitolewa na mkurugenzi wa kampuni ya Total Tanzania, Jean-Francois Schoepp, katika hafla ya kuhitimisha Wiki ya Huduma kwa wateja, jijini Dar es Salaam.

Schoepp aliwashukuru wateja wao nchi nzima kwa miaka 50 ya uwapo wake nchini. "Hili limewezekana kwa sababu ya uwapo wenu na imani yenu kwenye bidhaa na huduma zetu. Tunawathamini sana, tupo tayari kusikiliza changamoto na mahitaji yenu ili tuweze kuwapatia huduma na bidhaa zilizo bora.

Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa wa kampuni hiyo, Marsha Msuya, alisema, aliwaahidi a wateja wake kuwa wataboresha huduma zao kulingana na matakwa ya wateja.

Katika sherehe hiyo, Total pia iliwatunukia vyeti na zawadi mbalimbali wafanyakazi wake walioshiriki kwenye mashindano mbalimbali yaliyoandaliwa na kampuni hiyo.

**Alisema pia safari hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kwani wameweza kuwashawishi wafanyabiashara na watu wengine kutoka China kuja Tanzania kujionea fursa za uwekezaji na kufanya utalii jambo ambalo litaiingizia nchi fedha za kigeni.**

# Watatu kortini tuhuma za utakatishaji mil. 64/-

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

WAKAZI watatu wa Kijiji cha Kalinzi Wilaya ya Kigoma wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma kwa makosa manne ya wizi na utakatishaji fedha wa Sh. 64,182, 322.75 mali ya Kalinzi Organic Coffee Growers.

Washtakiwa ni Charles Hume, Yothani Daniel na Orest Luziro, wote ni wakazi wa Kijiji cha Kalinzi Wilaya ya Kigoma.

Wote kwa pamoja walipandishwa kizimbani juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Gadiel Mariki na walisomewa mashtaka yao walikana makosa yote matatu na wako mahabusu katika gereza la Bangwe kutokana na makosa mawili ya utakatishaji fedha, ambayo hayana dhamana.

Hakimu Mariki alisema washtakiwa wote mtakwenda mahabusu kutokana na makosa mliyoshtakiwa nayo makosa mawili ni ya utakatishaji fedha hayana dhamana.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Mawaliki wawili wa Serikali Shabani Masanja na Raymond Kimbe, walidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ili wakamilishe.

Hakimu Mariki alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Novemba 29, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali Shabani Masanja, alidai kosa la kwanza ni la wizi ambapo Januari 18, mwaka 2012 katika eneo la Benki ya NMB Tawi la Kigoma washtakiwa kwa pamoja waliiba Dola za Marekani 41,488.25 (sawa na Sh. 64,182,322.75) mali ya Kalinzi Organic Coffee Growers.

Alidai kosa la pili ni la wizi ambapo Febuari 7 mwaka 2012, katika Benki ya NMB Tawila la Kigoma washtakiwa waliiba Dola za Marekani 33,191.62 (sawa na Sh. 51,347,436.14) mali ya Kalinzi Organic Coffee Growers.

Alidai kosa la tatu la utakatishaji fedha Januari 18 mwaka 2012, katika Mkoa wa Kigoma washtakiwa kwa pamoja walihamisha Dola za Marekani 41,488.25 kupitia Fund Transfer namba 516FTFX12180002 kutoka kwenye akaunti ya Dola namba 5167300004 kwenda kwenye akaunti ya fedha za Kitanzania namba 5166600015 akaunti zote zilikuwa za Kalinzi Coffee Farmers Group wakati wakijua fedha hizo zimepatikana kwa njia ya wizi.

Aidha, alidai kosa la nne ni la utakatishaji fedha ambapo Febuari 7, mwaka 2012 katika Mkoa wa Kigoma washtakiwa kwa nia ya kuficha uhalifu wao walihamisha Dola za Marekani 33,191.62 kupitia Fund Transfer namba 516FTFX12180002 kutoka kwenye akaunti ya Dola namba 5167300004 kwenda kwenye akaunti ya fedha za Kitanzania namba 5166600015 akaunti zote zilikuwa za Kalinzi Coffee Farmers Group wakati wakijua fedha hizi zimepatikana kwa njia ya wizi.



Distributed via ippmedia

Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Jean Francois Schoepp, akitunuku cheti cha ufanyakazi bora, kwa mtumishi wa kampuni hiyo, Jasmin Malende, wakati wa tafrija mchapalo, kuhitimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja mwisho wa wiki jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Tasaf yamwezesha kijana kuanzisha kiwanda kidogo

**Na Elizabeth Zaya, NJOMBE**

AWARD Juma, mkazi wa Mtaa wa Ramadbania mkoani Njombe, amekuwa kivutio kwa wananchi wa mkoa huo, baada kuanzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza viatu ndani ya nyumba yake.

Kijana huyo amefungua kiwanda hicho baada ya kujiwekea akiba kidogo kidogo baada ya kuingizwa katika mpango wa kunusuru kaya masikini tangu mwaka 2015, unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Akizungumza mbele ya maofisa wa Tasaf waliomtembelea, Juma alisema kabla ya kuingizwa katika mpango huo, alikuwa anaishi katika mazingira magumu, huku akilea wadogo zake wawili ambao alikuwa ameachiwa na wazazi wake ambao wamefariki.

Alisema kazi pekee ambayo ilikuwa inamsaidia kupata kipato ni kuwashonea watu viatu vinavyokatika, ambayo hata hivyo ilikuwa ya kusuasua kutokana na kutokuwa na wateja.

"Mimi sikufanikiwa kwenda shule kutokana na hali ya maisha kutoka kwa wazazi wangu, kwa hiyo nilikuwa naenda kukaa kijiweni kwa mafundi wanaoshona viatu, na kupitia kwao nilianza kujifunza kidogo kidogo mpaka nikaanza kuwashonea watu,"

Aliongeza: "Nilianza kupata pesa kidogo kutokana na kazi hii, japokuwa ilikuwa haitoshi kwa sababu kwa siku nilikuwa na uwezo wa kupata hata Sh.1, 000 mpaka 1,500, lakini niliwapunguzia wazazi wangu mzigo."

Juma alisema baada ya wazazi wake kufariki na kuachwa wadogo zake wawili ndipo maisha yalizidi kuwa magumu na hata chakula chao cha kila siku kuwa kigumu.

"Tulipata shida sana na hawa wadogo zangu, ila Mungu ni mkubwa mwaka 2015 Tasaf kupitia wananchi wa mtaa huu walituona, wakatuingiza kwenye mpango, wakawa wanatupatia Sh.40000 pesa ambayo naweza kusema kwamba huo ndio ulikuwa mkombozi wangu,"alisema Juma na kuongeza:

"Kwa mara ya kwanza nilihakikisha kwamba naitumia pesa hiyo kwa malengo, kwanza kununulia sare za wadogo zangu shuleni, chakula nyumbani na naweka akiba kwa ajili ya kuboresha kibanda changu cha kushona viatu, kila nilipokuwa nikipewa pesa hiyo nilikuwa naweka akiba kidogo kwa ajili ya 'shoe shine'."

Juma anasema ili kuboresha ushonaji wake, mwaka 2017 alianza kwenda kujifunza kwa wamasai namna wanavyotengeneza viatu vyao na kwamba baada yao hapo akaanza kutengeneza mwenyewe.

"Kama mnavyoona hivi ni viatu ambavyo ninatengeneza mwenyewe, niliamua kutumia nyumba hii niliyoachiwa na wazazi wangu, kwa hiyo hiki ndiyo kama kiwanda changu kwa sasa, na watu wengi wanakuja kunishangaa namna ninavyofanya kazi hii wakati hata sijaisomea, naishukuru sana Tasaf kwa hapa iliponifikisha, lengo langu ni kufungua kiwanda kikubwa niajiri na vijana wengine," alisema Juma

Alisema kwa sasa changamoto kubwa aliyonayo ni ukosefu wa soko na kuiomba serikali kumsaidia kumuunganisha na fursa za masoko.

Mratibu wa Miradi ya Tasaf Mkoa wa Njombe, Peter Magema, alisema tayari wako kwenye mchakato wa kumuunganisha na fursa za masoko.

# AfDB yaombwa kuendelea kufadhili miradi barabara

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, ameiomba Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), kuendelee kutekeleza mkakati wake wa ufadhili wa miradi mbalimbali nchini ikiwamo ya barabara.

Aliyasema hayo jijini Dodoma alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo kuhusiana na maendeleo na utekelezaji wa miradi ya barabara inayofadhiliwa na benki hiyo.

"Tunawashukuru AfDB kwa kuwa miongoni mwa wadau muhimu katika kutoa ufadhili wa utekelezaji na uboreshaji wa barabara nyingi nchini, tunaomba muendelee na ufadhili kwani bado tunahitaji kuendelea kuunganisha mtandao wa barabara kati yetu na nchi jirani," alisema Waziri Kamwelwe.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha miaka 11 iliyopita Benki hiyo imetoa zaidi ya Sh. Trilioni mbili kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 1,655 ambapo kati ya hizo kilometa 1,168 zimeshakamilika na 487 zinaendelea kujengwa.

Alitaja baadhi ya miradi ya barabara iliyofadhiliwa na Benki hiyo na ambayo imekamilika kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo ni ukarabati wa barabara ya Arusha - Namanga (km 105), barabara ya Singida - Babati - Minjingu ( km 223.5), barabara ya Iringa - Dodoma (km 260) na barabara ya Namtumbo - Tunduru (km 193).

Ameongeza kuwa miradi mingine ya barabara inayoendelea kutekelezwa kupitia ufadhili wa Benki hiyo ni ujenzi wa barabara ya Tabora-Koga- Mpanda (km 349), barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka kwa Awamu ya II, barabara ya Tanga - Pangani - Bagamoyo (km 246), barabara za mzunguko katika Jiji la Dodoma, na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato jijini humo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa AfDB, Amos Cheptoo, alisema benki yake itaendelea kuunga mkono na kufadhili miradi mbalimbali ikiwamo ya barabara lengo ni kuifanya Afrika kuendelea kiuchumi.

Alisema lengo la kuja kwake Tanzania ni kuangalia utekelezaji wa miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Benki hiyo ili kuona maendeleo yake.



Baadhi ya magari likiwamo la Jeshi la Polisi, Wilaya ya Maetu, mkoani Simiyu, yakiwa yamebeba vyombo kuchota maji kwenye kisima kilichopo katika kijiji cha Mwagwila, nje ya kidogo ya mji wa Mhanuzi juzi, na kwenda kuyagawa kwa wananchi wa mji huo, ambao wamekumbwa na adha ya maji kwa zaidi ya siku 20 sasa. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

## 'Serikali inatambua mchango taasisi dini'

Na Elizabeth Faustine, MWANZA

SERIKALI imesema inatambua mchango wa taasisi za dini katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Kauli hiyo imetolewa na Ofisa Tarafa wa Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Godfrey Mzava, kwa niaba ya Mbunge wa Ilemela, Angeline Mabula, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati wa hafla ya harambee ya ujenzi wa kanisa la EAGT Kata ya Kahama wilayani Ilemela.

Mzava alisema, Serikali inatambua michango ya taasisi za kidini kwa jamii ikiwamo utoaji wa elimu, huduma za afya na kiroho zinazosaidia kuchochea amani, upendo na kupunguza matendo yasiyofaa katika nchi.

"Serikali inatambua mchango wenu katika kuleta maendeleo, niwahakikishie ushirikiano kwa jambo lolote lile mtakaloona linamanufaa kwa watu wetu," alisema Mzava.

Mchungaji wa kanisa hilo, Festo Kwideka, alisema kanisa limekuwa na changamoto ya sehemu nzuri ya kuabudu, hivyo kuanza ujenzi wa jengo la kiasa.

Naye Dorice Merengo akisoma risala, alisema ujenzi unahitaji vifaa mbalimbali na kuwaomba wadau wengine kujitokeza kuunga mkono ili ukamilike kwa wakati.

**"Serikali inatambua mchango wenu katika kuleta maendeleo, niwahakikishie ushirikiano kwa jambo lolote lile mtakaloona linamanufaa kwa watu wetu," alisema Mzava.**

# Kibano kodi kwa wachimba madini

Na Alphonce Kabilondo, GEITA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amewataka wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini nchini vikundi, kampuni inayozalisha madini kulipa ushuru wa huduma ya uwajibikaji kwa jamii na kodi ya huduma.

Biteko alitoa kauli hiyo mkoani Geita wakati akiweka jiwe la msingi kwenye zahanati ya gereza la Wilaya ya Geita inayojengwa kwa ufadhili wa Halmashauri ya Mji wa Geita na Mgodi wa GGML kupitia fedha ya wajibikaji wa makampuni.

Biteko amesema kila mgodi unaomilikiwa na kikundi ,kampuni ambao unazalisha madini unatakiwa kulipa huduma ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii na kodi ya huduma.

Waziri huyo alisema wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini wanatakiwa kutambua kuwa tozo hizo si kwa kampuni kubwa pekee kama GGML bali ni kwa mgodi yote yenye leseni za uchimbaji zinazozalisha madini hayo.

Biketo alisema lengo la serikali ni kuhakikisha mikoa iliyojaliwa kuwa na madini inasongambele kimaendeleo ukiwemo mkoa wa Geita.

"Wamiliki wa leseni za uchimbaji wa madini, kikundi ,makampuni , kila mgodi unaozalisha madini hakikisheni mnatoa kwenye halmashauri husika fedha ya uwajibikaji wa kampuni katika jamii pamoja na kodi ya huduma ya tozo hii siyo kwa kampuni kubwa pekee bali kila mmiliki wa leseni ya madini anaezalisha madini," alisema Waziri Biteko .

Pia waziri huyo amewataka wawekezaji nchini wa sekta ya madini kampuni kuzingatia sheria ya( Local Courntent )kwa kuwapa kipaumbele wazawa katika ajira ,pamoja na biashara .

Awali Mkuu wa gereza la Geita, Mussa Mkisi, akisoma taarifa ya ujenzi wa zahanati hiyo kwa Waziri Biteko, alisema kuwa ujenzi wa zahanati hiyo ulianza mwezi julai mwaka huu ambapo sh. milioni 108 zimetumika kwa hatua ya kwanza .

Mkisi alisema zahanati hiyo ikikamilika itatoa huduma ya ushauri wa kitalaam na vipimo kwa majeshi yote askari polisi ,magereza, wafungwa pamoja na wananchi wote wa Mji wa Geita .

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Leonard Bugomola, alisema Halmasahuri ya Mji imejenga zahanati tatu kupitia fedha ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii kutoka Mgodi wa GGM ambazo zimekamilika kwa asilimia 100 zinasubiri kufunguliwa .

Mbunge wa Geita Mjini, Costantine Kanyasu, alisema Halmashauri ya Mji Geita inatarajia kufungua zahanati mpya tatu zitakazosaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Geita huku akilipongeza jeshi la magereza kwa ujenzi wa zahanati hiyo .

Kanyasu alisema kuwa mwaka 2015 Halmashauri ya Mji wa Geita ilikuwa ikikusanya Sh. bilioni 1.8 kwenye mapato yake ya ndani lakini mwaka 2017 baada ya sheria ya kurekebishwa makusanyo yameongezeka .

## Wanawake 506 waambukizwa VVU

**Na Jaliwason Jasson, KITETO**

WANAWEKE 506 wilayani Kiteto mkoani Manyara wameambukizwa na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) baada ya kupimwa mwaka 2018.

Hayo yalisemwa na Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoani Manyara, Emma Ngatoluwa, wakati akizungumza na viongozi wa dini na wadau mbalimbali wa kupinga ukatili.

Mratibu huyo alisema watoto waliozaliwa na wanawake wenye maambukizi hayo ni 561 na watoto 478 ambao walipewa dawa ya kinga.

"Watoto wanatumia dawa hizi kwa wiki sita hivyo na wakiletwa wana wiki nne hatutawapa dawa kinga maana haitamsaidia,"alisema Ngatoluwa.

Mtaalamu huyo alisema katika Wilaya ya Kiteto, wanawake wanajitahidi kuhudhuria kliniki na kwenda kupima afya zao, hatua ambayo inasaidia kupunguza kiwango cha maambukizi.

Hawa Juma, mkazi wa Babati, aliwashauri wataalamu wa afya kutembelea nyumba za ibada na kutoa ushauri wa kitaalamu na si kusubiri wahusika wawakute kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Naye Joachim Laurent alisema ili kudhibiti maambukizi mapya, elimu na ushauri nasaha vitolewe kwa makundi ambayo ni hatarishi.

Samson Sanka alisema maambukizi hayo yatapungua endapo vijana watapunguza hanasa kwani ndio chanzo cha kichocheo cha maambukizi.

**"Watoto wanatumia dawa hizi kwa wiki sita hivyo na wakiletwa wana wiki nne hatutawapa dawa kinga maana haitamsaidia,"alisema Ngatoluwa.**

# Waziri ataka maofisa mifugo kwenda vijijini

**Na Allan Isack, ARUSHA**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, amewaagiza maofisa mifugo kufika maeneo ya vijijini kwa wafugaji kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa ili kupata malighafi bora zitakazotumika viwandani.

Aliyasema hayo jana alipotembelea mradi wa kiwanda kipya cha kuchakata na kusindika nyama kilichoko Longido mkoani hapa.

Manyanya alisema maofisa mifugo wana wajibu wa kutoa elimu kwa wafugaji wa mbuzi na ng'ombe kufuga mifugo bora na ya kisasa ambayo itatumika kiwandani hapo.

Alisema endapo wafugaji watapewa elimu hiyo, watapata uwezo wa kuzalisha bidhaa bora ambazo zitaleta ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi.

"Nimetembelea kiwanda hiki na nimefarijika sana kujionea ukubwa na ubora wake. Natumaini kiwanda kikikamilika kitaleta ukombozi kwa wafugaji wote nchini ambao watapata fursa ya kuuza mifugo kiwandani hapa," alisema Manyanya.

Alisema kukamilika kwa kiwanda hicho, kitapunguza tatizo la wafugaji kupeleka mifugo nje ya nchi kwa ajili ya kutafuta masoko.

Sambamba na hilo, alisema uwapo wa kiwanda hicho, utaendana na sera ya serikali ya kufikia uchumi wa viwanda, hivyo kuwataka wafugaji kuchangamkia fursa iliyopo kiwandani hapo ili kuinua kipato na kukuza uchumi wa nchi.

Mkuu wa Wilayani ya Longido, Frank Mwaisumbe, alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kupokea ng'ombe 300 mpaka 500 na mbuzi 3,000 kwa wakati mmoja.

Alisema kiwanda hicho kitatoa ajira kwa wananchi wilayani humo kwa kuwa wananchi watauza malighafi zinazotokana na mifugo hiyo zikiwamo pembe, ngozi na kwato.

Mwaisumbe alisema kiwanda hicho pia kitaiongezea serikali mapato kwa kukusanya kodi na tozo mbalimbali.

"Wafugaji kutoka mikoa yote nchini, wataruhusiwa kuleta mifugo yao hapa, hivyo tunawaomba wafugaji wafuge kisasa ili kupata mifugo yenye ubora ambayo itawaongeza kipato kwa kila mfugaji," alisema Mwaisumbe.

Mhandisi wa mradi huo, Ambros Mwangonela kutoka kampuni ya Eliya Food Oversees Ltd, alisema mradi huo utakamilika Machi, mwakani na umegharimu Sh. bilioni 10.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wengine, Lucas Mollel, alisema kiwanda hicho, kitakuwa mkombozi kwa wananchi kwa kuwa watapata soko la uhakika la kuiuzia bidhaa zao.


Distributed via ippmedia

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (katikati), akisikiliza maoni ya wadau wa kilimo mkoani Arusha juzi. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi Kilele cha Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda na Viungo (TAHA), Jacqueline Mkindi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Shule zapewa kompyuta 80 kupunguza ukatili kijinsia

**Na Allan Isack, ARUSHA**

SHULE Nane za sekondari katika Wilaya za Monduli na Ngorongoro Mkoa wa Arusha zimepewa kompyuta ndogo 80 (Tablet), zilizowekewa mfumo maalumu wa kutoa na kupokea taarifa zinazohusu ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Mfumo huo hautakuwa na gharama yoyote kwa watumiaji kwa kuwa utakuwa ukitumiwa bila kuwa na kifurushi cha data.

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, akizungumza wakati wa uzinduzi na ugawaji wa kompyuta hizo katika mji mdogo wa Mto wa Mbu jana, alisema mradi huo unatekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Pastoral Women's Council(PWC), maarufu kwa jina la Tapala.

Alisema lengo la mradi huo ni kuzuia matukio ya unyanyasaji kwa wanawake na wasichana yanayoendelea katika jamii.

Kwitega alisema mradi huo unatekelezwa katika vijiji vinane vya jamii ya wafugaji kwa kipindi cha miaka mitano na unafadhiliwa na shirika la kimataifa la Ubelgiji la Trias.

Alisema shirika hilo lilianzisha mradi huo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi 3,000, walimu 120, viongozi wa mitaa na jamii wanaozunguka shule hizo.

"Ukatili wa kijinsia ni vitendo viovu vinavyozalilisha watu vinavyotesa, vinavyonyanyasa, vinavyokandamiza na havijali haki za kuishi kwa binadamu na ukatili unaweza kufanywa kwa watoto wa kiume au kike," alisema Kwitega.

Alisema utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa ukatili wa kijinsia ni tatizo kubwa linaloikabili dunia kwa sasa hususani katika nchi zinazoendelea.

"Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) katika utafiti wake wa mwaka 2013, takribani asilimia 35 ya wanawake duniani wamefanyiwa ukatili wa kijinsia wa kupigwa au kubakwa katika maisha yao,"alisema.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinakabiliwa na tatizo la ukatili wa kijinsia na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2015/16 kupitia taarifa ya idadi ya watu na afya, zinaonyesha kwamba asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 na 49, wamefanyiwa ukatili wa kijinsia wa aina mbalimbali," aliongeza Kwitega

Mkurugenzi wa Trias Kanda ya Afrika Mashariki, Bart Casier, alisema lengo la mradi huo ni kuungana na serikali katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.

"Mkutano huu ni muhimu sana kwani vita dhidi ya ukatili wa mwanamke na mtoto wa kike si rahisi, kunahitajika kutokomeza matukio haya ili kujenga mpya na yenye kuheshimiana," alisema Casier.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Denis Mgiye, alisema matukio ya ukatili wa kijinsia mkoani hapa kwa takwimu za Julai hadi Septemba, mwaka huu, jiji la Arusha linaongoza kwa matukio 427, Halmashauri ya Arusha DC matukio 371, Meru matukio 93, Monduli matukio 136, Karatu 186, Longido 101 na Ngorongoro 34.





# RTO ageukia shule bubu za udereva

**Na Mary Mosha, MOSHI.**

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Kilimanjaro (RTO), Mrakibu wa polisi (SP) Zauda Mohammed, amesema shule za udereva ambazo hazijasajiliwa mkoani hapa kwa kutokidhi vigezo, zimekuwa zikizalisha madereva ambao ni chanzo kikubwa cha ajali za barabarani.

Akizungumza jana na wamiliki na wakufunzi wa shule za madereva zinazotoa huduma mkoani hapa, RTO Zauda alisema Kilimanjaro ina shule nyingi za udereva lakini ajabu ni kwamba ni shule 17 tu ndizo zilizokidhi na kukamilisha taratibu zote za usajili.

"Kati ya Novemba 12 hadi 15, mwaka huu, ofisi yangu imefanya ukaguzi kwa shule mbalimbali na kukagua magari na madarasa kama yanakidhi viwango ikiwamo suala la ubovu wa magari na alama zote za barabarani katika madarasa wanayotumia.

Katika ukaguzi huo tulibaini kuwa kuna shule nne za udereva ambazo zimekuwa zikitoa huduma pasipo kusajiliwa na zinazalisha madereva wasiokidhi viwango na wamekuwa chanzo kikubwa cha ajali za barabarani," alisema.

Aliongeza kuwa: "Madereva wengi wanaozalishwa kinyemela katika shule za madereva zisizokidhi vigezo wanakuwa bado hawajaiva vizuri na ndio wamekuwa chanzo kikubwa cha ajali za barabarani zinazoepukika."

Mmoja wa wamiliki wa shule za madereva mkoani hapa, ambaye ni Mkurugenzi wa Kilimanjaro Driving School, Cosmas Munuo, alisema mbali na madereva wanaozalishwa na shule bubu ambazo hazijasajiliwa pia waendesha bodaboda na bajaji wamekuwa chanzo kikubwa cha ajali.

Mkufunzi wa madereva kutoka Wide Institute of Driving, Joseph Mallya, aliishukuru ofisi ya usalama barabarani mkoani hapa kwa kuandaa kikao hicho ambacho kimekuwa daraja kwao na wadau mbalimbali wa usafiri na usafirishaji.

"Wito wangu kwenu nyote ni kuuendeleza mshikamano huu uwe endelevu ili kwa pamoja tutokomeze mzimu wa ajali za barabarani hasa katika kipindi hiki tunakoelekea katika sikukuu za mwisho wa mwaka. Katika kipindi hiki, mkoa huu huwa na ongezeko kubwa sana la watu na magari," alisema.



Ofisa Maendeleo ya Jamii, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Mark Masue (kushoto), akiwaeleza walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani humo, jinsi ukatili wa kiuchumi unavyoathiri maendeleo ya wanawake. Walimu hao wanashiriki mradi wa kujengea jamii hamasa juu ya uwepo wa mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili hususani dhidi ya watoto wa kike. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Ahukumiwa miaka 30 kwa ubakaji

**Na Mary Mosha, SIHA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Siha Mkoani Kilimanjaro imemhukumu Peter Shayo (19) mkazi wa kijiji cha Lawate wilayani hapa, kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kumbaka msichana mwenye umri wa miaka 18.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Elibahati Petro wa mahakama hiyo baada ya mshitakiwa kukiri kufanya kitendo hicho kinyume cha kifungu 130(1)(2)(b) na kifungu 131(1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Simon Feo, alidai mahakamani hapo kuwa mshitakiwa alitenda kosa hilo Novemba 7, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi ambapo mshitakiwa na mwathirika walibaki nyumbani wenyewe wakati mwenye nyumba akiwa amekwenda kazini.

Feo alidai kuwa siku ya tukio, mshtakiwa alimfuata mwathirika wa tukio aliyekuwa anakunywa chai sebuleni na kumshika kwa nguvu huku akimpiga na kumvua nguo na kuanza kumwingilia kimwili.

Baada ya kufanyiwa kitendo hicho, aliomba msaada kwa majirani ndipo alipopelekwa hospitalini na daktari alithibitisha kuwa aliingiliwa kimwili.

Upande wa mashtaka ulisema kuwa mshtakiwa ni mkosaji kwa mara ya kwanza lakini kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo na kuonekana kujirudia, uliomba mahakama itoe adhabu kali kwa yeye na wengine wenye tabia kama hiyo.

Hata hivyo, mshtakiwa aliomba mahakama kumpa adhabu ndogo kwa madai kuwa yeye ni yatima pia anategemewa na ndugu zake. Mahakama ilitupilia mbali maombi hayo na kumpa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 30 jela.

Kutokana na mshtakiwa kukiri kosa lake sheria inamzuia kukata rufani kwenye kesi isipokuwa tu kwenye adhabu husika.

## Serikali yapatiwa ushauri uwekezaji

**Na Mary Mosha, MOSHI**

SERIKALI imeombwa kuimarisha ushirikiano baina ya taasisi moja na nyingine ili kuepuka vikwazo visivyo vya lazima, vinavyochangia kuwakatisha tamaa wawekezaji makini.

Kadhalika, taasisi hizo zimetakiwa kuishauri serikali pale inapoonekana kusababisha vikwazo katika utekelezaji wa baadhi ya masuala ambayo hayatengenezi mazingira rafiki katika kukuza uwekezaji.

Meneja Msaidizi wa Marenga Mills, Priva John, aliyasema hayo jana wakati wa mahojiano maalum na Nipashe kuhusu mazingira rafiki ya uwekezaji ili kila upande unufaike na fursa zilizopo.

Aliomba serikali kuwa na ofisi ya pamoja ambayo itamfanya mwekezaji kupata huduma katika taasisi mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Mapato (TRA), Uhamiaji, Idara ya Kazi, Tanesco na Ardhi.

John pia aliomba serikali iangalie namna ya kupunguza mrundikano wa kodi unaowakabili wawekezaji wa ndani hali ambayo inasababisha kukwama kwa wazawa wenye mitaji midogo.

Alisema ikiwa serikali itaona umuhimu wa kupunguza mrundikano wa kodi kwa wawekezaji wazawa utaweza kusaidia kuimarisha thamani za bidhaa wanazozalisha na kuwa na bei nafuu kwa wateja wao.

Mapema mwaka huu, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, aliomba taasisi za umma kuondoa urasimu katika kusaidia wawekezaji kuendesha shughuli zao mkoani hapa na badala yake wafuate sheria.

Mapema Meneja wa TIC Kanda ya Kaskazini, Daudi Riganda, alisema kikao hicho kitaunda kamati ya kusimamia uwekezaji mkoani hapa lakini pia vitafanyika vikao vingine katika mikoa ya Arusha, Tanga na Manyara ili kuwaondolea vikwazo wawekezaji.

Alisema kamati hiyo itakuwa na jukumu la kurahisisha huduma kwa wawekezaji, ingawa aliongeza kuwa hali ya uwekezaji mkoani hapa ni ya kuridhisha licha ya kuwa na changamoto ndogo zinazoshughulikiwa na ofisi za Uhamiaji, Idara ya Kazi na nyinginezo.

Kwa upande wake, mkuu wa Uhamiaji mkoani hapa, Albert Rwelamira, aliomba wawekezaji kufuata sheria ikiwamo kutofika nchini na kuanza kazi kabla ya kukamilisha kwa taratibu ikiwamo kuwa na vibali vya kufanya kazi nchini.

"Linaloleta changamoto ni pale mwekezaji anakuja nchini wakati bado hajapata kibali cha kazi. Sheria inamtaka aombe kibali akiwa huko huko nje ya nchi na akiambiwa vibali viko tayari ndiyo aje. Wale wanaokuja kabla ya kukamilisha hayo ndiyo wanasumbuliwa," alisema.

"Mtu anayeomba kibali cha ukaazi ni lazima awe amepata kibali cha kufanya kazi nchini kwanza. Kama mwekezaji amepata kibali cha kazi na si tishio kwa usalama wa nchi, sidhani kama anaweza kupata usumbufu wowote," alisisitiza.



Ukurasa 19

**Wanawake waja na ilani waanika figisu za uchaguzi**

China kujenga reli kwa manufaa ya Afrika



Ukurasa 17



**Kuhofia hatima mafao kulivyomsukuma 'Ben' kununua ardhi, vitega uchumi**

Ukurasa 15

siasa

JUMATANO NOVEMBA 20, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 20

**Rais mzawa wa Bolivia aikimbia nchi kujihifadhi 'peponi' Mexico**

SINTOFAHAMU MITAA

# Wachambuzi washukia wanasiasa, waonya hakuna tija kutunisha misuli

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI za uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji zimeanza rasmi Jumapili iliyopita ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya kikatiba ya kuchagua viongozi wa serikali za ngazi za vijiji, mitaa na vitongoji na wajumbe mbalimbali.

Lakini, kumekuwa na sintofahamu baina ya CCM, serikali na vyama vya upinzani ambavyo vimeususia uchaguzi huo.

Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaanzisha, kuhalalisha na kutambua umuhimu na kufanyika uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa na vijiji.

Kwa misingi hiyo, ibara ya 146 (2)c ya sheria hiyo kuu ya nchi, inaliagiza bunge kutunga sheria na kuweka taratibu kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi ambao unatajwa ndani ya katiba kuwa ni kwa ajili ya kuendeleza demokrasia na maendeleo ya watu.

Hali ilivy tofauti na vingine, Chama Cha Mapinduzi, kimeshaanza kampeni zake juzi Jumapili Novemba 17, ajenda

**INAENDELEA UK.16**



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo. **PICHA: MTANDAO**

**Mkapa asimulia mgogoro Kenya amtaja JK alivyomwengua Ruto** Ukurasa 14

# Mkapa asimulia mgogoro Kenya amtaja JK alivyomwengua Ruto

Na Mashaka Mgeta



Msuluhishi Benjamin Mkapa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**


Distributed via ippmedia

Makamu wa Rais wa sasa William Rutto.

> Kwenye uchaguzi huo, Raila alishindana kwa karibu na Rais aliyekuwa anamaliza awamu ya kwanza ya utawala wa miaka mitano, Mwai Kibaki wa chama cha Party of National Unity (PNU).

BAADA ya Uchaguzi Mkuu wa Kenya uliofanyika Desemba 27, 2007, taifa hilo liliingia kwenye vurugu zilizosababisha vifo vya maelfu ya raia wake, wengine wakijeruhiwa na kuyahama makazi yao.

Wakenya walishambuliana, waliuana kwa silaha za kijadi na zinazotumia risasi za moto, wengine walichomwa moto. Hali ilikuwa mbaya sana.

Hata hivyo, jitihada za haraka za kulinusuru taifa hilo lenye uchumi mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki zilifanyika kupitia tume ya usuluhishi iliyoongozwa na aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Kofi Annan.

Mstaafu Benjamin Mkapa, wakati huo akiiongoza awamu ya tatu ambaye alikuwa mjumbe katika tume hiyo iliyofanikisha kufikia makubaliano ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Kiongozi wa Orange for Democratic Change (ODM) Raila Odinga akawa Waziri Mkuu.

Kwenye uchaguzi huo, Raila alishindana kwa karibu na Rais aliyekuwa anamaliza awamu ya kwanza ya utawala wa miaka mitano, Mwai Kibaki wa chama cha Party of National Unity (PNU).

Mstaafu Mkapa ameandika kitabu kinachoitwa My Life, My Purpose kinachoweza kutafsiriwa 'Maisha Yangu, Kusudio Langu' ambapo pamoja na mambo mengine, anaelezea ushiriki wake na 'sakata' za mgogoro huo wa kisiasa nchini Kenya.

Sura ya 15 ya kitabu hicho imesheheni maelezo ya Mkapa kushiriki mazungumzo ya upatanishi nchini Kenya na baadaye Sudan Kusini na mashariki mwa Jamhuri Kidemokrasia ya Congo (DRC).

## SIKU 39 ZA KAZI

Anatumia uwanja wa kitabu hicho kueleza mambo na matukio yaliyowakuta katika siku 39 za usuluhishi wa mgogoro uliotokana na vurugu za baada ya Uchaguzi Mkuu wa Kenya, kiasi cha kutishia amani, utulivu na usalama kwenye nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Vurugu hizo zilitokea baada ya Kibaki kutangazwa mshindi wa urais Desemba 27,2007 kwa nguvu kubwa matokeo hayo, yaliyopingwa na Odinga na waliokuwa waangalizi wa ndani na nje wa uchaguzi huo.

Odinga na ODM walikuwa wanapinga ushindi wa kura 4,584,721 (sawa na asilimia 46.42) alizotangaziwa Kibaki dhidi ya 4,352,993 (sawa na asilimia 44.07) za Odinga.

Hivyo ili kupata suluhu ya mzozo huo, 'tume ya Annan' akaundwa na kupata wawakilishi kutoka upande wa Odinga wa ODM na Kibaki wa PNU. ODM iliwakilishwa na Musalia Mudavadi, William Ruto, Sally Kosgei na James Orengo wakati upande wa PNU walikuwapo Profesa Sam Ongeri, Mutula Kilonzo, Martha Karua na Moses Wetangula.

## MAJADILIANO YA SULUHU

Mkapa anasema wajumbe wa ODM na PNU wasingeweza kufikia makubaliano mpaka Odinga na Kibaki walipokutanishwa kwenye chumba, wakiwa na wasuluhishi pekee, akiwamo Graça Machel, mke wa aliyewahi kuwa Rais wa Afrika Kusini, Nelson Mandela, ambaye pia ni mjane wa Rais wa Kwanza wa Msumbiji Samora Machel.

Kabla ya hapo, Mkapa anaeleza kupitia kitabu hicho kwamba ubishani mkubwa kati ya pande mbili hizo ulihusu mshindi halali wa Uchaguzi Mkuu wa Kenya wa mwaka 2007 na kiongozi aliyestahili kutangazwa kuwa Rais.

Anasema haikuwa rahisi kwa ODM kuafiki na kuukubali ushindi wa urais kwa Kibaki.

Mwandishi Mkapa anasema (kama ilivyo kwa vikao vingenevyo vya usuluhishi), kuna wakati walikutana na kila upande na baadaye kuzikutanisha pande zote pamoja.

Anaeleza kwamba pande hizo zilipokutanishwa pamoja, wajumbe wao walijenga hoja kali kiasi cha kumfanya afikirie wangeweza 'kutoana shingo.'

Baadaye, Mkapa, anasema ulipitishwa uamuzi wa kuwaengua wajumbe wawili, Ruto wa ODM na Karua wa PNU kutokana na ushiriki wao usiokuwa wa kuridhisha.

Anasema hatua za kutengwa kwa wawili hao kushiriki mazungumzo ya amani kulitokana na uamuzi uliofikiwa na aliyekuwa Rais wa Tanzania, Jakaya Kikwete.

Anasema kuondolewa kwa Ruto na Karua kutoka kwenye mchakato wa kupata suluhu kuliwezesha kufikiwa makubaliano ya kugawana mamalaka kati ya Kibaki na Odinga.

Mkapa anasema Ruto, wakati huo akiwa ODM na ambaye kwa sasa ni Makamu wa Rais katika utawala wa chama cha Jubilee na Karua aliyekuwa PNU na kwa sasa anaiongoza Narc Kenya leader, walikuwa 'watu wagumu' kufanyakazi nao. Mkapa anasema wakati wa mazungumzo hayo, wawili hao walikuwa wakitoa kauli zenye mrengo wa kuibua taharuki mara kwa mara.

"Hali ilibadilika wakati tulipowapata Kibaki na Odinga pasipokuwapo Karua na Ruto," Mkapa anasema.

Kwa upande mwingine, Mkapa anaeleza kuwa wajumbe wa timu ya usuluhishi kutoka upande wa Kibaki walikuwa wagumu katika mjadala na kufikia makubaliano kuliko ilivyokuwa upande wa timu ya Odinga.

Hata hivyo, gazeti la Sunday Nation lililipowasiliana na Ruto kuhusu hoja hizo za Mkapa, alikaririwa akijibu kwa kifupi, "Kenya imesonga mbele" wakati Karua kwa upande wake amekaririwa akisema, "mwacheni Mkapa afurahi."

Mkapa anaelezea uzoefu wake katika kadhia hiyo iliyotokea Kenya kuwa ni moja ya kazi ngumu ya usuluhishi aliyowahi kupewa nje ya Tanzania.

Mwaka 2000, Mkapa alishughulikia 'mgogoro wa kisiasa' na kufanikiwa kumzuia aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Salmin Amour, maarufu kama Komandoo kuongeza muda wa utawala wake baada ya kuwapo madarakani kwa miaka 10.

## MUSEVENI AMZUSHIA

Mkapa anakumbusha kuwa baadaye Rais Yoweri Museveni, akiwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, alijiunga nao baadaye Januari 2008, ili kusaidia baadhi ya mambo.

Lakini Mkapa anasema, katika hali isiyotarajiwa, Rais Museveni alimtuhumu kwamba anamuunga mkono Kibaki.

Hata hivyo, Mkapa anasema kushiriki kwake mazungumzo hayo muda mfupi baada ya vurugu za Uchaguzi Mkuu zilizotokea Desemba 2007, ulitokana awali kupitia mwamvuli wa Jumuiko la Marais na Wakuu wa Nchi Wastaafu barani Afrika. Mkapa anasema aliyewahi kuwa Rais wa Msumbiji, Joaquim Chissano, alimwita Mkapa na marais wastaafu Quett Katumile Masire Botswana na Kenneth Kaunda wa Zambia na kuwataka wachukue hatua za haraka kabla ya kuharibika zaidi.

Mkapa anakumbuka madhila (taswira) alizoziona kwenye uwanja wa mpira wa Eldoret na Kanisa la Kiambaa ambapo kiasi cha zaidi ya wanawake 40 na watoto walichomwa moto mpaka kufa Januari Mosi, 2008.

"Watoto masikini wasiokuwa na hatia waliuawa na kujeruhiwa. Inahuzunisha. Uhuru una maana gani kwa watu hawa wanaotesaka, waliowapoteza wapendwa wao ama waliojeruhiwa na kuyakimbia makazi yao?," Mkapa anahoji kupitia kitabu hicho.

Anaendelea kuhoji, "Ni namna gani kiongozi anaweza kuyaona haya yakitokea? Ni hali mbaya. Nina Imani hali hii haiwezi kutokea nchini mwangu.".

## KIBAKI Vs ODINGA

Mkapa anasema kwenye kikao kilichowakutanisha Kibaki na Odinga wakiwa na wanasheria wao Amos Wako na James Orengo, wasuluhishi walieleza bayana namna mzozo huo ulivyokuwa zaidi ya 'maji ya shingo' kwao.

"Tulijifungia ndani hadi mwishowe tukapata suluhu. Tuliwasisitizia viongozi hao Kibaki na Odinga kuwa jambo la maana lilikuwa kuheshimiana na kuanzisha uhusiano wa kufanya kazi kwa pamoja..." anaeleza kwenye kitabu hicho.

Mkapa anaongeza kuwa wakati huo, Kibaki na Odinga walitambua kuwa hali ile haipaswi kuendelea kuwapo, hivyo ipo haja ya kutafuta suluhu. Mkapa anasema, hatimaye ilikubaliwa kuundwa serikali ya Umoja wa Kitaifa ikiwa na mawaziri 44 na naibu mawaziri wengi tu.

Mkapa anasema wakati Ruto na Karua waliposikia wanapaswa kushuhudia utiaji saini makubaliano hayo, walikasirika na kusema kulikuwapo njama za kumshawishi Kibaki kukubali.

***0754691540***

# Hatima mafao ilivyomsukuma 'Ben' kununua ardhi, uwekezaji

**Na Ani Jozeni**

RAIS mstaafu Benjamin Mkapa, almaarufu Ben anasema licha ya kuondoka Ikulu na kukabidhi kijiti kwa mrithi wake, hisia ya mafao yanayotolewa kwa marais wastaafu kubadilika siku za mbeleni, ilimsukuma kununua ardhi na kuwekeza.

Mkapa anautaja wasiwasi kuhusu mafao, kuwa pamoja na kwamba marais wastaafu wanapata mafao, alikuwa na hisia kuwa yanaweza kubadilishwa siku za mbeleni na hivyo kumweka yeye na mkewe katika mazingira yasiyotabirika kifedha.

Hivyo , ili kujihakikishia maisha bora ya badaye walijitahidi na mkewe Anna kununua ardhi maeneo mbalimbali na mara kadhaa ilikuwa ni kusaidiwa na marafiki zao au za watu wanaowafahamu kwa kutembelea maeneo kadhaa, kama Lushoto, Kigamboni na Morogoro na kwingineko.

Walinunua ardhi Kigamboni, aidha shughuli ya kufuga huko Bunju aliyotafuta mkewe na kupangisha huku Upanga.

Ndivyo anavyoyosema katika sura ya 15 ya kitabu chake cha My Life My Purpose kuhusu kumbukumbu za maisha yake, kilichozinduliwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.



Mkapa na Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Tonny Bair. **PICHA: MTANDAO**

Distributed via ippmedia

### HAKUNA KUSTAAFU

Katika andiko hilo, Ben anasema hakustaafu kikamilifu na amekuwa akihushishwa na shughuli nyingi za kimataifa, anazozifahamu tangu awali na kwamba hajawahi kustaafu na kutulia nyumbani, ila kinachojiri ni kubadilisha kazi anazofanya.

Mkapa anasema alipata ahueni kubwa alipoondoka Ikulu kama Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu, na ahueni hiyo ikawa kubwa zaidi alipoachia uenyekiti wa chama, akikumbushia kuwa ilikuwa kawaida kwa rais kumaliza muda wake kama mwenyekiti wa chama (hadi uchaguzi wa viongozi katika chama ufanyike wakati wa mkutano mkuu, miaka miwili baada ya uchaguzi mkuu). Anaeleza kuwa mtangulizi wake, Ali Hassan Mwinyi, aliomba amwachie uenyekiti wa chama mara alipochaguliwa kuwa rais, na kwa upande wake, akamwambia mrithi wake Jakaya Kikwete kuwa hatangoja aombwe kuondoka.

Aliamua kuitisha mkutano mkuu maalum wa chama na kumtaka Kikwete achukue uenyekiti. Alipomweleza dhamira yake hiyo alimjibu,'kama ndivyo unavyotaka, sawa,' akabakia mjumbe wa Baraza la Wazee wa CCM ambalo wajumbe wake ni wenyeviti na manaibu wenyeviti wa zamani. Anasema hata hivyo wanakutana kwa nadra sana, hivyo akawa hana nafasi yoyote katika chama mbali ya kuwa mwanachama wa kawaida.

### UJUMBE KAMATI KUU

Mkapa anatoa maelezo yatakayowashangaza baadhi ya watu wanaoona kuwa marais wastaafu kama watu muhimu katika Kamati Kuu ya CCM inayoitwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, wakati kiuhalisia ni kuwa wanaitwa kwa mapendekezo ya mwenyekiti, na siyo wajumbe moja kwa moja.

Hata hivyo wenyeviti wa chama wastaafu wanaonekana ndani ya Kamati Kuu kila wakati, tofauti na makamu wenyeviti wastaafu.

> Alipewa wito huo kwa sababu alikuwa mjumbe wa Tume ya Afrika ikiongozwa na waziri mkuu wa zamani Uingereza, Tony Blair ambayo ilitoa pendekezo la kuundwa kwa mfumo huo, mwaka 2004.

Mkapa katika andiko hilo , anataja pia kuwa watu wamejaribu kumhusisha na siasa za kuelekea uchaguzi mkuu 2015, hasa katika kuchagua mgombea, jambo ambalo hakulipenda hata kidogo.

### ANAKOFANYA KAZI

Mkapa anataja maeneo ambayo aliombwa kuwasaidia mara baada ya kustaafu kuwa ni bodi ya African Wildlife Foundation (AWF) ambako aliyekuwa Rais wa Botswana, Sir Quett Ketumile Masire, alikuwa tayari amejiunga.

Anasema alikubali kuingia bodi hiyo kwani alishawahi kuwa katika bodi ya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), wakati huo, akiwa mhariri wa magazeti ya chama (kabla ya mwaka 1976). Anasema anapenda kutembelea mbuga za wanyama na angefurahi kama angekuwa na muda zaidi, 'na raslimali zaidi' kuweza kutembelea huko mara nyingi zaidi.

Aidha, anasema kuwa alifuatwa pia na wasimamizi wa Club de Madrid ambako viongozi wa nchi tofauti walioko madarakani na waliomaliza muda wao wanabadilishana mawazo, akionekana kuguswa na kina cha ufahamu aliobainisha katika mikutano yao. Anasema alishangaa alikuwa anakosa mengi kwa kutokuwa na muda wa kukutana na watu kama hao akiwa madarakani, akiainisha kuwa ni wazi angekuwa na fursa zaidi za aina hiyo mawazo yake yangekuwa mapana zaidi, apate uelewa sahihi zaidi wa jinsi nchi zinavyokwenda au kubadilika, jambo ambalo si rahisi kujifunza kwa kutenda madarakani.

Akiwa katika Club de Madrid alipata mwaliko wa kuingia katika mradi wa jamii shirikishi kimataifa, 'The Shared Societies Project,' inayotafiti njia za kuhakikisha umoja na mshikamano katika nchi mpya zinazofikia uhuru ambazo zina mtawanyiko wa dini na asili ya jamii za watu wake.

Aliona jinsi Tanzania ilivyoneemeka kufaulu kulinda amani na mshikamano baada ya uhuru. Aliombwa kuwa mwenyekiti mwenza wa 'Investment Climate Facility for Africa,' mfuko wa kuboresha mazingira ya uwekezaji na hivyo kupanuka kwa ajira barani Afrika. Ni uwekezaji katika mipango maalum inayohitaji hakimiliki thabiti.

Alipewa wito huo kwa sababu alikuwa mjumbe wa Tume ya Afrika ikiongozwa na waziri mkuu wa zamani Uingereza, Tony Blair ambayo ilitoa pendekezo la kuundwa kwa mfumo huo, mwaka 2004.

Akizungumzia fikra ya jopo la ICF) (Investment Climate Facility for Africa), anatoa mfano wa kugundua tatizo na kulifanyia kazi, akitumia mfano wa kazi za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Rais mstaafu anaonyesha masikitiko kuwa miradi ya ICF haikufaulu nchini Tanzania licha ya kuwa hapa ndiyo makao makuu ya shirika au mfuko huo.

Sababu kubwa ni kushindwa kupata umiliki halisi wa ardhi unaowezesha mfuko huo kukopesha watu kwa msingi wa kuwa na mali isiyohamishika kama kinga. Ni tatizo ambalo rais mstaafu alikabiliana nalo akiwa madarakani lakini hulka za taasisi na mwelekeo wa kikatiba na kisheria vilimshinda nguvu, kwa mfano alipomkaribisha Profesa Hernando de Soto kuelezea umuhimu wa hatimiliki katika ardhi. Jitihada hiyo haikuwafikia Watanzania (au tuseme wasomi na wapanga sera serikalini) kuelewa umuhimu wa hati ya umiliki na uhuru mpana wa uwekezaji ndani ya kipindi kinachotambuliwa na hati hiyo, kuruhusu mikopo hata kama mtu amepanga bidhaa kando ya barabara, mradi hati ile inampa uhuru wa kubakia hapo bila bughudha kwa kipindi fulani kinachotajwa.

Badala yake wapanga sera wakagundua umuhimu wa hatimiliki ya makazi yasiyo rasmi na kwa upande mwingine, urasimishaji wa biashara ndogo (zikaitwa za wanyonge), ziratibiwe siyo kupata hatimiliki ya muda ya mahali ilipo bali itambuliwe na kulipa kodi, suala likaishia hapo, ndiyo ukaitwa Mkakati wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania Mkurabita).

Baadhi yetu tuliokuwa wakinzani wa sera za utawala wa Rais Mkapa akiwa madarakani tunashangazwa na kina cha kukubali kinagaubaga (ukurasa wa 224) kuwa kusitasita kwa Tanzania kukubali mabadiliko ya sera kuendana na kuwezesha uwekezaji "kunatoa picha ya athari za utamaduni wetu katika maendeleo ya uchumi."

Anaainisha kuwa bado kuna ukungu wa Ujamaa tuliopitia awamu ya kwanza kuwa unatawala mawazo yetu katika kupanga sera, hali inayokwamisha juhudi za kupanua uwekezaji, uwezeshaji wa watu ndani ya nchi na kutoka nje, hivyo fursa kubwa za kimataifa kama ICF zilikwama, hazizai matunda hapa.

Akielezea kuhusika kwake katika mradi muhimu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP) ambalo huunganisha shughuli za mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) nchini, anataja anavyopata taabu kusafiri ambako anahitaji kuwa na msaidizi, mlinzi wake mkuu na wasaidizi wengine wawili wa usalama.

Hata hivyo anaeleza mshangao wake kuwa serikali ya Tanzania inamtaka asafiri pia na ofisa wa protokali kwa safari zake na mikutano, wakati yeye siyo ofisa wa Mambo ya Nje hapa nchini.

Kwa jinsi alivyoeleza, inaelekea anatakiwa kuwa na 'protocol officer' huyo na amlipie kutoka kwa fedha zake na siyo kuwa anaambatanishwa na kulipiwa na serikali. Anaona kama mzigo na taabu isiyohitajika.

# Wachambuzi washukia wanasiasa, waonya hakuna tija kutunisha misuli



Kiongozi Mkuu wa ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe.



Distributed via ipinmedia

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe.

**INATOKA UK.13**

kuu ikiwa ni kuzungumzia mafanikio ya serikali ya katika kipindi cha miaka mine iliyopita. Hilo ni jambo jema na hakuna anayelipinga.

Hata hivyo, kutokana na sintofahamu iliyoletwa na vyama vya upinzani kususia uchaguzi huo, unaotarajiwa kufanyika Jumapili ijayo ni wazi kuwa haitoshi kukaa kimya bila wapinzani CCM na serikali kurekebisha mambo.

Hii ni kwa sababu mkwamo huo unatishia mustakibali wa taifa kisiasa.

Baadhi ya wadau wanaozungumza na Nipashe wanasema ni lazima CCM, wapinzani na serikali kumaliza mkwamo huo na kuwezesha kufanyika uchaguzi kwa mujibu wa sheria na taratibu hata kama siku ya kuchagua viongozi hao ni Jumapili ijayo.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata), Hebron Mwakagenda, anasema ni lazima wahusika hawa wakuu wakutane wajadiliane na kupata suluhu.

Anasema kuwa katika siasa kila jambo linazungumzika hivyo, hakuna sababu ya kuendeleza sintofahamu hiyo iliyoanza mara baada ya vyama vya upinzani kususia uchaguzi kwa madai kuwa havijatendewa haki, haina tija kwa nchi.

"Nashauri tuyazungumze tuokoe taifa letu, ni wito wa Jukata kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa -Tamisemi, vyama vya upinzani na CCM tuamue juu ya mustakabali wa nchi yetu." Anashauri Mwakagenda.

Anaeleza kuwa katika hili la mkwaruzano wa kususia uchaguzi wa serikali za mitaa hakuna mshindi na kwamba kutunishiana misuli ni kuikwamisha nchi na hakuna atakayenufaika.

> Nashauri tuyazungumze tuokoe taifa letu, ni wito wa Jukata kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa –Tamisemi, vyama vya upinzani na CCM tuamue juu ya mustakabali wa nchi yetu.

Anawakumbusha wahusika wakuu kuwa kuendelea na sintofahamu hiyo kunaliumiza taifa na hakuisaidii CCM wala upinzani popote hivyo warudi kwenye meza ya mazungumzo na kumaliza mkwamo.

## MASWALI NI MENGI

Mwanasheria na wakili wa kujitegemea Edson Kilatu, anasema suala hili linaacha maswali mengi na linahitaji maelezo ya kutosha kutokana na sababu mbalimbali zilizotolewa kwenye kuwaengua wagombea wa upinzani waliotaka kushiriki kwenye uchaguzi huo wa serikali za mitaa na vijiji.

Anasema hoja ambayo Tamisemi inayosimamia uchaguzi huo, itatakiwa kuitolea maelezo katika mchakoato wa kupata ufumbuzi wa mkwamo huo, ni pamoja na hili, kama watu wengi waliojitokeza wanashindwa kujaza fomu kikamilifu kutokana na kushindwa kuelewa maelezo, ni wakati wa kuchunguza kuna tatizo gani kubwa hivyo ndani ya fomu hizo?

"Lakini sifa mojawapo ya uchaguzi huu wa serikali za mitaa ni mgombea kufahamu kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza. Ni kigezo kimojawapo kikubwa, sasa kama ndivyo miongozo, taratibu na sheria za uchaguzi zilitakiwa kuwa rafiki kiasi cha kutokumfanya mwenye sifa za kawaida akapoteza sifa za kushiriki na kuenguliwa kirahisi kama ilivyotokea," anasema Kilatu.

Anafafanua kuwa kama sifa ni kusoma na kuandika inakuwaje mgombea ananyimwa nafasi kwa sababu ya upungufu mdogo kama pengine kukosea herufi ya jina lake.

Kama anaitwa 'Asifiwe' akaandika 'Asifwe', halikutakiwa kuwa jambo la kumkosesha nafasi hiyo kwa sababu cha msingi ni pamoja na kujua kusoma na kuandika na hana elimu ya kiwango cha juu.





Mwenyekiti wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba (kushoto). Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi James Mbatia.

Anataja baadhi ya madai yanayotolewa na wagombea wa upinzani kuwa wameenguliwa kwa madai kuwa wamejiandikisha mara mbili.

Kilatu anashauri kuwa hili nalo kuna haja ya kulitazama kwasababu hakukuwa na udhibiti wakati wa kuwaandikisha wagombea hao wala wapigakura wengine wote.

Mwanasheria huyu anaonya juu ya kubadilisha kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa kila wakati na kuchelewa kuzitoa kwa wadau wakiwamo vyama vya upinzani kuwa ni tatizo linaloibuliwa na wanasiasa.

Anasema mabadiliko ya mara kwa mara ya kanuni huenda hayatoi nafasi kwa wagombea kueleweka na kwamba hata mwaka huu suala la kucheleweshwa kanuni hizo lililalamikiwa na wadau hasa wapinzani.

"Kwa mfano mwaka 2014 kulikuwa na kanuni za wakati huo. Mwaka huu kuna kanuni za 2019. Swali la kujiuliza hivi kanuni hizo zilizotolewa miezi michache kabla ya kuchukua fomu na kugombea washiriki walizielewa? Tanzania ilivyo tujiulize hivi kuna uwezekano wa washiriki wetu huko vijijini, vitongojini wakazielewa kweli?" anahoji.

Hata hivyo, anaihoji Tamisemi kuwa pamoja na kuandaa kanuni hizo na kuzitoa miezi mitatu kabla ya uchaguzi ilifanya jitihada zozote kuwawezesha wadau kuzielewa? Ilitolewa elimu ya uraia kuwasaidia wagombea hao?

## UWAZI

Mwanasheria huyo anashauri kuwa masuala ya uchaguzi yanahitaji kufanyika kwa uwazi zaidi hasa kwenye kufahamu kanuni, haki na vigezo kwa wagombea, kuwapinga au kuwawekea mapingamizi inapohitajika kufanya hivyo.

"Wagombea wa upinzani ambao wamekataa kushiriki kwenye uchaguzi huo wanalalamikia mapingamizi wakisema kwa mfano kuwa inakuwaje kuweka pingamizi wakati fomu za wanaowapinga hazijawekwa wazi au kuonekana hadharani."

Kilatu anaona kuwa ni jambo linaloweza kuzua maswali kuwa unampingaje mgombea ambaye huna taarifa zake? Unapata wapi fomu ya mgombea huyo wakati haijaonekana kwenye ubao wa matangazo au hadharani?

Anaonya kuwa masuala kama hayo yanachangia kuufanya uchaguzi huo kulalamikiwa kuwa hauendi kwa utaratibu wa uwazi na kusababisha kuacha maswali mengi yanayosababisha kuususa.

Suala jingine ambalo wagombea hawa wanalilalamikia ni eneo la kukosekana utaratibu wa kuandika taarifa na kusaini pale mgombea anapowasilisha fomu.

> Kwa mfano mwaka 2014 kulikuwa na kanuni za wakati huo. Mwaka huu kuna kanuni za 2019.

Anasema wagombea wanaolalamika wanasema baadhi yao baada ya kukabidhi fomu hizo waliondoka lakini hawana ushahidi kwa vile hakuna sehemu ya kusaini na kuweka taarifa na kumbukumbu rasmi kuhusu kuwasilisha na kupokea fomu hizo.

Viongozi wa upinzani walitangaza kujitoa kwenye kinyang'anyiro hicho baada ya kulalamikia kuchezewa rafu kwenye kuchukua na kurejesha fomu.

Walidai wagombea wao wakati wa kurejesha fomu walifungiwa milango na baadaye kuambiwa muda umekwisha na kufanyiwa mambo ambayo walidai zaidi ya asilimia 80 ya wagombea wake (Chadema) wamekatwa.

Mwisho

# China yaahidi kujenga reli kwa manufaa ya Afrika



Muhandisi akiongoza treni ya kisasa Jijini Nairobi. **PICHA: MTANDAO**

**NAIROBI,** Kenya

BAADA ya uzinduzi wa awamu ya pili wa ujenzi wa reli nchini Kenya iliyotarajiwa kuendelezwa hadi mpaka wa Kenya na Uganda eneo la Malaba , kulikuwa na hofu huenda uzinduzi huo ukawa mwisho wa mradi mkubwa zaidi baada ya China kudaiwa kuwa wamekataa kuufadhili.

Kufuatia fununu hizo, BBC ilifanya mahojiano na Balozi wa China nchini Kenya, Wu Peng, kuhusu msimamo wao katika mradi huo.

"Tunaamini kuwa ujenzi wa reli kutoka Naivasha mpaka Kisumu utaweza kuinua hali ya uchumi ya Kenya na kuwa kituo cha biashara cha Afrika Mashariki."

Aliendelea:" China itaendelea kuwaunga mkono katika jitihada zote za kukamilisha reli hiyo.Hatujabadili mawazo yetu katika uwekezaji wetu na wala kutokuwa na imani na hiki kinachoendelea kwa sababu ujenzi huu una manufaa makubwa kwa bara la Afrika".

Balozi huyo aliongeza kuwa China imejizatiti katika uwekezaji huu na vilevile inaheshimu maamuzi ambayo serikali ya Kenya inayatoa katika miradi yake.

"Tunaamini kuwa Kenya inaweza kufanya maamuzi mazuri kwa kuzingatia uchumi wake na fedha zilizopo, ila kile ambacho ninachoweza kusema ni kuwa kwa upande wa China na upande wa Kenya zinafanya kazi kwa pamoja ili kuzindua hatua inayofuata ya ujenzi huo."

Balozi Wu Peng, alibainisha kuwa wanafanyia kazi ufadhili wa ujenzi huo ingawa kila kitu kina utaratibu.

Alithibitisha kuwa China, haina mpango wowote wa kumiliki mali yoyote ya taifa la Kenya kwa kile wanachokifanya.

Tofauti na uzinduzi wa reli ya kutoka Mombasa hadi Nairobi, ilivyozinduliwa kwa mbwembwe mwaka 2017, uzinduzi wa reli hii mpya haujapewa umuhimu mkubwa.

Wachambuzi wanasema serikali inakabiliwa na wakati mgumu kuelezea faida za kiuchumi za mradi huo kwa sababu baadhi ya vituo havina shughuli nyingi katika mkoa wa bonde la ufa.

Mpango wa kuendeleza ujenzi wa reli hiyo hadi Kisumu, kupitia Ziwa Victoria, hadi Uganda umekatizwa na hatua ya China kujiondoa katika ufadhili wake.

Katika kongamano la viongozi wa Bara la Afrika na China jijini Beijing, China ilisema itafadhili miradi iliyo na manufaa ya kiuchumi pekee. **BBC**

# Prof. Mukandala na simulizi Ben Mkapa tangu 'kadogoo'

## • Upishi nyumbani; shuleni 'tatu bora' wa 'kudumu; kazini 'alimkosha' Nyerere

Na Romana Mallya

WASWAHILI wana usemi 'mbuyu ulianza kama mchicha' na 'ukiona vinaelea, vimeundwa.' Vyote vinabeba maana kubwa kwa maisha ya Rais mstaafu Benjamin Mkapa, ambayo hadi sasa kuna joto kubwa la simulizi ya maisha yake.

Ni msisimko unaoanzia kitabu alichoandika 'My Life, My Purpose' na kuizindua alipotimiza umri wa miaka 81, tarehe 12 ya mwezi huu.

Makamu Mkuu mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Rwekaza Mukandala, ana simulizi ya Rais mstaafu Mkapa alikochipukia hadi kung'ara leo, mithili ya dhahabu ya kisiasa, ambayo ndiyo ilikuwa jukumu lake katika sherehe za uzinduzi.

Akichambua maisha ya utotoni, anasema Rais mstaafu Mkapa, alifundishwa kupika chakula na mzazi wake, Mama Stephania akiwa mdogo.

Baba yake, Mzee Matwani alikuwa Mpishi Msaidizi katika Misheni ya Ndanda na alibeba ndoto ya mwanawe kama ilivyo kwa kila mzazi, pindi atakapomaliza masomo ama awe padre, daktari au mwalimu.

Anasema, ndoto za mzazi wake, Mzee William Matwani, ziliyeyuka na kuishia katika siasa.

Prof. Mukandala anasema:"Alipokwenda shule iliyopo kijijini Lupaso, Ndanda na hatimaye St. Francis Pugu na (Chuo Kikuu) Makerere, huko alijifunza kupika, kufinyanga, kubuni na kuchambua mawazo na kuyaweka sawa kama msomi mbunifu na mwandishi."




Rais mstaafu, Benjamin Mkapa.

### WAZAZI WAKE

Prof. Mukandala anasema Mzee Matwani akiwa mpishi msaidizi, Wamisionari walimbatiza na wakamfundisha kusoma, kuandika na kuhesabu na kumfanya Katekista.

"Mama hakuwa na muda wa kujifunza kusoma na kuandika, kwani yeye ndiye alikuwa msingi wa familia, akihakikisha analima, kulisha familia, na kuwalea watoto.

Mkapa anasema, wamisionari walimpeleka baba yake Lupaso alikoeneza dini na kufundisha shule za kienyeji au 'Bush School' zao.

"Alikuwa mkali, lakini msikivu na mpenda haki. Wazazi hawa ndio vinara wa sehemu hii ya kwanza ya simulizi hii. Waliishi pamoja kwa uadilifu na heshima kubwa, na mapenzi ya pamoja kwa watoto wao,' anasema Prof. Mukandala, aliyesisitiza kwamba ingawa wazazi hao hawakwenda shule, walipenda watoto wao wote wasome.

"Pamoja na kwamba mzee Matwani alikuwa na kipato kidogo lakini cha uhakika kila mwezi, kilifanya familia ionekane iko tofauti. Hii ilisababisha wivu na hatimaye chuki kutoka kwa jamii.

"Wivu huu na chuki ulisababisha tukio moja baya ambalo Mkapa analikumbuka kwa uchungu. Mwaka 1947, kulitokea ukame mkali basi watu wakamleta mganga wa kienyeji akaamua kuwa mama mzazi, mama yake na bibi yake ndio walikuwa wameloga na kuzuia mvua.

> "Baada ya miezi minne, Agosti 1962, aliitwa jijini Dar es Salaam, kujifunza udiplomasia nchini Colombia Marekani. Baada ya mwaka mmoja alirudi nchini akaajiriwa wizarani.

"Walipigwa na kuteswa hadi Padri Mzungu alipofanikiwa kuwanasua. Bibi wa mama aliaga dunia muda mfupi baada ya tukio hilo.

### KUTEMBEA SIKU MBILI

Anasema Mkapa na mwenziwe mmoja, ndiyo waliopata bahati ya kuendelea na masomo ya sekondari kutoka darasa la kati ya watoto 25 hadi 30 la wakati huo, kuchaguliwa ilikuwa bahati nasibu.

Prof. Mukandala anasema, Shule ya Sekondari Ndanda aliyosoma Rais mstaafu Mkapa, ilikuwa umbali wa kilomita 60 kutoka Lupaso.

"Yeye na wenzake walitembea kwa miguu,bila viatu kwa siku mbili wakiwa wamebeba kichwani vitu vyao ambavyo vilikuwa vimefungwa katika mkeka. Baadaye alipata sanduku la chuma. Walimu wa Ndanda walikuwa Wamisionari na walikazia sana sala na kazi 'Ora et labora," anasema.

Prof. Mukandala anasema, wanafunzi walipika chakula wenyewe na kwa kuwa Mkapa alikuwa mdogo, alipewa kazi ya kuosha vyombo.

"Kawaida alivibeba vyombo kichwani mpaka mahali pa kuviosha na kuvirudisha. Anasema kubeba vyombo hivyo ndiyo sababu ana upara hadi leo.

"Mwaka 1952, akiwa na umri wa miaka 15, aliamua kwenda Seminari darasa la nane. Baada ya muda mfupi aliamua kuwa upadre haukuwa wito wake, akarudi Ndanda kuendelea na shule," anasema.

### MWANZO WA SIASA

Prof. Mukandala anautaja mwaka 1957, ndio Rais Mkapa alichaguliwa kwenda katika shule ya St. Francis College Pugu (sasa Ougy Sekondari), ikiwa shule kuu ya Wakatoliki Tanganyika.

"Akiwa Pugu, alianza kupata mwamko wa kisiasa. Aliunga mkono harakati za kupata uhuru kwa kuandika barua kwa Mhariri wa gazeti la 'Tanganyika Standard ambalo sasa ni Daily News akiunga mkono hoja ya Uhuru.Barua ilichapishwa, ingawa alitumia jina bandia," anasema mchambuzi huyo.

Anasema, kijana huyo aliposhinda mitihani yake ya kujiunga Chuo Kikuu Makerere, akiwa na daraja la kwanza, kati ya wanafunzi watatu bora katika wanafunzi 51.

"Akiwa Makerere alikumbana na mambo mengi mapya: Alikuwa darasani na wanafunzi wa rangi tofauti, kwa mara ya kwanza alikwenda kucheza dansi ya kisasa na alipangiwa chumba cha kulala.

"Mwamko wake wa kisiasa uliendelea. Alijiunga na Bodi ya Wahariri ya gazeti la 'Transition' na alikuwa mwanachama hai wa kikundi cha wanafunzi cha TANU, akiwa Katibu na hatimaye Mwenyekiti. Alishiriki kwenye siasa za wanafunzi hapo chuoni," anasema Mukandala.

### KUGOMBEA URAIS

Anasema akiwa chuoni Makerere, Mkapa aligombea nafasi ya urais, ingawa hakushinda na walipiga kura nyingi walikuwa wanafunzi wa kike, ambao walivutiwa kwa jinsi alivyojieleza kuliko mpinzani wake.

"Aliteuliwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Wanafunzi na hatimaye alikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi la Wanafunzi hapo Makerere.

"Alihitimu masomo yake Aprili 1962,miezi minne baada ya Tanganyika kupata Uhuru. Alitunukiwa Shahada ya Lugha na Fasihi ya Kiingereza na Fonetiki. Alikuwa tayari kuifukuzia nia na ndoto yake," anasema Profesa Mukandala, ambaye ni mwanazuoni wa Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma.

### ALIOTA UWAZIRI

Anasema simulizi ya maisha ya utu uzima ya Mkapa iko katika sehemu mbili.Kwanza, ni alipoanza kazi mpaka alipogombea Urais na pili ni maisha ya Urais.

"Sehemu hii ya simulizi imejaa sifa heshima na upendo mwingi kwa Mwalimu Julius Nyerere. Anastaajabu kwa jinsi Mwalimu alivyoiunganisha nchi katika kupigania vita vya ukombozi wa bara la Afrika. "Kama wazazi wake mzee Matwani na Bibi Nambanga walikuwa mashujaa wa sehemu ya kwanza ya maisha yake, hakika Mwalimu ndiye shujaa katika sehemu hii ya pili.

"Anamueleza Mwalimu kama labda alitumwa na Mungu kwa makusudi, akiwa mtu mzima na mhitimu wa Chuo Kikuu Makerere, Mkapa alipenda kuajiriwa kwenye Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.

"Kwanza ilishindikana, lakini baadaye akaambiwa, itawezekana kama ataajiriwa kama bwana shauri mkufunzi wa wilaya wakati akisubiri. Kwa hiyo, aliajiriwa hivyo huko Dodoma, Aprili mwaka 1962.

"Baada ya miezi minne, Agosti 1962, aliitwa jijini Dar es Salaam, kujifunza udiplomasia nchini Colombia Marekani. Baada ya mwaka mmoja alirudi nchini akaajiriwa wizarani.

"Kazi yake kubwa ilikuwa kuchukua muhtasari wa mazungumzo Waziri wake au Rais alipopata wageni. Anamsifia kwa ujasiri pale alipovunja uhusiano na Uingereza.

"Wakati huu, Mkapa alitumia muda wake binafsi ama kusoma habari Radio Tanzania Dar es Salaam, au kumchumbia Anna," anasema.

Anachambua kitabu hicho na kueleza siku moja aliambiwa anaitwa Msasani kwa Mwalimu Julius Nyerere, aliyemweleza anamteua kuwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Nationalist. Ilibidi aende Uingereza kujifunza mambo ya magazeti kwenye magazeti ya The Mirror.

"Alirudi na kuanza kazi chini ya Mwalimu kama Mhariri Mkuu, Mkapa alikuwepo Arusha wakati wa Azimio, mwenzie Nsa Kaisi ndiye aliyebuni neno la Arusha Declaration, walilitumia kwenye The Nationalist, Mwalimu akalipenda, basi hayo maamuzi yakaitwa hivyo," anasema.

Anasema, Mkapa aliruhusiwa kuhudhuria mikutano ya Kamati Kuu ya TANU, ambayo wakati ule ilitawaliwa na malumbano ya hoja na uchambuzi yakinifu, ambao anadai umepotea sasa.

# Wanawake waja na ilani yao waanika figisu, kero uchaguzi

Na Sabato Kasika



Wadau wa uchaguzi wakiwa katika picha ya pamoja. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

KATIKA kuhakikisha kuwa uchaguzi unafanyika bila manung'uniko, wadau katika ngazi ya taifa hivi karibuni wanakutana jijini Dar es Salaam na hoja kadhaa zinajadiliwa. Mojawapo ni nguvu ya polisi katika kudhibiti mikutano ya kisiasa, rushwa ya ngono na kuwapuuza wenye ulemavu kushiriki kwenye uchaguzi kwa ngazi mbalimbali.

Aidha, mkutano huo ulilenga kuwajengea wadau hao uelewa wa pamoja juu ya mahitaji muhimu yaliyomo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Wanawaake ya mwaka 2020.

Washiriki wa mkutano huo ni pamoja na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), wawakilishi wa vyama vya siasa, jeshi la polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Wengine walioalika katika mkutano huo ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni Ulingo wa Wanawake na Siasa, Mtandao wa Wanawake na Katiba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec) na ya Zanzibar (Zec).

### KERO ZA WADAU

Baadhi ya washiriki wanaozungumza na kuchangia maoni mbalimbali ambayo wanaamini yatasaidia kufanikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Mkuu wa mwaka 2020 ni pamoja na Zahra Ali Hamad.

Zahra Naibu Katibu Ngome ya Wanawake CUF Zanzibar, analinyooshea mkono Jeshi la Polisi akilitaka kufanya kazi bila upendeleo na kukumbusha kuwa bila utawala bora hakuna maendeleo.

Anataka kuwe na mabadiliko akisema,"polisi waache uwanja wa kufanya siasa uwe tambarare badala ya kuegemea upande mmoja wakati nchi hii ni yetu sote na tunatakiwa kuijenga kwa kushirikiana bila upendeleo wowote," anasema.

Madai hayo yanaungwa mkono na Mwenyekiti wa Ngome ya Wanawake ya ACT -Wazalendo, Chiku Abwao, anayesema kwamba polisi ni kikwazo kikubwa kwa siasa za Tanzania na kuwataka wabadilike.

"Tumezuiliwa siasa za majukwaani, lakini hata vikao vya ndani polisi wanakuja kutufanyia fujo na kutukamata. Kwa ujumla ni kwamba wametuziba midogo tusiongee, hii siyo sahihi, wabadilike," anasema Abwao.

Mwanaharakati, Gemma Akilimali, anayetoa mchango wake anasema umefika wakati sasa wanawake kuchagua wanawake wenzao wanaowania uongozi bila kuangalia vyama wanavyotoka, ili mradi wawe na uwezo wa kuongoza.

"Dhana ya kwamba wanawake hawapendani isipewe nafasi kabisa, kwani sisi wote ni kitu kimoja, ndiyo maana tumekutana hapa bila ubaguzi wa vyama, tukiruhusu dhana hiyo itatugawa," anasema Gemma.

Mtandao wa Wanawake, Katiba na Uongozi, ukiwasilishwa na Maria Chale,unaona kuwa bado kuna tatizo la ubaguzi unaotokana na ulemavu hali inayosababisha wenye mahitaji kutochaguliwa katika uongozi.

> "Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa weledi, lakini pia tusitake mambo yaharibike ndipo tunyoosheane vidole, hata nyie asasi za kiraia, katika mikutano yenu shirikisheni askari wetu, wapo nchi nzima.

Distributed via ippmedia

"Mbali na hilo huwa kuna tuhuma za rushwa ya ngono katika vyama vya siasa hasa wakati wa mchakato wa kupata wagombea, hali ambayo inakwamisha wanawake kupata nafasi za uongozi," anasema Maria.

### POLISI WAJITETEA

Kwa upande wake mwakilishi wa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Inspekta Issa Asali, anawataka wadau hao kufanya shughuli zao, huku ajenda kuu ikiwa ni usalama, kwa vile usalama, amani na utulivu vikikosekana, hakuna ustawi wa jamii.

"Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa weledi, lakini pia tusitake mambo yaharibike ndipo tunyoosheane vidole, hata nyie asasi za kiraia, katika mikutano yenu shirikisheni askari wetu, wapo nchi nzima," anasema Inspekta Asali.

Anasema wanasiasa na wadau wengine wakifanya shughuli zao huku wakiweka mbele ajenda ya usalama, hakutakuwa na malalamiko yoyote kwa jeshi hilo, lakini wakifanye kinyume, jeshi haliwezi kukaa kimya.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukururu) ni mdau kwenye masuala ya uchaguzi, mwalikishi wake, Mercy Manyalika, akizungumzia suala la rushwa, anawataka Watanzania waelewe thamani wa kura zao kuliko vitu wanavyopokea na kuweka madarakani viongozi wabovu.

"Wote watakaokumbana na kadhia hiyo ya rushwa ikiwamo ya ngono, wapige simu namba 113 wakiwa sehemu yoyote nchini, Takukuru itachukua hatua haraka iwezekanavyo," anasema Mercy.

### TUME YAWAALIKA

Akizungumzia suala la haki za wananchi , Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Mathew Mwaimu, anawataka wadau wote watakaokumbana na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu, watoe taarifa.



Mkurugenzi wa TGNP, Liliani Lihundi, akizungumza katika mkutano huo.

Mwaimu anasema ofisi za tume hiyo ziko wazi kwa ajili ya kushughulikia vitendo vya ukikwaji wa haki za binadamu zikiwamo za baadhi ya watu kubaguliwa kwa sababu ya ulemavu.

### ILANI YA WANAWAKE

Katika mkutano huo, wadau hao wanashauriana namna ya kuhakikisha wanawake wanapata nafasi na kushiriki kikamilifu kwenye nafasi za uongozi wakati wote wa mchakato wa uchaguzi.

Lilian Lihundi ni Mkurugenzi wa TGNP, ambaye wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, anasema Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake imeandaliwa na TGNP na inaendeleza madai ya wanawake watetezi wa haki za kushiriki uongozi wa kisiasa.

"Ilani hii ni ya tano iliyobeba madai yetu rasmi tukiwa wadau na washiriki wakuu katika michakato mbalimbali ya uchaguzi . Ilani ya kwanza ilikuwa ya mwaka 2000 ikijulikana kama Ilani ya Wapigakura," anasema Liundi.

Anafafanua kuwa baada ya hapo zinafuata Ilani nyingine za mwaka 2005, 2010, 2015, na kwamba Ilani zote maandalizi yake yaliongozwa na TGNP Mtandao kupitia Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi.

"Ilani ya sasa inajumuisha sauti za wanawake kutoka makundi mbalimbali chini ya uongozi wa TGNP Mtandao, kwa kushirikiana na Women Fund Tanzania na Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi," anasema.

### LENGO LA ILANI

Liundi anataja lengo kuu la ilani hiyo kuwa ni kudai ushiriki wa wanawake katika uongozi wa taifa ikiwa ni pamoja na ushiriki katika chaguzi zote kama wapigakura na walioteuliwa kuwania nafasi mbalimbali katika chaguzi.

"Ilani pia inataka tuwe washindi na waliopewa dhamana ya kuongoza taifa katika nyadhifa mbalimbali kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, na pia inatuhamasisha tukatae kuendelea kutumiwa kama wapigadebe," anasema.

Anaongeza kuwa ilani hiyo inawataka wanawake wasiwe wasindikizaji katika kampeni, waburudishaji kwenye sherehe au kampeni za uchaguzi na waathirika wa ufukara na umaskini.

"Tuhamasike na kushikamana ili kupambana na mifumo kandamizi hususan mfumo dume, ambao huathiri upatikanaji wa haki zetu na hatimaye kudumaza uchumi na maendeleo ya jamii yote wake kwa waume," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, ilani hiyo pia inavilenga vyama vya siasa kuanzia wanachama, uongozi na mashabiki wake na kwamba hapa nchini vyama hivyo ndivyo njia pekee ya kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi.

"Vyama vya siasa ni walinzi wa lango kuu la kuingia kwenye siasa za uchaguzi, kwa maana hii ni kwamba vyama hivyo huamua ni nani aingie ni nani aachwe, ni nani awezeshwe kushinda na pia ni nani aachwe akiogelea mwenyewe kwenye uwanja wa ushindani usio haki na huru kwa wanawake walio wengi," anasema.

Anasema, ilani hiyo pia inalenga serikali iliyoko madarakani na itakayoshika madaraka na taasisi zake, na kwamba iliyoko madarakani ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha uwanja shindani wa kisiasa ni huru na salama kwa makundi yote hususan wanawake.

# Rais mzawa wa Bolivia aikimbia nchi kujihifadhi 'peponi' Mexico



Evo Morales. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

WAKATI Rais Nicolas Maduro, nchini Venezuela amefaulu kushikilia madaraka ndani ya upinzani mkubwa bungeni na kutangazwa serikali pinzani inayoongozwa na Spika wa Bunge, nchini Bolivia mambo yamekwenda tofauti na Rais Evo Morales amekimbia nchi.

Siku moja baada ya Morales kuikimbia Bolivia kutokana na maandamano ya muda mrefu na mapigano ya hapa na pale kati ya wafuasi wake na upinzani, serikali ya mpito ilitangazwa na kiongozi wake, mwanamama Jeanine Anez.

Rais huyo mteule alikuwa Naibu Mwenyekiti wa Baraza la Senate la nchi hiyo, akitokea chama tawala cha Rais Morales.

Hatua ya kwanza aliyotangaza mwanamama huyo anayeiongoza Bolivia kwa sasa ni kuondoa mezani suala la Morales kushiriki uchaguzi mkuu utakapofanyika tena ili kuunda serikali yenye msingi wa kutosha bungeni kwa wingi wa kura. Wachunguzi wa mambo walisema kuwa Morales aliamua kuachia madaraka baada ya wakuu wa majeshi kuonyesha kutokumuunga mkono, wakati ambapo nchini Venezuela, jeshi limebakia kuwa tiifu kwa chama cha kimapinduzi kilichoko madarakani.

Hitaji la kutangaza kuwa Morales hawezi kusimama tena kugombea linatokana na wafuasi wake kuendelea kuandamana tangu aondoke madarakani, wakitaka arudi atetee kiti chake katika uchaguzi mpya, hali itakayoshindikana.

Kabla rais huyo aliyejiuzulu hajamaliza wiki moja uhamishoni, maandamano yalipamba moto ya kutaka arudi, kwani ni kipenzi cha watu walio wengi nchini humo wanaotokana na wakazi wa jadi wa Bolivia.

> "Hivyo alikaa madarakani kwa wiki tatu za muhula wake wanne, na aliposhindwa kuwatuliza waandamanaji, jeshi likamshauri aachie madaraka aende uhamishoni.

Nchi hiyo kama yalivyo mataifa mengine ya bara la Amerika ya Kusini zinamchanganyiko wa watu wa asili na wahamiaji kutoka Ulaya waliogeuza bara hilo kuwa koloni lao, eneo pana la Brazil likachukuliwa na Ureno na eneo lililobaki kutwaliwa na Hispania. Hivyo Bolivia ni moja ya nchi za bara hilo zinazoongea Kihispania, na kama ilivyo kwingineko kuna harakati za kudumu za kitabaka zinazoendana na hali hiyo.

Maandamano nchini Bolivia yamechukua sura ya watu wa jadi kutaka kiongozi wao arudi, kwani Morales alikuwa mtu wa kwanza kutoka jamii hiyo kufikia ngazi ya kuwa rais wa nchi hiyo. Hata hivyo uhusiano wake na wananchi wa kawaida au watu wa jadi wa Bolivia una mikanganyiko . Aidha, Morales anatokea jimbo la Chapare, ambalo wachunguzi wa habari wanasema linafahamika sasa kwa kilimo cha coca, majani yanayotengezea madawa ya kulevya. Taarifa zinasema kuwa polisi waliwazuia wafuasi wa Morales kutoka eneo hilo kufika mji wa karibu wa Cochabamba, ambako mapigano kati ya wafuasi na wapinzanii wa Morales wamekuwa katika purukushani barabarani kila wakati, kabla Morales hajajiuzulu.

Waandamanaji walibeba mabango kuonyesha kuwa wanahisi kuondolewa madarakani kwa kiongozi huyo ni kwa sababu anatoka miongoni mwao, kuwa 'wakuja' hawajawahi kukubali kuwa mmoja wao anaweza kuwa kiongozi wa nchi.

Ina maana hawatilii maanani misukosuko ya uchumi iliyotokea hadi ikabidi Morales kuachia ngazi, ila tu anatokea katika jamii yao na kwa hiyo kuachia ngazi ni jambo lisilokubalika kwao.

Inaelekea ni hisia kama hizo zilizomfanya Morales atake kudumu madarakani muda mrefu hata kwa njia za figisu figisu, katika kupiga na kuhesabu kura, kwani licha ya kukaa madarakani miaka 13, hawataki aondoke.

Taarifa nyingine zinasema kuwa jijini La Paz, mji mkuu wa Bolivia, baadhi ya vituo vya petroli viliikuwa havina nishati hiyo. Wafuasi wa Morales walikuwa wamefunga njia kutoka mji wa El Alto ambako mafuta yanasambazwa zaidi kutoka huko. Kuzuia kuuza mafuta ni kutaka utawala uruhusu Morales arudi.

Nchini Mexico ilionekana kana kwamba Morales yuko miongoni mwa marafiki, baada ya taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje kusema kuwa uhuru wa Morales wa kuzungumza hautawekewa vikwazo vya ziada ukilinganisha na uhuru wa kawaida wa raia wa Mexico.

Inaelekea taarifa hiyo ilitolewa pale kiongozi wa serikali ya mpito ya Bolivia kuicharura Mexico kwa kumruhusu Morales kutumia jukwaa la ukimbizi wake kutafuta kuungwa mkono nchini Bolivia. Mexico ni nchi ambayo hivi sasa ina watu wengi wanaoichukia Marekani kutokana na sera ya Rais Donald Trump, kusukuma agenda ya kujenga ukuta kati ya nchi hizo mbili, akizuia kwa nguvu uhamiaji.

Taarifa zilisema kuwa Morales alijiuzulu kwa shinikizo la jeshi baada ya maandamano makubwa kote nchini kwa wiki kadhaa kupinga figisu zilizoonekana katika uchaguzi mkuu Oktoba 20 ambako Morales alitangazwa mshindi.

Hivyo alikaa madarakani kwa wiki tatu za muhula wake wanne, na aliposhindwa kuwatuliza waandamanaji, jeshi likamshauri aachie madaraka aende uhamishoni.

Wafuatiliaji wa kura kutoka Umoja wa Nchi za Amerika ya Kusini (OAS) walisema kuwa data walizokusanya kuhusu kupiga na kuhesabu kura hadi matokeo zilionyesha ulikuwapo udanganyifu mwingi na Morales akajikuta akikwama kuunda serikali inayokubalika, hasa Baraza la Bunge la Senate.

Suala linaloisumbua Bolivia hivi sasa ni kama Morales ana haki ya kikatiba kushiriki katika uchaguzi mwingine, suala linalotokana na Morales, akiwa madarakani, kukataa kufanyika kura ya maoni kuhusu ukomo wa mihula ya urais.

Kiongozi wa muda Anez alisema chama cha Harakati Kuelekea Ujamaa kinachomuunga mkono Morales kina haki sawa kushiriki katika uchaguzi, watafute wagombea na huku akihakikisha kuwa Morales hawezi kugombea tena.

Kuvuruga uchaguzi na kuondolewa kwa maandamano inakuwa ni ishara ya kutofaa tena kuwa madarakani, hali inayomaanisha kuwa lazima muda upite, muhula mmoja au zaidi, asigombee.

Hivi sasa serikali za Amerika ya Kusini zimejigawa kwa makundi, kati ya zile za mwelekeo wa kimapinduzi na za kihafidhina, mgawanyiko wa jadi barani humo unaoendana na umiliki ardhi kwa kununua na kwa urithi wa jadi.

Aidha, kuna ushirika wa umiliki ardhi na biashara kubwa kwa upande mmoja na milki ya jadi na tabaka la wafanyakazi, na wasioajiriwa au biashara ndogondogo kwa upande mwingine. Wenyeji wa Morales, serikali ya Mexico, ilisema hatua ya kuondolewa madarakani Morales ni kama mageuzi ya kijeshi, kama tawala nyingine za mwelekeo huo zilivyosema.

Serikali ya mpito ya Bolivia hata hivyo inaungwa mkono na tawala kadhaa za kihafidhina kama Brazil, Guatemala na Colombia, pamoja na Uingereza na Marekani.

Anez pia alitangaza kuitambua serikali mbadala nchini Venezuela inayotambuliwa na Marekani ikiongozwa na Juan Guaido kama kiongozi halali wa nchi hiyo, akijiunga na Marekani na nchi nyingine 50 hasa za Magharibi, zinazokataa uhalali wa Nicholas Maduro, rafiki wa Morales, kama rais wa Venezuela.

Hata hivyo serikali ya mpito Bolivia ina matatizo makubwa ya jinsi ya kujihalalisha kisheria, kwani Bunge, Baraza la Wawakilishi na Baraza la Senate yameshikiliwa na wafuasi wa Morales. Wanazo fursa kuamua kinachofuata.

Msako vile vile ulikuwa umeanza dhidi ya baadhi ya wasaidizi wa karibu wa Morales, akiwemo Juan Ramon Quintana, ambaye anatafutwa na aliyechukua nafasi yake, kwa mujibu wa Arturo Murillo, waziri mpya wa Mambo ya Ndani. Wachambuzi kadhaa wanaona kundi la kijadi linalomuunga mkono Morales kama tishio kwa umoja na amani nchini humo kwani linakataa mabadiliko. Wanataka mifumo kizamani ilindwe, hasa jadi ardhi.



## Wakulima wahimizwa taarifa TMA

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameshauriwa kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ili walime mazao ambayo yanaendana na hali ya hewa.

Ushauri huo ulitolewa jana na Meneja wa TMA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Issa Hamad, alipokuwa anazungumza na wandishi wa habari ambapo alisema taarifa hizo ni muhimu kuzingatiwa na wakulima.

Alisema baada ya wakulima kupata taarifa hizo wanatakiwa kuwaona maofisa kilimo ili wawashauri aina ya mbegu za mazao zinazofaa kutumika kulingana na taarifa hizo ambazo alisema zinatolewa kila siku kupitia vyombo vya habari.

Hamad alisema wakati mwingine wakulima huwa wanalalamika kuwa mazao yao yanaharibika kutokana na hali ya hewa lakini chanzo kikubwa ni wao wenyewe kutofuata taarifa hizo.

"Kwenye nyombo vya habari kila siku tunatoa taarifa za hali ya hewa, sasa wananchi wetu wanatakiwa wazingatie taarifa hizo ili ziwasaidie kwenye kilimo chao," alisema Hamad.

Alisema wameboresha utoaji wa taarifa hizo kwa madai kuwa zinapatikana hata kwenye mitandao ya kijamii ili kuwarahisishia wale ambao hawafuatilii vyombo vya habari.

**"Kwenye nyombo vya habari kila siku tunatoa taarifa za hali ya hewa, sasa wananchi wetu wanatakiwa wazingatie taarifa hizo ili ziwasaidie kwenye kilimo chao," alisema Hamad.**

# Amri ya DC yakwamisha msimu kilimo

Na Nebart Msokwa, MBARALI

WAKAZI wa Kitongoji cha Nyeregete katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wamekwama kuendelea na maandalizi ya msimu ujao wa kilimo baada ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, kuwazuia kufanya shughuli yoyote kutokana na mgogoro wa ardhi unaoendelea.

Wananchi hao ambao wanaishi katika eneo la Katenge katika Kitongoji cha Nyeregete wilayani humo, wamezuiliwa kwa barua maalum kutoka katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ikiwataka kutofanya shughuli yoyote kwenye ardhi yao mpaka watakapopewa maelekezo mengine.

Wakizungumza na wandishi wa habari juzi, wananchi hao walisema endapo tatizo hilo halitatatuliwa mapema kuna hatari wakakumbwa na baa la njaa mwakani kwa maelezo kuwa wanategemea kilimo kuendesha maisha yao.

Edwin Msigala alisema tangu waanze kuishi katika eneo hilo hawajawahi kuwa na mgogoro na kijiji chochote, lakini wanashangaa sasa hivi serikali inatoa amri ya kuwazuia wasiendeleze maeneo yao.

Alisema wameshaandaa mbegu za viazi ambavyo walitakiwa wapande, lakini baada ya kuzuiliwa kulima wana wasiwasi kuwa zitaharibika endapo wataendelea kuzuiliwa na Mkuu huyo wa Wilaya.

"Sisi hapa tunakaa sio eneo la mtu ni la kwetu tangu muda mrefu tulikuwa tunalitumia kwa ajili ya kilimo na ufugaji ambazo ndio shughuli zetu hapa, sasa hii amri ya Mkuu wa Wilaya itatuathiri sana, maana hatujazoea maisha mengine," alisema Msigala.

Nae Makresia Pawa, alisema wanayatumia hayo mashamba kuendeshea maisha ikiwamo kusomesha watoto hivyo akamuomba Mkuu wa Wilaya kuwaruhusu waendelee kuyatumia kwa madai kuwa hawana mgogoro na mtu ama taasisi yoyote.

Alisema kwa jinsi wanavyoona hali ilivyo, kuna uwezekano kuna baadhi ya watu wenye nia ovu ambao wanataka kuidanganya serikali kuwa kuna mgogoro ili wanufaike na mashamba hayo.

Pawa alimuomba Mkuu wa Wilaya na wasaidizi wake kufuatilia suala hilo kwa umakini ili kuepuka kuwaumiza kwa kuwapora maeneo hayo ambayo yanafahamika kwa asili kuwa ni ya kwao.

"Sisi tunaiomba Serikali iwe makini inaposhughulikia suala hili maana kuna uwezekano baadhi ya watu wanatuzunguka wanataka tuondolewe ili wao wanufaike na mashamba yetu," alisema Pawa.

Naye Nchambi Kalambo, alisema yeye alifika katika eneo hilo muda mrefu na kwamba kwa wakati huo lilikuwa pori na hawajawahi kuwa na mgogoro na mtu sasa wanashangaa mgogoro unakoanzia.

Mfune alikiri kuwazuia wananchi hao kufanya shughuli zozote katika eneo hilo kwa madai kuwa eneo hilo ni mali ya umma lakini linatumika kwa manufaa ya watu wachahe wa eneo la Katenge.

Aliwataka wananchi hao kuwa watulivu kwa maelezo kuwa atatoa maelekezo muda sio mrefu na kwamba wasiwe na wasiwasi kuwa watachelewa msimu wa kilimo.


Distributed via ippmedia

Wananchi wa Kitongoji cha Nyeregete katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakiwaonyesha waandishi wa habari sehemu ya maeneo yao juzi ambayo wamezuiliwa na Mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfune (hayupo pichani), kuendelea kuyatumia kwa maelezo kuwa kuna mgogoro wa ardhi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Sababu waathirika ajali kukosa fidia

Na Nebart Msokwa, MBEYA

IMEELEZWA wananchi wengi wanaopata ajali za barabarani wanakosa haki yao ya kufidiwa na kampuni za bima kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya masuala ya bima.

Hayo yalisemwa jana na Mkaguzi wa Polisi Kitengo cha Usalama barabarani Mkoa wa Mbeya, Joseph Mahundi, ambapo alisema kwa mujibu wa sheria za nchi ni haki ya mhanga wa ajali kupata fidia za matibabu kutoka kwenye kampuni husika.

Alisema kwa sasa vyombo vyote vya moto vinatakiwa kuwa na bima ambayo moja kati ya majukumu yake ni kumfidia mtu anayepata madhara kutokana na chombo hicho lakini wengi huwa hawafuatilii na hivyo kuikosa haki yao.

Mahundi alisema endapo mhusika hajafuatilia huwa ni vigumu kulipwa fidia kwa madai kuwa kampuni huwa zinasubiri kupelekewa taarifa ili ziweze kulipa.

"Kwa sasa tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajuwe maana ya bima na namna ambavyo wanatakiwa kufidiwa endapo watapata madhara wakiwa ndani ya vyombo vya moto ama wanapotembea barabarani," alisema Mahundi.

Alisisitiza kuwa mchakato wa kulipwa fidia kwa mtu anayepata ajali huanzia katika Jeshi la Polisi kupitia kitengo cha upelelezi wa majalada ya ajali za barabarani na kwamba baada ya hapo mhusika anatakiwa kupeleka taarifa zake kwenye kampuni husika za bima ili alipwe.


Hata hivyo, alisema kutokana na elimu inayotolewa na Jeshi la Polisi baadhi ya wananchi wameanza kujitokeza na kwenda kuomba kusaidiwa ili walipwe fidia zao kutokana na ajali zinazowakuta.

Aliwataka wananchi wanaopata ajali kuhakikisha wanapata nyaraka za kuwawezesha kutibiwa kutoka Jeshi la Polisi kwa maelezo kuwa ni miongoni mwa vielelezo vinavyomsaidia mtu kupata matibabu.

Pia aliwataka wamiliki wa vyombo vya moto kuhakikisha wanavikatia bima halali vyombo vyao ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria.

Takwimu za Shirika la Afya duniani (WHO), zinaonyesha kuwa watu milioni 1.25 hufariki kila mwaka kutokana na ajali za barabarani na wengine kati ya milioni 20 mpaka milioni 50 hupata ulemavu wa kudumu.

Aidha, takwimu hizo zinaonyesha kuwa ajali nyingi zaidi hutokea barani Afrika hasa mataifa ya kusini mwa Jangwa la Sahara.





## Wakulima washauriwa kitaalamu

**Na Ibrahim Joseph, CHEMBA**

WAKULIMA Wilaya ya Chemba, wametakiwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu unaotolewa na wataalamu wa kilimo na taarifa za utabiri wa hali ya hewa ili kulima mazao yanayostahimili kiwango cha mvua msimu husika.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, alipokuwa akizungumza kwenye uzinduzi wa kilimo cha alizeti kwa wilaya hiyo unaofadhiliwa na kampuni ya Three Sister Ltd.

Odunga alisema kuna umuhimu mkubwa wa kutumia taarifa za hali ya hewa na ushauri wa wataalamu ili kupanda mazao yanayolingana na upatikanaji wa mvua uliopo.

Alisema sababu za kufanya uzinduzi huo wa kilimo cha alizeti katika wilaya hiyo ni kutokana na zao hilo kuwa miongoni mwa mazao yaliyopewa kipaumbele kwenye kilimo katika msimu ujao unaotarajiwa kuanza mapema mwezi ujao.

"Wakulima pia acheni tabia ya kulima mazao ya chakula na biashara kwa mazoea kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayojitokeza kila wakati," alisema.

Aidha, alisema kutokana na kulima kwa mazoea, mwaka jana wilaya ya hiyo ilivuna chakula pungufu tani 21,000 ambapo walivuna tani 37,000 za mazao tofauti na malengo ya kupata tani 58,000 za chakula.

Alibanisha kuwa asilimia 80 ya wakazi wa wilaya hiyo ni wakulima na ya asilimia 20 iliyobaki ni wafugaji, na kaya zilizopo ni 52,000 zilinazojishughulisha na kilimo ni 36,000.

Aliongeza kuwa pamoja na kutegemea mvua katika kilimo wilaya wameweka mipango ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji ili kuinua uchumi wa wananchi wa eneo hilo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Three Sisters Ltd, Mariamu Majengo, alisema mradi huo wa kilimo cha alizeti ni wa miaka mitatu kuanzia 2019 mpaka 2021.

Majengo alisema mradi huo unalenga kutoa mafunzo kwa wakulima ili kuwajengea uwezo wa kulima mazao yanayostahimili ya hali ya hewa katika maeneo yao.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika Vijiji 10 vilivyopo kwenye Kata sita za Wilaya ya Chemba kupitia vikundi vya wakulima kwa kutumia kilimo cha mashamba darasa.

Alivitaja Vijiji hivyo ni Mondo, Pongai, Waida, Daki, Jenjeluse, Dalai, Tandala, Chambalo, Rofati na Tumbakose.

# Viongozi wa dini waaswa kampeni nyumba za ibada

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

VIONGOZI wa dini nchini wametakiwa kuacha tabia ya kuwaruhusu viongozi wa kisiasa kuzitumia nyumba za ibada kufanya kampeni wakati huu wa harakati za uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu na uchaguzi mkuu 2020.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Maridhiano Taifa, Askofu Osward Mlay, kwenye kongamano la kuliombea taifa pamoja na uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema viongozi wa dini wanatakiwa kuacha kuwaruhusu viongozi wa kisiasa kuzitumia nyumba za ibada kufanya kampeni zao.

"Nyumba za ibada haziruhusiwi kutumika katika kufanya kampeni kama wataka kuombewa waje, lakini sio kutumia misikiti na makanisa yetu kufanya kampeni za uchaguzi," alisema.

Alisema jumuiya hiyo iliundwa kusaidia katika kutatua changamoto zilizopo katika jamii ikiwamo migogoro ya wakulima na wafugaji.

"Muasisi wa Jumuiya hii ni Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ambaye leo pia tungekuwa naye, lakini kutokana na mambo yake kubana hataweza kuwa nasi lakini tu kwa ujumla Jumuiya hii inafanya mambo makubwa sana katika kuisadia jamii kwani ni mchanganyiko wa dini zote pamoja na watu wa jamii mbalimbali tupo kwa ajili ya kufanya maridhinano ili kuendelea kuilinda amani yetu tuliyonayo," alisema.

Aidha, alisema pamoja na Jumuiya hiyo kufanya mambo makubwa kwa maslahi ya jamii lakini bado wamekuwapo watu wachache ambao wamekuwa wakibeza jitihada zake kwa kuwaita matapeli.

"Mheshimiwa mgeni rasmi, jumuiya kama ulivyosikia katika utambulisho hapa watu walipo ni kutoka katika maeneo mbalimbali ya nchi, wapo watu kutoka Kigoma, Mara kwa hiyo hatuwezi kuwasumbua watu kotoka katika maeneo hayo halafu sisi tuwe matapeli kama tunavyoitwa," alisema.

Akijibu risala ya katibu huyo, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, (Tamisemi), Mwita Waitara, aliwataka wakuu wote wa mikoa na wilaya kutoa ushirikiano kwa jumuiya hiyo ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

Waitara alisema Jumuiya hiyo ni chombo muhimu katika Taifa ambacho kinaweza kuisaidia serikali kutatua migogoro katika jamii kwenye maeneo ambayo haiwezi kufika.

"Nitoe wito kwa wakuu wote wa mikoa na wilaya kuhakikisha kuwa wanaipa ushirikiano jumuiya hii katika maeneo yao ili iweze kufanya kazi zake kikamilifu na kuendelea kudumisha amani ya nchi iliyopo," alisema Waitara.




Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, akijaribu kuwasha moja ya pikipiki zilizotolewa msaada na kampuni ya Three Sisters Ltd, kwa ajili ya maofisa kilimo, katika Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Taasisi zinazoajiri wageni zategwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

TAASISI zinazoajiri raia wa kigeni nchini zikiwamo shule, zimeagizwa kuhakikisha maofisa wake wanahudhuria mafunzo ya lazima ya wiki moja katika Chuo cha Kikanda ya kuwajengea uwezo ili kujua taratibu za kuwahudumia raia hao.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Chuo cha Uhamiaji cha kikanda nchini, Kamishna Maurice Kitinusa, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mikakati ya kudhibiti wahamiaji haramu nchini.

Alisema mafunzo hayo ni ya lazima kwa taasisi zote nchini zinazoingiza wafanyakazi kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kufanya kazi kwenye shule na maeneo mengine.

Alitaja maofisa wanaopaswa kupata mafunzo hayo ni meneja rasilimali watu, ofisa uhusiano na mwanasheria wa taasisi kutokana na wengi wao kutojua taratibu za kuwahudumia wageni hao.

"Unakuta raia wa kigeni anaomba aandikiwe barua ili akaombe kibali cha kufanya kazi, inawawia vigumu kwa sababu hawajui masuala hayo," alisema Kamishna Kitinusa.

Alisema mafunzo hayo yatakuwa nchi nzima, na yatalenga taasisi zote ambazo zinaingiza wageni na kuwajiri.

"Naziagiza taasisi kuhakikisha wanaleta watu walioanishwa kwa ajili ya mafunzo hayo la sivyo hakuna atakayeruhusiwa kuingiza raia wa kigeni endapo taasisi yake haitakuwa na cheti cha mafunzo hayo," alisema Kamishna Kitinusa.

Akizungumza kusaini mkataba wa kudhibiti wahamiaji haramu na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wahamiaji (IOM), alisema utasaidia chuo kujiendesha kupitia mafunzo wanayopata pamoja na vifaa wanavyotoa kwa chuo.

Alisema shirika hilo limefanikisha kutengeneza wataalamu katika kutambua vyombo vya usalama wenye uwezo wa kutoka ushahidi mahakamani kupitia nyaraka feki zinazotengenezwa.

"Pia wataalamu wana uwezo wa kutengeneza karatasi ambazo hutumika kutengeneza vitambulisho bila wengine kugushi,"alisema.



HABARI ZANZIBAR

# Shein aona fursa EAC

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema eneo la Afrika Mashariki ni zuri kiuchumi iwapo litatumia vizuri.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua maonyesho ya wajasiriamali kuadhimisha miaka 20 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Fumba wilayani Magharibi Unguja.

Alisema nyenzo muhimu ni ushirikiano wa pamoja katika jitihada za wakuu wa nchi kuimarisha utawala bora.

Alisema utangamano wa Afrika Mashariki umeweka vipaumbele vitano baina ya mwaka 2017 hadi 2021, miongoni mwake ni uimarishaji wa mzunguko huru wa utengenezaji na utoaji wa bidhaa miongoni mwa nchi hizo, uimarishaji wa maendeleo ya viwanda na kuongeza ubora katika bidhaa, usalama na utawala bora.

Rais Shein alisema suala la kuendeleza viwanda limepewa kipaumbele katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Alisema maonyesho hayafanywi kwa ajili ya kuangalia vitu, kuuza na kununua tu, bali kujifunza kwa njia mbalimbali mbinu za kiufundi na mikakati ya kibiashara ili kuimarisha miradi mikubwa na midogo.

Alisema serikali yake imefurahishwa na uamuzi uliochukuliwa wa maonyesho hayo kufanyika Zanzibar katika Mji wa Fumba ambao ni alama ya maendeleo makubwa kutokana na kuendelea kuimarishwa na mfanyabiashara mzalendo Said Salim Bakhresa kwa kushirikiana na serikali.

Alisema maonyesho hayo yana umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa mipango ya kuendeleza viwanda na kukuza shughuli ya ujasiriamali.

Rais Shein alisema sekta ya viwanda ina umuhimu wa pekee katika ujenzi wa taifa, akifafanua kuwa maendeleo ya viwanda hulisukuma taifa kujitegemea katika kuyamudu mahitaji yake kiuchumi.

Alisema sekta hiyo pia ni muhimu katika kuzalisha ajira na kurahisha soko la bidhaa zinazozalishwa nchini, hasa katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Alisema ili viwanda viendelee, lazima pawe na masoko ya kutosha ya kuuza bidhaa na huduma zinazotolewa ambalo ndiyo lengo la maonyesho hayo kuwakutanisha wateja, watengenezaji bidhaa na watoa huduma mbalimbali.

Dk. Shein aliongeza kuwa kuna haja ya kufikiria mbinu bora zaidi zitakazotumika katika kuvipa thamani vitu vya asili, viwe katika ubora na viwango vya juu kwa lengo la kuvutia masoko ya ndani na nje.

Alisema ubunifu ni jambo muhimu katika kuiendeleza miradi ya kibiashara na viwanda na kuondokana na fikra kwamba ujasiriamali ni kutengeneza bidhaa ndogo.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Maudline Castico, alipongeza ushirikiano mkubwa uliopo kati yao na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Bunge pamoja na jumuiya zote za wajasiriamali.




Distributed via ippmedia

Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid (katikati), akizindua kitabu cha mpango mkakati wa ukondoishaji wa masuala ya kijinsia ndani ya Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ataka takwimu sahihi serikalini

**Na Rahma Suleiman,ZANZIBAR**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia, ameitaka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kuhakikisha inatoa takwimu zisizo na shaka na zenye umakini ili kusitokee mtu kuzihoji.

Akizungumza katika maadhimisho ya siku ya takwimu ya Afrika yaliyofanyika Mazizini mjini Unguja, waziri huyo alisema takwimu zikitolewa kwa usahihi, zitasaidia kukuza mambo mbalimbali yakiwamo ya kiuchumi na shughuli za kijamii.

Alisema takwimu ni taarifa, elimu na ujuzi na haiwezi kudharauliwa, hivyo ni umuhimu kuhamasisha matumizi yake.

Alisema katika Bara la Afrika, kuna tatizo kubwa la watu kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine hasa vijana kuhamia mijini na wakati mwingine kumekuwa kukitokea upotoshaji wa takwimu za makundi mbalimbali.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mayasa Mahfoudh Mwinyi, alisema katika kuhakikisha upatikanaji wa takwimu zenye ubora, ofisi hiyo inaendelea kutoa takwimu mbalimbali kupitia utafiti, sensa na takwimu za kawaida ili kupata takwimu zitakazotumika katika kutathmini mafanikio ya programu za kitaifa.

Alisema kwa sasa, ofisi hiyo inaendelea na ukusanyaji wa taarifa za utafiti wa mapato na matumizi ya kaya (HBS) wa mwaka 2019/2020 kwa lengo la kupata viashiria vya kupima hali ya umaskini katika kijamii.

## Spika ajivunia wanawake Baraza la Wawakilishi

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, amesema uendeshaji wa shughuli za baraza kwa sasa umezingatia jinsia na kutoa kipaumbele kikubwa kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika chombo hicho cha kutunga sheria.

Maulid aliyasema hayo wakati akizindua kitabu cha mpango mkakati wa masuala ya kijinsia ndani ya baraza hilo.

Alisema marekebisho ya kanuni za baraza yametoa nafasi kubwa na kutambua mchango wa mwanamke katika kushiriki shughuli za chombo hicho pamoja na kamati zake.

Alisema awali hakukuwa na sheria ya aina hiyo, akieleza kuwa hata kamati ya uongozi wa Baraza la Wawakilishi ilikuwa na mjumbe mmoja tu mwanamke.

''Marekebisho ya kanuni kwa kiasi kikubwa yamefungua milango na fursa kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika chombo cha kutunga sheria. Hivi sasa zipo kamati tatu zinaongozwa na wanawake,'' alisema.

Spika huyo alisema uzinduzi wa mkakati huo kwa kiasi kikubwa utawawezesha wajumbe wanawake kuongezeka zaidi katika baraza hilo kwa kupata mafunzo juu ya chombo hicho.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawakilishi Wanawake (Uwawaza), Mgeni Hassan Juma, alisema wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi, hasa wanawake, wamehamasika kushiriki mijadala ya chombo hicho.

Alisema elimu wanayoitoa kupitia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawake imeibuwa ari na uwezo mkubwa kiasi ya baadhi ya wajumbe wa baraza kuibuka na hoja binafsi.

''Mafunzo haya yametusaidia sana kwa sababu kila baada ya miaka mitano, tunapata wajumbe wapya katika Baraza la wawakilishi kwa asilimia 70. Sasa, tutawajenga kielimu ili washiriki kikamilifu katika baraza kwa kuibuwa mijadala yenye tija,'' alisema.

Ofisa wa Ubalozi wa Finland nchini, Rukka Raetikainen, alisema ushirikishwaji mzuri wa mwanamke katika chombo cha kutunga sheria utasaidia kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kutungwa sheria nzuri zenye maslahi kwa mwanamke.

''Nimefurahishwa kupata taarifa kwamba baadhi ya kamati za Baraza la Wawakilishi zinaongozwa na wanawake,'' alisema.

# Wajane wambana DC kulipwa fidia

**Na Rose Jacob, UKEREWE**

ZAIDI ya wajane 20 waishio katika Kijiji cha Ihebo wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuwasaidia kulipwa fidia ya miti zaidi ya 5,000 iliyokatwa na Mkuu wa wilaya hiyo, Corner Magembe, na kuitaifisha, huku maeneo ya makaburi yakigeuzwa kuwa matanuru ya kuchoma mkaa.

Baadhi ya wajane hao kwa niaba ya wenzao, walidai DC Magembe Septemba 26, mwaka huu akiwa na askari mgambo 40 pamoja na askari polisi alifika katika kijiji cha Ihebo na kuamuru kukatwa kwa miti hiyo mali ya familia 15 za kijiji hicho.

"Sisi tunachohitaji ni kulipya fidia maana miti aliyokatwa ni mali yetu na ukiangalia miti hii haikupandwa hivi karibuni ni ya miaka mingi tangu mimi nikiwa binti na sasa nina miaka 71.

"Tunashangaa kwa kile alichodai mkuu wa wilaya eti ni mali ya Shule ya Msingi Ihebo jambo ambalo sio sahihi,"alisema Mtimba Ngofila, mjane na mkazi wa Kijiji cha Ihebo.

Simon Machunda, mkazi wa kijiji hicho alisema mwaka 1928 lilianzishwa kanisa la Wasabato na lilianzisha Shule ya Msingi Ihebo mwaka 1933 ambapo miti hiyo iliyokatwa ikiwamo katika nyumba za wanakijiji, lakini mwaka 1967 serikali iliitaifisha shule hiyo na kuweka bikoni mwaka 2017 kwa usimamizi wa Polisi.

Alidai kuwa hawakuwatendea haki wanakijiji waliokuwa wamezunguka maeneo ya shule hiyo kwa kuwa ardhi na miti iliingizwa katika eneo la shule.

Aidha wajane hao pamoja na wakazi wa kijiji hicho walilalamikia kitendo cha eneo la hifadhi ya makaburi ambako kuna miti iliyokatwa kugeuzwa matumizi kutokana na baadhi ya wakazi wa kijiji hicho kuanza kulitumia kuchomea mkaa.

Fares Masembejo, mkazi wa Kijiji hicho ,alisema hatua ya hifadhi hiyo ya makaburi, jirani na uwanja wa Shule ya Msingi Ihebo kugeuzwa sehemu ya matanuru ya kuchomea mkaa imetokana na DC Magembe kuagiza miti zaidi ya 5,000 ya mbao na matunda yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 800 iliyodaiwa kupandwa ndani ya mipaka ya shule ikatwe mara moja.

Hatua ya mkuu huyo wa wilaya kuagiza miti hiyo ikatwe ni baada ya familia hizo kukaidi agizo lake la kutaka watu wote waliovamia mipaka ya shule kuvuna miti yao ndani ya siku 14.

"Mimi niliwapatia siku 14 familia ambazo zimevuka mipaka na kuingia ndani ya eneo la shule kwa makusudi na kuamua kupanda miti," alisema Magembe na kuongeza:

"Waivune na endapo watashindwa nitaivuna na kuitaifisha na kuwa mali ya shule na ndicho kilichotokea."



Mbunge wa Musoma Vijijini, mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (kulia) akizundua kampeni za Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, katika Kata ya Kiriba, wikiendi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waziri Mahiga aifunda THBUB

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Augustino Mahiga, ameitaka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), kuimarisha misingi ya utawala bora nchini ili kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa jamii nchini.

Akizungumza katika kikao kilichofanyika kwenye ofisi za Wizara ya Katiba na Sheria kati yake na Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mathew Mwaimu, alisema kuwa tume hiyo ni chombo muhimu ambacho kimepewa mamlaka ya kusimamia mambo mawili ambayo ni haki za binadamu na utawala bora.

"Mheshimiwa Rais anaposema serikali hii ni ya wanyonge, anataka wale watu walio kwenye mamlaka walijue hilo na wazingatie utawala bora katika kuhudumia jamii, na nyie ndio wenye jukumu la kuhakikisha misingi ya utawala bora inaimarika nchini," alisema Waziri Mahiga.

Dk. Mahiga alisema pamoja na changamoto zinazopigiwa kelele na wadau wa masuala ya haki za binadamu, lakini ni ukweli ulio wazi kuwa serikali ya awamu ya tano imetekeleza na inaendelea kutekeleza haki mbalimbali kwa vitendo na kuhakikisha haki hizo wananchi wanazipata.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sifuni Mchome, alieleza kuwa masuala ya haki za binadamu yanafanywa na taasisi nyingi, hivyo kipindi hiki wawekeze nguvu zao katika kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria nchini.

"Tume ni lazima muonekane mnachukua hatua, wekeni mkakati wa viashiria vya kubaini haraka changamoto zinazoelekea kuathiri utawala bora na kuzifanyia kazi," alisema Prof. Mchome.

Awali Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, alimuahidi Waziri Mahiga kuitumia vyema dhamana waliyopewa katika kusaidia serikali kutimiza lengo lake la kuifikisha nchi katika uchumi wa kati.

# Michikichi kuwa mbadala uagizaji mafuta

**Na Ashton Balaigwa, KIGOMA**

WAKATI Tanzania Ikitumia Sh. bilioni 443 kila mwaka kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi,Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI) imepanga kuendeleza zao la michikichi katika maeneo ambayo zao hilo linastawi.

Miongoni mwa maeneo hayo ni wilaya za Kyela (Mbeya), Mkuranga na Bagamayo (Pwani) Tanga na Zanzibar, lengo likiwa kuzalisha mafuta hapa nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, wakati wa ziara yake mkoani Kigoma kwa ajili ya kuangalia uzalishaji wa mbegu bora za michikichi kufuatia agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Dk. Mkamilo alisema mikoa hiyo ambayo imefanyiwa utafiti imeonekana ina uwezo mkubwa wa kustawi michikichi, hivyo kusaidia kuzalisha mafuta hatua ambayo itachangia kupunguza tatizo la uhaba wa mafuta ya kula nchini.

" Ipo mikoa ambayo ina fursa ya kulima zao la michikichi ukiachilia Mkoa wa Kigoma, sasa tumepanga kuongeza nguvu katika mikoa hiyo kwa kupeleka mbegu za kisasa na zenye tija kwa ajili ya kuhakikisha tunazalisha mafuta ya michikichi ili kumaliza tatizo la uhaba wa mafuta nchini," alisema Dk. Mkamilo.

Mkurugenzi wa TARI, Kihinga, Dk. Filson Kagimbo, alisema wamekuja na mkakati wa kufufua zao la michikichi kwa sababu linatoa mafuta mengi kwa ekari ukilinganisha na mazao mengine ambayo yanazalisha mafuta nchini.

Akizungumzia uzalishaji wa michikichi katika Mkoa wa Kigoma, alisema mkoa huo una nafasi kubwa ya kuongeza uzalishaji wa mafuta kwa wakulima wake kutumia mbegu bora, hivyo wanafanya utafiti ili kuongeza tija watoke kutoka tani 1.6 kwa hekta moja hadi tani 3-4 kwa hekta moja.

Alisema mkakati wa TARI ndani ya miaka mitatu ni kusambaza miche milioni 15 kwa wastani wa miche milioni 5 kwa kila mwaka, hatua ambayo itasaidia kupunguza gharama Serikali kwa ajili ya kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, iwapo Tanzania itafanikiwa kuongeza uzalishaji wa mafuta na ziada inaweza kuiuzia Kenya ambayo inaagiza asilimia 80 ya mafuta ya kula kutoka nje pamoja na nchi za Rwanda, DRC na Sudan.

Naye Kaimu Meneja Mtafiti wa Mazao kutoka TARI, Dk. Geofrey Kajiru, alisema kazi kubwa inayofanyika sasa ni kubadilisha mtazamo wa wakulima ili waachane na mbegu za zamani ambazo hazina tija na badala yake watumie mbegu za kisasa aina ya tenera ambazo zinatoa mafuta kwa wingi.

**" Ipo mikoa ambayo ina fursa ya kulima zao la michikichi ukiachilia Mkoa wa Kigoma, sasa tumepanga kuongeza nguvu katika mikoa hiyo kwa kupeleka mbegu za kisasa na zenye tija kwa ajili ya kuhakikisha tunazalisha mafuta ya michikichi ili kumaliza tatizo la uhaba wa mafuta nchini," alisema Dk. Mkamilo.**

## HABARI KIMATAIFA

# EU yajitenga na Marekani kisa wakimbizi

**WASHINGTON,** Marekani

UMOJA wa Ulaya (EU) umejitenga na uamuzi wa Marekani wa kubadili sera yake kuelekea ujenzi wa makazi ya walowezi unaofanywa na Israel kwenye ukingo wa magharibi.

**Hatushughulikii wala kutoa uamuzi wa mapema kuhusu hatima ya ukingo wa magharibi. Hilo ni kwa waisraeli na wapelestina kujadiliana.**

Washington imesema haizingatii tena kuwa ujenzi huo unakiuka sheria za kimataifa.

Mkuu wa sera za kigeni wa EU, Federica Mogherini, alisema msimamo wa umoja huo kuhusu sera ya makazi ya Israel hautobadilika kwa kuwa inakwenda kinyume na sheria za kimataifa.

Mogherini alisema sera hiyo ya Israel inaweka kizingiti juu ya uwezekano wa kupatikana suluhisho la mataifa mawili pamoja na amani ya kudumu kwenye mzozo kati ya taifa hilo na Palestina.

Matamshi yake yamekuja baada ya Marekani jana kutangaza kuunga mkono haki ya Israeli ya kujenga makazi ya wayahudi kwenye eneo inalolikalia kwa nguvu la ukingo wa magharibi.

Tangazo hilo lililotolewa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo lilisema Marekani imefikia hitimisho kwamba sera ya Israel kuhusu makazi ya walowezi haiendi kinyume na sheria za kimataifa.

Wakati wa mkutano wake na waandishi habari mjini Washington Pompeo alisema utawala wa Rais Donald Trump unabadili sera ya utawala wa Rais Mstaafu, Barack Obama kuelekea suala la makazi ya walowezi wa Israel.

"Hatushughulikii wala kutoa uamuzi wa mapema kuhusu hatima ya ukingo wa magharibi. Hilo ni kwa waisraeli na wapelestina kujadiliana. Sheria ya kimataifa hailazimishi matokeo wala haiweki kizingiti cha kisheria kwa suluhisho lililofikiwa baada ya majadiliano," alisema Pompeo.

Kulingana na Pompeo, matamshi ya Marekani kuhusu suala la makazi ya walowezi yamekuwa yakitofautiana.

Alisema mwaka 1978 Rais wa zamani, Jimmy Carter alihitimisha kuwa ujenzi huo ni kinyume cha sheria ya kimataifa lakini Rais Ronald Reagan alisema mwaka 1981 kuwa makazi hayo hayakiuki sheria. Kwa uamuzi huo, Marekani imeipa kisogo sera yake ya karibu miongo minne iliyobainisha kuwa ujenzi wa makazi kwenye eneo hilo unakiuka masharti ya sheria ya kimataifa.

Kadhalika tangazo hilo limefikisha idadi ya maamuzi matatu makubwa chini ya utawala wa Rais Trump kwamba Marekani imeegemea na kuipendelea Israel na kupuuza misimamo ya Palestina na mataifa ya kiarabu.

Uamuzi huo wa Marekani ni ushindi kwa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, anayehangaika kusalia madarakani baada ya chaguzi mbili zilizoshindwa kumwezesha kuunda serikali.

Netanyahu aliusifu msimamo huo mpya wa Marekani ambao hata hivyo umewakasirisha wapalestina wanaozingatia ujenzi wa makazi kwenye ardhi ya ukingo wa magharibi ni kinyume na sheria.

Mpatanishi mkuu wa Palestina kwenye mazungumzo ya amani, Saeb Erekat alisema hatua hiyo ya Marekani inarudisha nyuma kanuni za kimataifa za kutatua mizozo kwa njia za amani. **DW**

# Chuo Kikuu Hong Kong chazingirwa, Beijing yatoa vitisho

**HONGKONG,** China

WANAHARAKATI wa kupigania demokrasia wamekutana kwa siri wakiwa mafichoni katika makao makuu ya Chuo Kikuu cha Hong Kong, baada ya wenzao kuvamiwa usiku.

Wakati huo huo, China imesema haitofumbia macho hali ya vurugu inayoendelea Hong Kong na kutoa vitisho dhidi ya waandamanaji.

Hata hivyo, Rais wa Hong Kong ambaye yuko chini ya mamlaka ya China, Carrie Lam, aliwataka waandamanaji waliokimbilia katika Chuo Kikuu cha Hong Kong kuweza kujisalimisha haraka iwezekanavyo kabla ya hatua kali hazijachukuliwa.



Maandamano mjini Hong Kong yaliendelea mwanzoni mwa wiki hii, na makabiliano makali yalishuhudiwa baina ya Jeshi la Polisi na wanaharakati wa kupigania demokrasia walioingia ndani ya majengo ya chuo kikuu, na kushambulia polisi kwa fataki na mishale.

Polisi walitishia kutumia risasi za moto dhidi ya waandamanaji hao, endapo wasingeacha kuwalenga maofisa wake.

Miale ya moto iliyotokana na mfululizo wa milipuko ilionekana kutoka ndani ya majengo pindi maafisa wa Jeshi la Polisi wa kutuliza fujo walipoingia kwenye viunga vya chuo hicho siku ya jumatatu alfajiri. **RFI**



Distributed via ippmedia

Rais mpya wa Sri Lanka, Gotabaya Rajapaksa (kushoto), akiapa baada ya kutangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi kwa kupata kura zaidi ya asilimia 50. **PICHA: XINHUA**

# Askari 50 wauawa mapigano na waasi

**BUJUMBURA,** Burundi

JESHI la Burundi limepoteza askari zaidi ya 50 katika mapigano na watu wenye silaha yaliyotokea usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili katika Msitu wa Kibira, Wilayani Mabayi, Mkoani Cibitoke, Kaskazini Magharibi mwa nchi hiyo.

Vyanzo vya habari kutoka serikali ya Burundi na jeshi ambavyo havikutaka majina yao yatajwe vimethibitisha taarifa hiyo na kusema kuwa askari wengi waliuawa baada ya ngome yao inayopatikana katika eneo la Marura kuvamiwa, lakini vimesema kuwa shambulio hilo liliendeshwa Rwanda.

Hata hivyo, serikali ya Burundi na Jeshi bado hawajathibitisha kuhusu kutokea kwa tukio hilo. Lakini mashahidi kutoka Wilaya ya Mabayi wamethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubaini kwamba askari wengi wamejeruhiwa na wengine hawajulikani waliko.

Tarifa zaidi zilieleza kuwa hakuna kundi hata moja la waasi ambalo limekiri kuhusika na shambulio hilo, lakini hivi karibuni kundi la waasi la Red-Tabara lilitangaza kuwa limeanzisha vita dhidi ya utawala wa Rais wa Burundi, Pierre Nkurunziza.

Kwa mujibu wa vyanzo kadhaa kutoka Wilaya ya Mabayi, raia wanaoishi karibu na Msitu wa Kibira wamelazimika kuyahama makazi yao kufuatia kuzorota kwa hali ya usalama katika eneo hilo.

Burundi inaendelea kukumbwa na hali ya sintofahamu ikiwa imesalia miezi isiozidi kumi kabla ya uchaguzi wa urais. **RFI**

# Uturuki kuweka viwanda Simiyu

**Na Mwandishi Wetu, Simiyu**

KATIKA kutekeleza Diplomasia ya Uchumi, Ubalozi wa Tanzania nchini Uturuki umeambatana na wawekezaji kutoka nchini humo kwa ajili ya kuwekeza katika viwanda mkoani Simiyu ambavyo vinatarajiwa kutoa zaidi ya ajira 2,000.

Uwekezaji huo utajumuisha kiwanda cha nguo na cha kutengeneza vyombo vya nyumbani ambao una thamani ya dola za kimarekani milioni 50.

Viwanda hivyo vitajengwa katika eneo la Isanga, Bariadi na vinatarajiwa kuanza uzalishaji mwakani.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika eneo ambalo linatarajiwa kujengwa viwanda hivyo, mwekezaji huyo, Mustafa Albayram, alisema ameridhishwa na mazingira ya uwekezaji baada ya kutembelea maeneo mbalimbali kwa lengo la kuangalia mazingira wezeshi.

Mwekezaji huyo akiwa ameambatana na Balozi wa Tanzania nchini Uturuki, Prof. Elizabeth Kiondo, aliiomba serikali kutatua baadhi ya changamoto ili kuuwezesha uwekezaji huo.

Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na miundombinu yote muhimu hususani ya umeme ili uwekezaji huo uanze mara moja baada ya kukamilisha taratibu zote zinazohitajika ikiwa ni pamoja na usajili wa kampuni na kutafuta hati miliki ya ardhi.

"Tumeamua kuwekeza Simiyu, kila kitu kikienda sawa kiwanda cha nguo kinaweza kujengwa na kufanya kazi ndani ya miezi tisa mpaka mwaka mmoja. Kiwanda cha vyombo vya nyumbani miezi minane baada ya usajili wa kampuni. Nitarudi tena Simiyu kukamilisha masuala ya hati miliki ya ardhi, sitaki kumwangusha Balozi maana amefanya mengi kwa ajili yetu," alisema Albayram.

Naye Prof. Kiondo alisema mwekezaji ameridhishwa na eneo hilo na kuushukuru uongozi wa Mkoa wa Simiyu kwa kutoa ardhi ya kujenga viwanda hivyo huku akibainisha kuwa ombi kubwa la mwekezaji ni upatikanaji wa nishati ya kutosha kwa kuwa viwanda hivyo hutumia umeme mwingi.

Balozi Kiondo aliongeza kuwa hayo ni matokeo ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa vitendo, hivyo ubalozi utaendelea kuhamasisha wawekezaji wengine zaidi kuwekeza nchini, hatimaye kufanikisha azma ya uchumi wa viwanda.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alimhakikishia mwekezaji huyo upatikanaji wa mahitaji yote muhimu na kuahidi kushirikiana na taasisi za serikali zinazohusika kuhakikisha anapata huduma zote kwa wakati na pasipo urasimu wowote.

Kuhusu umeme, Mtaka alisema katika bajeti ya mwaka 2019/20, Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoozea umeme ambacho kitajengwa karibu na eneo la uwekezaji huo.




Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse (kulia), akijipongeza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (kushoto), wakati wa ufunguzi wa tawi jipya la benki ya Exim Mtaa wa Mkwepu jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## DC aagiza makandarasi mradi kuswekwa ndani

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, ameagiza kuswekwa ndani kwa makandarasi wawili raia wa China wa Kampuni ya CRJE kwa kushindwa kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata taka kilichoko Mabwepande, jijini Dar es Salaam.

Chongolo alifikia uamuzi huo jana baada ya kampuni hiyo kushindwa kukamilisha mradi huo kwa wakati huku Mhandisi Mshauri wa Manispaa, Emanuel Tilya, akisisitiza kuwa wamekuwa hawatoi ushirikiano licha ya kwamba yuko kwenye eneo la mradi.

Akizungumza wakati wa ziara aliyoifanya jana ya kukagua miradi inayojengwa na halmashauri hiyo, Chongolo alisema kwa muda mrefu amekuwa akizungumza na mkandarasi huyo kuhusu kukamilisha mradi huo kwa muda uliopangwa lakini hakufanya hivyo.

Alisema halmashauri inahitaji kiwanda hicho haraka ili kutumiwa na wananchi ambao ndio wanufaika wa mradi huo lakini mkandarasi aliyepewa kazi hiyo anawarudisha nyuma.

Kwa mujibu wa Chongolo, halmashauri imeshawalipa fedha kwa ajili ya ujenzi huo lakini kinachofanyika ni fedha hizo kuzipeleka kwenye miradi yao mingine jambo ambalo limefanya hadi sasa kusuasua kwa mradi.

"Nimekuja hapa zaidi ya mara tatu. Mara ya kwanza nilikuja nikaongea nao wakaniahidi watakamilisha kwa muda uliopangwa. Mara ya pili nilikuja hapa nikafoka hadi nikakasirika lakini hali imeendelea hivi hivi. Sasa sijawakamata nimewashikilia hadi pale watakapoleta mpango kazi wao uliojitosheleza," alisema Chongolo.

"Hatuwezi kukaa na watu wa namna hii, tumetoa pesa nyingi kwa ajili ya kukamilisha mradi huu mapema halafu wanatuchezea. Kama wataleta leo, kesho nitawaachia, kadiri watakavyowahi kuniletea huo mpango kazi wao ndio na mimi nitawaachia, askari kamata hao waweke ndani.

# Serikali yakuna Baraza la Kilimo bei ya mazao

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Baraza la kilimo Tanzania, umeipongeza Serikali kutokana na uamuzi wake wa kutangaza kutokuingilia kupanda kwa bei ya mazao ya mahindi.

Umesema kwamba uamuzi huo wa kutiongilia bei hasa ya mahindi na unga utazidi kumsaidia mkulima kuanza kunufaika na sekta ya kilimo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Kilimo Tanzania, Jacquliene Mkindi jana jijini Arusha, uamuzi wa Serikali wa kutokupanga bei elekezi kwa mazao hayo ni hatua muhimu katika kutetea nafasi ya mkulima katika kilimo biashara na soko huru..

"Sisi kama Baraza la Kilimo kwa dhati kabisa tunaipongeza Serikali kwa uamuzi wake huu wa kutetea soko huru la mazao kwa kutokupanga bei elekezi kwa wakulima wa mahindi, hii inazidi kuonyesha dhamira njema ya Serikali ya kuzidi kumsaidia mkulima wa Tanzania," alisema Mkindi.

Taarifa imeeleza kuridhishwa kwa na utendaji kazi wa viongozi wa juu wa Wizara ya Kilimo, na kwamba mara kadhaa wamekuwa wakisikika wakimtetea mkulima kwa kulinda mazao yake baada ya kutoka shambani.

"Waziri wa Kilimo amekaliliwa akitoa msimamo wa Serikali wa kutokupanga bei elekezi kwenye unga na mahindi jambo hili ni jema sana, lakini pia hata Naibu wake aliwahi kusema Serikali haina mpango wa kuzuia kuuza mazao nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kutokupanga bei elekezi kwa mazao ya kilimo, Sisi kama Baraza la Kilimo kwa niaba ya wakulima nchini tunafarijika sana tukisikia kauli hizi zikitoka kwa viongozi wetu," alisema Mkindi.

Hivi karibuni akijibu swali bungeni Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisisitiza msimamo wa serikali wa kutokuingilia na kupanga bei elekezi kwa mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuondoa marufuku ya uuzaji wa mazao nje ya nchi.

"Ni matumaini ya Baraza kuwa kama sera za kutoingilia masoko zikidumishwa, baada ya miaka michache ijao Tanzania itakuwa mzalishaji mkubwa wa chakula hasa mahindi na mchele na kuwa mazao haya yatakuwa ni miongoni mwa mazao yatakayowakomboa wakulima kiuchumi kwani kuna soko kubwa kwa nchi zinazotuzunguka," ilisema taarifa hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza la Kilimo, Janet Bitegeko, alisema kwa sasa Tanzania inazalisha zaidi ya tani milioni 6 za mahindi na kwamba lengo ni kufikia tani milioni 8 ifikapo20/2021,

"Sisi kama Baraza tunaamini kama wakulima watapata bei nzuri kwa miaka 3 au 4 mfululizo bila kuingiliwa, kuna uwezekano mkubwa wa kufikia uzalishaji wa tani milioni 15 za mahindi kwa mwaka, kwa sababu wakulima wengi zaidi watakuwa na ari kubwa," alisema.

"Tunaamini wakulima wakiendelea kupata bei nzuri watakuwa na uwezo wa kununua pembejeo kama mbolea, madawa na mbegu bila ya ruzuku yoyote kutoka serikalini na uzalishaji utaongezeka hivyo hata bei nazo zitashuka," aliongeza.

Taarifa hiyo ya Baraza la Kilimo imewataka wakulima kote nchini kutumia fursa hiyo vema kwa kuongeza uzalishaji wenye tija ili kupata faida kwa ajili ya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MASHINE INAUZWA** DE-OILING MACHINE. Mashine ya kukausha mafuta kutoka katika vyakula vilivyokaangwa na mafuta kwa mfano Crisps, karanga, korosho nk. Kwa mawasiliano: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**MASHINE INAUZWA,** SEASONING MACHINE. Mashine ya kuchanganya chumvi au pilipili nk. Kwenye vyakula kama karanga, korosho, crisps nk. Kwa mawasiliano piga simu namba: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.


**MASHINE INAUZWA,** PACKING MACHINE. Mashine ya kupaki karanga, korosho, crisps nk. Kwa mawasiliano piga simu namba: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila*

### KUPOTEA KWA PASIPOTI




**CHARLES GASPAR MPERA**

anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam tarehe **12/09/2018** na itaisha muda wake **11/09/2028.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi:
**KMT/RB/2880/2019.**

XXXXXX

### KUPOTEA KWA CHETI




**Asnah S. Msuakollo anatangaza kupotea kwa cheti cha nne chenye index namba S.1665-0013 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Nyasaka.**

**Yeyote atakaekiona atoae taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: KU/B/1/VOL/00.**

115524702

### KUPOTEA KWA VYETI



**KHERI KASSIM NGEMERA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4104-0533 kilichotolewa na ANDREW FAZA MEMORIAL SEKONDARI mwaka 2009. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S2365-0031 kilichotolewa na LORD BADEN POWELL MEMORIAL HIGH SCHOOL mwaka 2012.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi:**
**DAR/KIJ/RB/384998/2019.**

### KUPOTEA KWA KADI

**ERNEST MWITA NYAMHANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TATA-BUS** yenye namba ya usajili **T489 DDH** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**GE/TR/RB/9162/019**


115525202

### KUPOTEA KWA KADI

**ERNEST MWITA NYAMHANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TATA-BUS** yenye namba ya usajili **T785 DCQ** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**GE/TR/RB/9162/019**

115525202

### KUPOTEA KWA VYETI



115525502

**Fedrick G. Masigati** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0754-0037** kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2003 katika shule ya Sekondari Urambo, Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba P0119-0588** kilichotolewa na Baraza la Mithihanila Taifa mwaka 2009 Shule ya Sekondari Kibaha na cheti cha Chuo kilitolewa na Chuo Huria Tanzania mwaka 2017. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi taarifa : **DAR/GOG/RB/486453/2019**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No; 234/2019

Ombi la RASHID HAMSINI MGAZA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HALIMA SELEMANI KISWILI.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/11/2019

115524602

Distributed via ippmedia

### KUPOTEA KWA KADI

**GOSBERT B. BLANDES** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina **Toyota Land Cruiser** yenye usajili wa namba **T250 APR** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/URA/RB/483369/2019**

115525602

### KUPOTEA KWA KADI

**ADAM RWEBANGILA JOSEPHAT** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina **Mitsubishi Canter** yenye usajili wa namba **T222 BAV** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona ataoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/URA/RB/483374/2019**

115525602

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**Ndugu Jovenary Mutalemwa Joseph** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 565 DJY MITSUBISHI ROSA.** NAMBA YA CHASSIS **BE63CE300012.** NAMBA YA ENGINE **4D33EAA0012.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**MBE/MBE/RB/487384/2019**

115525402

Kwa Habari Moto-moto usikose Gazeti lako la

NJOO UTANGAZE
BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# HAZARD APUUZA UZITO AKISISITIZA YUPO FITI

**MADRID,** Hispania

WINGA wa Real Madrid, Eden Hazard amesisitiza yupo "kwenye hali nzuri" baada ya kukumbana na shutuma juu ya kuongezeka uzito wake na analifanyia kazi suala hilo msimu huu.

Hazard alihamia Real kutoka Chelsea kipindi cha majira ya joto kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 100 na ingeweza kuongezeka hadi pauni milioni 130 kutokana na bonasi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa na wakati mgumu tangu atue Bernabeu akifunga bao moja tu katika mechi 11 za La Liga na Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa kiwango chake kimeimarika katika siku za hivi karibuni, akitoa pasi za mwisho tatu kwenye mechi nne alizocheza.

Alishutumiwa na vyombo vya habari mwanzoni mwa msimu huu, ambavyo vilidai kwamba, alitua Hispania akiwa ameongeza uzito, huku mapema mwezi huu, kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger akimuelezea Hazard kama "mzito sana."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye kwa sasa ndio anapigania kupunguza uzito, mapema wiki hii mchezaji mwenzake wa zamani wa Chelsea, John Obi Mikel alimuelezea kama "mchezaji aliyezubaa zaidi aliyewahi kucheza naye."

Hata hivyo, akizungumza na Sky Sports, Hazard alisisitiza kwamba yupo fiti na "mara zote" atajaribu kuwa kwenye ubora wake, akiwa na Real au Ubelgiji.

"Kwa kipindi cha mwezi uliopita nimejiona kuwa niko kwenye wakati mzuri," alisema.

"Nipo kwenye hali nzuri. Wakati nikiwa uwanjani mara zote najaribu kuwa kwenye ubora wangu, pamoja na Real Madrid au Ubelgiji. Ndio kwanza nimeanza kuwa kwenye kiwango changu."

Distributed via ippmedia

# Low aitoa Ujerumani kubeba taji Euro 2020

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA Joachim Low haamini kama Ujerumani inaweza kuchukuliwa kama moja ya timu yenye nafasi ya kushinda Euro 2020, akidai kwamba, England, Hispania, Ufaransa, Italia na Ubelgiji zipo juu ya kikosi chake.

Ujerumani ilifuzu kucheza michuano hiyo ya mwakani baada ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Belarus Jumamosi.

Kufuzu kwako kumekuja baada ya kuwa na matokeo mabaya kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana, wakati waliokuwa mabingwa hao watetezi wakatolewa kwenye hatua ya makundi.

Kikosi cha Ujerumani kimefanyiwa marekebisho mwaka jana huku Mats Hummels, Jerome Boateng na Thomas Muller hawaonekani kuwa tena chaguo kwenye kikosi hicho, huku Mesut Ozil alistaafu kucheza soka la kimataifa, akishutumu kubaguliwa na Shirikisho la Soka la Ujerumani.

Kikosi hicho cha Low kilishinda mechi sita kati ya saba kwenye michuano ya kufuzu Euro 2020, wakifunga mabao 24, lakini kocha huyo anaamini kikosi chake kinatakiwa kujiimarisha zaidi.

"Nafikiri, tumeridhishwa na kiwango cha timu mwaka huu," alisema Low akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa Jumanne dhidi ya Ireland Kaskazini.

"Linapokuja suala la maendeleo, kwa uhakika kabisa kuna mataifa yako mbele yetu kwa ubora.

"England, Hispania, Ufaransa, Italia na Ubelgiji – hizi ni timu ambazo naziona kabisa kwamba zipo mbele yetu kwa ubora.

"Michuano iliyopita kwa mfano, England walifanya maajabu makubwa kwenye Kombe la Dunia na bado wana nafasi kubwa kwenye michuano hii ya Euro."






# *Klopp ataka VAR iboreshwe zaidi*

**NYON,** Uswisi

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alitumia mkutano wa makocha wa Klabu za UEFA kutaka mabadiliko kwenye mfumo wa Teknolojia ya Maamuzi ya Usaidizi wa Video, VAR.

Mkutano huo ambao uliwahusisha makocha wote wa Klabu za Ulaya ulifanyika mjini Nyon nchini Uswisi, pamoja na Klopp pia ulihudhuriwa na kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.

Guardiola aliachwa amekasirika baada ya VAR kusaidia Liverpool kufungwa mabao 3-1 wakati City wakikataliwa penalti mbili. Huku Klopp akiwa mnufaika wa VAR, Mjerumani huyo alisisitiza kwenye mkutano huo kwamba VAR inatakiwa kuboreshwa zaidi, ambapo Guardiola alionekana kuunga mkono kauli hiyo.

Ilionekana kwamba mpira uligonga mkono wa beki wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold kwenye eneo la penalti kabla ya kocha wa 'Wekundu' hao kupata bao la ufunguzi kupitia Fabinho, lakini VAR ilikataa kuwa mpira uligonga mkono.

"VAR inaweza kuboreshwa, inawezekana. Haiwezi kuwa sahihi kwa asilimia 100, kila mmoja anajua hilo. Lakini kuna vitu vingi ambavyo haviko sawa," alisema Klopp kwenye mkutano huo.

# Barca bega kwa bega na Valverde - Abidal

**BARCELONA,** Hispania

ERNESTO Valverde anasapoti yote kutoka kwa uongozi wa Barcelona kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo, Eric Abidal, huku akiwaweka mbali 'Blaugrana' hao kutoka "klabu zinazobadilisha makocha baada ya matokeo mabaya."

Barcelona wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, wakiwa pointi sawa na Real Madrid lakini kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Levante na sare ya bila kufungana na Slavia Prague kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, ilionesha shaka ya uongozi wa Valverde.

Ronaldo Koeman amekuwa akitajwa kama ndiye mtu sahihi anayeweza kumrithi Valverde.

Lakini Abidal alibainisha kwamba, nafasi ya Valverde kamwe haijawahi kuwa kwenye mjadala wa uongozi wa timu hiyo, licha ya kubainisha wazi kwamba, ushindi wa LaLiga na kutolewa kwa Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Roma msimu wa 2017-18 kisha na Liverpool msimu wa 2018-19 mashabiki walionyesha kutokuwa na imani naye.

"Mara zote nasikia mjadala kuhusu Valverde," alisema Abidal akiiambia SPORT.

"Sawa na kile kichotokea Roma na Liverpool. Kwa sababu matokeo yanaweza kukufanya ufikiri kuhusu msimu mzima. Na hasa kwa namna ilivyotokea.

"Katika hali hii, unaweza kufikiri kwamba ndiye mtu wa kulaumiwa, lakini unaitwa kuchambua mambo kwa kina. Kocha analeta nini kwa wachezaji na kinyume chake?

"Tunamsapoti kocha na tunampa taarifa zote, ingawa anapewa kila siku na tumemhakikishia hilo."





# POCHETTINO ANAWEZA KUFUKUZWA TOTTENHAM

**LONDON,** England

NI wazi kwamba, siku za kocha wa Tottenham Hotspurs, Mauricio Pochettino zinahesabika, kwa mujibu wa ESPN.

Wakati Pochettino akiwa amekalia kuti kavu, makocha watatu Eddie Howe, Julian Nagelsmann na Carlo Ancelotti wanahusishwa kutua White Hart Lane.

Chanzo kimoja kutoka ndani ya klabu hiyo kimeitonya ESPN kwamba, kuna mazungumzo yanaendelea baina yake na uongozi wa Spurs kuhusu kuvunja mkataba.

Huenda nyota huyo wa zamani wa Argentina akafungashiwa virago muda mfupi ujao.

Matokeo mabaya yameweka rehani kibarua cha Pochettino ambapo tangu kuanza msimu huu timu hiyo haichezi katika kiwango bora.

Spurs inashika nafasi ya 14 katika ligi ikiwa nyuma kwa pointi 20 dhidi ya vinara Liverpool wenye alama 34.

Licha ya Spurs kufika fainali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, vigogo wa klabu hiyo wanamuona Pochettino hatoshi.

Uvumi wa kocha huyo kung'olewa Spurs ulikolezwa na wachezaji mwezi uliopita, lakini alivuka kihunzi hicho.

Licha ya kuonekana hafai Manchester United, Real Madrid na Paris Saint Germain zote zinamtolea macho.

Distributed via ippmedia

# Gareth ahofu Euro 2020 kumkosesha Qatar 2022

**LONDON,** England

GARETH Southgate amebainisha kwamba ugumu wa michuano ya Euro 2020 unaweza kusababisha mtu mwingine kabisa kuiongoza England kwenye Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar.

Ushindi dhidi ya Montenegro na Kosovo ulishuhudia wakipanda kileleni mwa Kundi A na kuonekana kuwa moja ya timu yenye nafasi kubwa kwenye Euro 2020, ambapo 'Simba Watatu' hao mechi zao za makundi inacheza kwenye Uwanja wa Wembley.

Kocha huyo amesema kwamba, kwa namna anavyoiona michuano hiyo, ni wazi kwamba itakuwa migumu na pengine kibarua chake kikaishia hapo na mtu mwingine kuiongoza England kwenye Kombe la Dunia 2022.

"Ndiyo, hiyo itategemea na namna tutakakofika kwenye michuano ijayo," alisema kocha huyo wa England maarufu kama Simba Watatu, ambaye mkataba wake unamalizika baada ya Kombe la Dunia Qatar mwaka 2022. "Ukiwa na wiki kama tuliyokuwa nayo, unaweza kuona kwamba, watu wanakuwa hawana tena mapenzi na wewe na hilo likiianza kutokea, unatakiwa kukaa pembeni.

"Hivyo, kwa uhakika kabisa najua namna gani kazi hizi zinavyobadilika kwa uharaka, lakini mara zote huwa tunapanga kwa muda mfupi.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AFUTA BAO LA SUAREZ USIKU

**Ni wakati washambuliaji hao wawili wa Barca wakifunga na kutoa pasi za mwisho Argentina na...**

**TEL AVIV,** Israel

ARGENTINA imelazimika kusubiri ['bao la usiku'] dakika za majeruhi kupitia mkwaju wa penalti uliozamishwa kimyani na Lionel Messi ili kuweza kuambualia sare dhidi ya mahasimu wao soka Amerika Kusini, Uruguay.

Katika mechi hiyo ya kirafiki iliyopigwa mjini Tel Aviv, Israel na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2, mshambuliaji mwenza wa Messi katika klabu ya Barcelona, Luis Suarez ndiye aliyetaka kuilaza Argentina mapema na viatu baada ya kuifungia Uruguay bao la pili dakika ya 68 kwa mpira wa adhabu ndogo kabla ya beki wa kati Martin Caceres kuunawa mpira ndani ya 18 na kusababisha penalti hiyo.

Edinson Cavani alifungua mlango wa mabao hayo kwa Uruguay katika dakika ya 34, bao ambalo lilidumu kipindi chote cha kwanza lakini baada ya mapumziko, dakika ya 63 Sergio Aguero aliisawazishia Argentina.

**Messi alikuwa katika mhemko wa ushindi tangu mwanzo wakati akikabiliana na changamoto mara nne katika kipindi cha kwanza, lakini jaribio la shuti lake lilitoka nje ya lango.**

Mshambuliaji huyo ambaye alifunga wakati wakishinda dhidi ya Brazil Ijumaa katika mechi yake ya kwanza kuichezea Argentina tangu Julai, mwaka huu alihusika katika mabao yote mawili kwenye mechi hiyo ya juzi nchini Israel.

Kwanza, mpira wake wa faulo ndogo aliopiga uliunganishwa kimyani kwa kichwa na mshambuliaji wa Manchester City, Aguero na kisha akaipatia timu yake sare kwa kuzamisha mkwaju wa penalti kimyani ikiwa ni baada ya awali kipa wa Argentina, Esteban Andrada kushindwa kucheza mpira wa faulo wa Suarez uliozama nyavuni na kufanya wapinzani wao hao kuwa mbele kwa mabao 2-1.

Lakini pia Suarez naye alihusika katika mabao yote mawili ya Uruguay kufuatia kupokea pasi ndefu kutoka kwa kiungo Lucas Torreira na kisha kumpasia Cavani ambaye hakufanya makosa kuuzamisha kimyani na kumwacha kipa Andrada akiwa hana la kufanya.

Timu zote mbili sasa zitatupia jicho katika nafasi ya kutoka ukanda wa Shirikisho la Soka Amerika Kusini (CONMEBOL) kufuzu Kombe la Dunia 2022 katika droo itakayofanyika Desemba 3, mwaka huu wakati raundi ya kwanza ya kinyang'anyiro hicho cha kusaka tiketi ya Qatar 2022 kikipangwa kuchezwa Machi mwakani.

## ZISIKUPITE

### BENITEZ KUMRITHI PELLEGRINI

WEST Ham watamgeukia Rafael Benitez kama wataamua kuachana na kocha Manuel Pellegrini. ***(Mirror)***

### POCHETTINO, LEVY KUTETETA

MAURICIO Pochettino amefanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy kuhusu mustakabali wake wa baadaye hapo Tottenham. ***(Telegraph)***

### WILLIAN AIGOMEA CHELSEA

KIUNGO wa Chelsea, Mbrazil Willian, 31, anajiandaa kukataa ofa ya kuongezewa mkataba wa miaka miwili na kusubiri hadi huu wa sasa utakapomalizika mwishoni mwa msimu ili kufanikisha kujiunga na Barcelona. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### NEYMAR AIKATALIA PSG

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Neymar, 27, amekataa nafasi ya kuongeza mkataba hapo Paris St-Germain kufuatia huu wa sasa unaomalizika mwaka 2022. ***(Sport)***

### ENRIQUE ANA NAFASI HISPANIA

SHIRIKISHO la Soka Hispania limetoa ofa ya nafasi kwa kocha Luis Enrique kurudi kuinoa timu ya taifa. ***(AS)***

### SMALLING ATAKIWA JUVE, INTER

JUVENTUS na Inter Milan zimeeleza nia yao ya kutaka kumsajili beki wa Manchester United na England, Chris Smalling, 29, anayeichezea Roma kwa mkopo kwa sasa, ambaye thamani yake ni zaidi ya pauni milioni 15. ***(Sun via Corriere della Sera)***

### KUMFUATA SZOBOSZLAI

ARSENAL inapanga kutuma mashushushu wake kumfuatilia kiungo wa Red Bull Salzburg raia wa Hungary, Dominik Szoboszlai, 19. ***(Football Insider)***

### POGBA KUITOSA REAL KWA JUVE

KIUNGO wa Manchester United, Mfaransa Paul Pogba, 26, angependelea zaidi kurudi Juventus kuliko kujiunga na Real Madrid. ***(Tuttosport - in Italian)***

### GUARDIOLA ATAJWA BAYERN

WAKALA wa Pep Guardiola, hawezi kuweka kando uwezekano wa kocha huyo wa Manchester City kurudi mapema kuinoa Bayern Munich. ***(AS)***

### FERNANDES ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inaweza kummiliki kiungo Mreno Bruno Fernandes, 25, katika dirisha la usajili la Januari kufuatia Sporting Lisbon kuripotiwa inahitaji kutengeneza fedha kwa ajili ya kulipa madeni yanayokadiriwa kuwa pauni milioni 57. ***(O Jogo - in Portuguese)***

### CHELSEA, LIVER KWA BERGE

CHELSEA imetia mguu kwa kiungo wa Genk, Mnorway Sander Berge, 21, ambaye pia yupo kwenye rada za Liverpool na Napoli. ***(Goal.com)***

### FERGUSON KUWEKWA SOKONI

WESTBROM inafikiria kumuuza beki wa England U-20, Nathan Ferguson, 19, katika dirisha la usajili la Januari kama mchezaji huyo hatakubali kuongeza mkataba wake wa sasa ambao unamalizika majira ya joto. ***(Express and Star)***

HABARI MICHEZO

## Kenya yatisha kwa hat-trick

**Na Adam Fungamwango**

MICHUANO ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake, imeendelea kuweka rekodi ya kufungwa mabao mengi, lakini juzi rekodi mpya ikiandikwa kwa kupatikana penalti nne na hat-trick tatu katika mchezo mmoja.

Katika mchezo wa mapema jana, Djibouti iliendelea kuwa jamvi la wageni kwenye michuano hiyo baada ya kubugizwa mabao 12-0 dhidi ya Kenya kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

Hiki ni kipigo cha pili kwa timu hiyo, kwani kwenye mechi ya kwanza ilikumbana na dhahama ya kupigwa mabao 13-0 dhidi ya timu ya Taifa ya Uganda kwenye uwanja huo huo.

Kwa matokeo hayo, Kenya inasonga mbele kwa kutinga hatua ya nusu fainali kwenye Kundi B, baada ya mechi ya kwanza kuichapa Ethiopita mabao 2-0, hivyo kukusanya pointi sita.

Kwenye mechi hiyo, Mwanalima Adam alifunga 'hat-trick' kwa mabao yake ya dakika ya 34, 87 na 89, huku Mercy Airo akifunga naye 'ha-trick' kwa kutupia dakika ya 54 na 66 yote kwa penalti na akakamilisha dakika ya 61.

Mchezaji mwingine aliyefunga 'hat-trick' ni Jentrix Milimu dakika ya 16 kwa penalti kisha akarudi kambani dakika ya 14 na 56 kabla ya kutupia la nne kwa mkwaju wa penalti dakika ya 86. Janeth Bundi alifunga dakika ya 45 na Vivian Corazine alipachika bao lake dakika ya 15.

## JKT Tanzania yaitishia Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Bakhresa, amesema kikosi chake kipo fiti kukutana na Yanga Jumamosi katika mchezo wa Ligi Kuu utakaopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema ameutumia vizuri muda huu wa mapumziko kupisha mechi za kimataifa, kuipa mbinu mpya timu yake akiwa na lengo la kuibuka na pointi tatu ili kujisogeza katika nafasi za juu.

"Lengo langu ni kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu ambayo msimu huu imekuja kivingine," alisema.

Aliwataka mashabiki wao kuendelea kuisapoti timu hiyo na kuahidi kufanya vizuri katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa.

"Nashukuru wachezaji wangu wana morali ya juu kuendelea kubakia kwenye Ligi Kuu, naamini kila kitu kinawezekana," alisema.

JKT Tanzania inashikilia nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 15 baada ya kushuka dimbani mara 10 msimu huu.

# KILI QUEENS DIMBANI IKIWAZA NUSU FAINALI

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI leo akikiongoza kikosi chake dimbani kuwavaa ndugu zao wa Zanzibar (Zanzibar Queens) kwenye mechi ya mwisho ya hatua ya makundi kuwania ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Queens), Bakari Shime, amesema akili yake sasa ni mchezo wa nusu fainali.

Juzi, kikosi hicho cha Shime kiliisambaratisha Burundi kwa mabao 4-0 ikiwa ni baada ya kuichapa Sudan Kusini mabao 9-0 katika mechi ya ufunguzi.

**Na leo Kilimanjaro Queens itashuka dimbani kuivaa Zanzibar Queens katika mchezo ambao ni kama wakukamilisha ratiba kwa timu zote mbili kutokana na kikosi hicho cha Shime kufuzu hatua ya nusu fainali wakati ndugu zao hao wa Zanzibar wakiwa wameshaaga mashindano hayo kutokana na kupoteza michezo yote miwili.**

Akizungumza na Nipashe jana, Shime alisema wamejipanga vizuri wakiwa na lengo la kuweka historia ya ubingwa kwa kutwaa kombe hilo kwa mara ya tatu mfululizo.

"Nashukuru wachezaji wangu wamejituma mpaka tumefanikiwa kuingia hatua ya kucheza nusu fainali, kikubwa ni kuzidi kumtanguliza Mungu mbele," alisema Shime.

Alisema mashindano hayo yana ushindani na changamoto nyingi kutokana na timu zote kufanya maandalizi makubwa.

"Mashindano yana ushindani, kila timu imejipanga vizuri ili kupata ubingwa kila mchezo huwa tunacheza kwa tahadhari kubwa," alisema kocha huyo.

Aidha, alisema wamejipanga vizuri kukutana na Zanzibar Queens leo na lengo lao ni kuendelea kushinda hadi kulitwaa taji hilo.



Winga wa Kilimanjaro Queens na mfungaji wa mabao mawili, Donisia Minja, akipasua katikati ya mabeki wa Burundi wakati wakishinda 4-0 kwenye mechi Cecafa Chalenji kwa wanawake iliyopigwa katika Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Distributed via ippmedia

## *Z'bar Heroes yaundiwa Kamati ya Hamasa*

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MWENYEKITI wa Kamati ya Hamasa ya timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mahmoud Mohammed, ametangaza wajumbe 19 watakaoshirikiana kwa karibu katika kuhakikisha wanatekeleza vema jukumu hilo.

Hivi karibuni Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, alimteua Mohammed kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa ya Zanzibar Heroes na kutakiwa kuunda safu yake ya wajumbe watakaoshirikiana naye.

Akiwatangaza wajumbe hao mbele ya vyombo vya habari katika Ukumbi wa Mikutano wa ZFF, Mohammed aliwataja kuwa ni Katibu wa ZFF, Mohamed Ali Hilal, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman na Kocha Mkuu wa Zanzibar Heroes, Hemed Suleiman Morocco.

Wengine ni Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'B', Rajab Ali, Mkuu wa wilaya ya Kusini Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, Katibu wa Wizara ya Vijana Sanaa Utamaduni na Michezo, Omar Hassan Omar 'King' na Ali Saleh Alberto Mbunge wa Mjimkongwe.

Wajumbe wengine ni Meneja wa Zanzibar Heroes, Ali Mohammed Ameir, Ofisa Habari wa ZFF, Hassan Mussa, Bahatisha Awaz Suleiman, Issa Kasim Issa na Omar Said Shaabani.

Wengine ni Ali Salim Ali Jazira Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, iraji Kwanzam Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni, Mohammed Said Dimwa Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Lagit Ali Ferji, Salula Hilali Salum Kisoda kutoka Pemba na Hafidh Ali Mohamed wa Pemba.

Akizungumza mara baada ya kumaliza kutaja wajumbe hao, mwenyekiti huyo alisema lengo la kamati hiyo ni kuijenga Zanzibar Heroes ambayo inatarajia kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) mwezi ujao nchini Uganda.


Alisema anaamini kwa kupitia kamati hiyo hakuna ambacho kitaharibika, hivyo aliwataka kuwa kitu kimoja ili kuona timu hiyo inakamilisha malengo yake.

Aidha, alisema wako katika mchakato wa kuunda kamati ndogo ya hamasa kwa waandishi wa habari za michezo ambayo itakuwa mbele katika kutangaza habari za timu hiyo kwa ajili ya kuwapasha habari Wazanzibar juu ya kinachofanyika katika timu hiyo ya Taifa, huku akiwataka wananchi kuichangia.

Alisema kamati hiyo ina mipango mingi ikiwamo kutoa jezi ya timu ya taifa ambayo itazinduliwa rasmi, hivyo aliwataka wananchi kuwa tayari kununua jenzi hiyo pindi itakapozinduliwa.

"Lengo ni kuichangia timu yao na si jingine, endapo wakinunua jezi hizo watakuwa wameichangia pakubwa," alisema.

Michezo
Jumatano Novemba 20, 2019
Nipashe



Messi afuta bao la Suarez usiku

UKURASA 30

MSITU...



Distributed via ippmedia

Mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, akipata upinzani mkali kutoka kwa 'msitu' wa mabeki wa Uruguay kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa Tel Aviv, Israel na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 juzi usiku. **HABARI UK.30**

# KASEJA AIONA TAIFA STARS AFCON 2021

## ●●● Asema sasa ni mwendo wa kupambana mwanzo mwisho, kila mchezaji katika kikosi cha Ndayiragije...

**Na Somoe Ng'itu**

KIPA chaguo la kwanza wa timu ya soka ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Juma Kaseja, amesema watapambana kwa nguvu zote hadi mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi kwa lengo la kuhakikisha wanakata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2021.

**Taifa Stars iliyoko chini ya kocha Etienne Ndayiragije, jana usiku ilishuka dimbani nchini Tunisia kuikabili Libya katika mchezo wa pili wa Kundi J wa kuwania tiketi ya kushiriki fainali hizo zitakachezwa nchini Cameroon.**

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuingia uwanjani jana, Kaseja, alisema wachezaji wa timu hiyo wanataka kuona Taifa Stars inashiriki kwa mara ya pili mfululizo kwenye fainali hizo kubwa, kwa sababu wanahitaji kuendeleza rekodi safi kwa timu hiyo.

Kaseja alisema wachezaji wengi walioko katika kikosi hicho wana ndoto za kucheza fainali hizo za Afcon na ili wapate nafasi ya kushiriki, wanatakiwa kupambana na wanaamini inawezekana.

"Tutapambana hadi mwisho, tunajua si kazi nyepesi, lakini kwa pamoja hakuna kitakachoshindikana, tunajiandaa na kujiweka tayari," alisema Kaseja, kipa huyo wa zamani wa Moro United, Simba, Yanga, Kagera Sugar na KMC FC, zote za hapa nchini.

Kaseja aliongeza kuwa kila mechi kwao ni sawa na fainali, hivyo hawatadharau mpinzani yeyote wanayekutana naye.

"Mechi zote tutacheza kwa nguvu na kasi inayofanana, tunajua wapinzani wetu pia wanajipanga kupata matokeo mazuri kila tutakapokutana nao, tunamuomba Mungu atuongoze kupata pointi iwe nyumbani au ugenini," Kaseja alisema.

Alisema pia anaendelea kumshukuru Ndayiragije kwa kumwamini na kumpa nafasi katika kikosi chake ambacho tayari kimeshapata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa ndani (CHAN), zitakazofanyika Aprili mwakani nchini Cameroon.

Kaseja ambaye alikuwa nje ya kikosi cha Taifa Stars kwa miaka sita, amechukua namba ya Aishi Manula wa Simba ambaye alikaa langoni katika mechi zote za kusaka tiketi ya kushiriki fainali zilizopita za Afcon na michezo mwili dhidi ya Senegal na Kenya huku Metacha Mnata akidaka katika mchezo dhidi ya Algeria. Katika mechi ya awali ya kuwania ya Kundi J kuwania kufuzu Afcon 2021, Stars ilitokea nyuma na kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Equatorial Guinea iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mchezo wa jana Libya iliikaribisha Stars nchini Tunisia kutokana na kuwapo kwa machafuko ya kisiasa nchini kwao, jambo ambalo Shirikisho la Soka Afrika (Caf), lilihofia usalama wa wachezaji na kuwataka wenyeji hao kuchagua uwanja watakaoutumia nje ya nchi.

# Simba sasa yafunguka wakuondoka

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wachezaji wawili wa Simba, Rashid Juma na Saidi Ndemla wakitakiwa kwa mkopo kuelekea kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili mwezi ujao Desemba 16, klabu hiyo imetoa masharti mazito kwa timu zinazohitaji nyota wao.

Klabu ya KMC ya Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam inamuwinda dogo Rashid wakati Singida United ipo mawindoni ikihitaji huduma ya Ndemla ili kujinusuru na wimbi la kushuka daraja.

Lakini Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa, amesema klabu yao itaweka masharti ya kuhakikisha mchezaji wao analipwa na timu husika kwa kiwango kile kile anacholipwa Simba kwa timu zinazowahitaji kwa mkopo katika dirisha dogo.

Mazingisa amesema Simba haitoruhusu klabu itakayomsajili mchezaji wake kumlipa mshahara ambao ni tofauti na wanaomlipa klabuni hapo.

Kocha wa Singida United, Ramadhan Nsanzurwimo ameonyesha nia ya kumsajili Ndemla ili akaokoe jahazi ambalo linaelekea kuzama wakati huu wakibuzura mkia kwenye Ligi Kuu wakiwa na pointi nne baada ya kushuka dimbani mara 11.

Kwa upande wa KMC iliyopo nafasi ya 16 ikiwa na pointi nane baada ya kushuka dimbani mara nane, uongozi wa klabu hiyo umeelezwa kuhitaji kwa udi na uvumba huduma ya Rashid ambaye naye hana nafasi katika kikosi cha kwanza cha Simba kama ilivyo kwa Ndemla.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002